# Nipashe

Jumatano Desemba 18, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580104

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710









## Mkulima afariki dunia baada ya kuonja sumu

UKURASA 10

# DAR YASIMAMA

## MAFURIKO yafunga barabara, nyumba zaanguka, TMA yaonya...*Endelea ukurasa wa 2*



Eneo la Jangwani jijini Dar es Salaam ambalo limejaa maji kutokana na mvua kubwa iliyonyesha jana, na kukwamisha magari kupita. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

## YALIYOMO


**UKURASA WA 2**

**WANAFUNZI WAFA MAJI WAKIOGELEA**

WANAFUNZI wawili wa Shule ya Msingi Mwakitolyo wilayani Shinyanga, wamefariki dunia...

**UKURASA WA 4**

**MKEMIA MKUU ATOA USHAHIDI KORTINI KESI 68**

MAMLAKA ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) Kanda ya Nyanda...

**UKURASA WA 5**

**HESLB YATOA UFAFANUZI WANUFAIKA WA MIKOPO**

BODI ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), imewataka wanafunzi...


## MTOTO AGONGWA MSAFARA WAZIRI

UKURASA 3

## Mbowe awajibu wanaohoji gharama ukumbi uchaguzi

UKURASA 2







**MICHEZO** **SIMBA, YANGA RASMI MTOANO MAPINDUZI** UK. 32

**MAONI, KATUNI UK.6**

# Dar yasimama

**Na Moshi Lusonzo**

MVUA kubwa iliyonyesha Dar es Salaam jana ilisababisha kusimama kwa shughuli za uzalishaji jijini humo kutokana na mafuriko huku baadhi ya nyumba zikianguka.

Mvua hiyo ambayo ilianza kunyesha majira ya saa 11 alfajiri ikisababisha mito kujaa, baadhi ya barabara kufungwa na watu kuhama makazi yao baada ya maji kufurika na kuhatarisha maisha yao.

Maeneo yaliathirika zaidi kwa mujibu wa ushuhuda wa Nipashe ni pamoja na Jangwani ambalo karibu kila msimu wa mvua limekuwa likikumbwa na mafuriko.

Mengine ni Sinza, Kigogo Mbuyuni, Mtoni, Tandale kwa Mtogole, Kariakoo, Posta, Vingunguti na Mwenge.

Waandishi wa Nipashe walishuhudia baadhi ya wakazi wa jiji hilo wakikimbia makazi yao na wengine wakijaribu kuokoa baadhi ya mali zao kwa kuzihamishia pembeni mwa barabara zinazopita jirani na makazi yao.

Katika eneo la Mwenge, Nipashe ilishuhudia ukuta mkubwa ulio pembeni mwa Barabara ya Bagamayo (kushoto unapotoka Bagamoto kwenda Posta) ukiwa umeanguka kutokana na mafuriko.

Pia, maji yalikuwa yamefurika kwenye barabara mpya inayojengwa kutoka Makumbusho hadi Mwenge. Ujenzi huo unafanywa kwa lengo la kuifanya Barabara ya Bagamoyo kuwa ya njia sita.

**MTO NG'OMBE TISHIO**

Nipashe pia ilishuhudia wakazi waliojenga pembeni mwa Mto Ng'ombe maeneo ya Sinza, Tandale kwa Mtogole hadi Kinondoni Mkwajuni, wakishindwa kuokoa mali zao baada ya mto huo kujaa maji na kuangusha baadhi ya nyumba.

Waandishi wetu walishuhudia nyumba yenye vyumba vitatu eneo la Mtogole ikisombwa na maji na kusababisha watu waliokuwa wakiishi, kulazimika kupewa hifadhi kwa majirani.

"Maji yamekuja kwa kasi sana, kwa muda mfupi tu nyumba zetu zote zilizopo hapa zimezingirwa, tumeshindwa kuokoa mali zetu, tulichokifanya ni kuchukua familia zetu na kukimbilia huku juu kwa usalama wetu," alisema Yusuph Mlamali, mkazi wa eneo hilo.

Nipashe pia ilishuhudia huduma za usafiri kupitia Barabara za Shekilango na Kawawa zikisitishwa kwa muda baada ya madaraja ya Mugabe na Kinondoni kufurika maji hadi juu.

**KIGOGO HAKUKALIKI**

Wakazi wa maeneo ya Kigogo Mbuyuni pia waliamua kugeuza vibanda vya mama lishe na maduka kama makazi yao ya muda kutokana na nyumba zao kuzingirwa na maji.

Nyumba zilizojengwa pembeni mwa Mto Msimbazi zilionekana zikiwa zimejaa maji yaliyokuwa yamefika usawa wa madirisha na hakukuwapo dalili za kuwapo watu wa kuokoa mali zilizokuwamo ndani.

**JANGWANI KAMA BAHARI**

Eleo la Jangwani ambako kuna maegesho ya mabasi ya mwendokasi, kulikuwa kumegeuka kuwa kama bahari kutokana na maji ya mafuriko kujaa na kusababisha kusitisha huduma ya usafiri huo.

INAENDELEA UK 8




Meneja Masoko wa Kampuni ya Tanfix Quality Choice, Frank Kizito (kushoto), akiwa katika mahojiano na Mtangazaji wa East Africa Televisheni, Samson Charles, katika kampeni ya Kibiashara Zaidi ya East Africa Television na East Africa Radio, ameelezea jinsi ambavyo bidhaa wanayozalisha ya 'Tiles Glue' inasaidia kuunganisha tiles bila kutumia saruji na mchanga. **MPIGAPICHA WETU**

# Wanafunzi wafa maji wakiogelea

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

WANAFUNZI wawili wa Shule ya Msingi Mwakitolyo wilayani Shinyanga, wamefariki dunia walipokuwa wanaogelea kwenye mbuga ya Mahiga iliyokuwa imejaa maji kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha.

Tukio hilo lilitokea juzi majira ya saa moja asubuhi, wakati wanafunzi hao, Mihayo Chalres (12) na Kulwa Seheli (12), walipokuwa wakiogelea.

Taarifa iliyotolewa jana na Kaimu Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Sophia Jongo, ilieleza kuwa wanafunzi hao walifariki dunia kwenye maji hayo baada ya kuzama kwenye kina kirefu na kukosa hewa.

Alisema chanzo cha tukio hilo ni wanafunzi hao kutochukua tahadhari wakati wakiogelea kwenye mbuga hiyo iliyojaa maji.

"Miili ya wanafunzi hao wawili tulifanikiwa kuiopoa ndani ya maji, daktari wa serikali aliifanyia uchunguzi na kutoa majibu kuwa walifariki dunia kutokana na kukosa hewa pindi walipozama kwenye maji," alidai.

Jongo alisema miili ya wanafunzi hao imekabidhiwa kwa wazazi wao ili kuendelea na taratibu za mazishi, huku akitoa wito kwa wanafunzi na wananchi kuchukua tahadhari mapema kwenye kipindi hiki cha mvua, kuacha kuchezea sehemu hatarishi au kuvuka barabara na mito iliyojaa maji.

# Mbowe awajibu wanaohoji gharama ukumbi uchaguzi

**Na Enock Charles**

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe, ametetea uamuzi wa chama hicho kufanyika mikutano yake katika ukumbi wa Mlimani City jijini Dar es Salaam, akieleza kuwa Chadema ni ya viwango, hivyo kustahili kufanyika mikutano katika eneo hilo.

Akizungumza na wajumbe wa Baraza Kuu la chama hicho jana, Mbowe aliwashangaa watu kadhaa wanaohoji gharama za kukodi ukumbi wa Mlimani City, na kueleza kuwa yeye kama Mwenyekiti anaamini katika vitu vya viwango, hivyo haoni tatizo kwa chama hicho kukodi ukumbi wa gharama kufanyia mikutano yake.

"Kuna watu wanasema ooh mnafanyia mikutano kwenye maeneo ya ghali Mlimani City, mimi Mwenyekiti wenu nasema sisi ni watu wa viwango, Chadema tunaamini umasikini ni laana sio sifa," alisema Mbowe.

Chama hicho kimekuwa kikifanyia mikutano yake ikiwamo ya uchaguzi wa mabaraza katika ukumbi wa Mlimani City tangu kuanza kwa chaguzi hizo zinazotarajiwa kufika tamati leo kwa kumchagua Mwenyekiti wa chama Taifa na makamu wenyeviti baada ya kumaliza chaguzi za mabaraza hivi karibuni.

Wanachama na wafuasi wa Chadema kutoka maeneo mbalimbali nchini wamepiga kambi eneo la Mlimani City Jijini Dar es Salaam, huku bendera za chama hicho zikipepea eneo hilo.

Ingawa gharama halisi ambazo Chadema imetumia kukodi ukumbi huo kwa ajili ya mikutano yake hazikuwekwa wazi, lakini Mlimani City ni miongoni mwa kumbi ambazo zina gharama kubwa jijini Dar es Salaam.

Nipashe ilipomuuliza Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Chadema, Tumaini Makene, hakuwa tayari kuziweka wazi gharama walizotumia, zaidi ya kueleza kuwa chama kiliukodi ukumbi huo kuanzia Desemba 7 hadi leo.

Katika hatua nyingine, Mbowe ameahidi



kuanzisha mfumo mpya wa mawasiliano wa chama hicho unaojulikana kama 'Chadema Digital' sambamba na kuendelea kudumisha umoja ndani ya chama hicho.

Kwa upande wake, Cecil Mwambe, ambaye pia anawania nafasi ya uenyekiti wa chama hicho, ameahidi mambo makubwa manne iwapo atachaguliwa, ikiwamo kujenga ofisi za kisasa za chama hicho na kuachana na ofisi za kupanga alizodai zinakigharimu fedha nyingi chama hicho Kikuu cha Upinzani nchini.

HABARI KITAIFA

# Afa kwa kugongwa na gari msafara wa waziri

Na Suleiman Rashid Omar, PEMBA

SAIDI Suleiman Omar (15), amefariki dunia baada ya kugongwa na gari lililokuwa kwenye msafara wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, George Simbachawene, kisiwani Pemba.


Ajali hiyo ilitokea eneo la Masota Shengejuu wakati msafara huo uliokuwa ukitoka Chake Chake kwenda Njuguni wilayani Wete kukagua mradi wa kisima cha maji safi na salama.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kaskazini Pemba, Shekhan Mohamed Shekhan, alidai kuwa wakati msafara huo ulipofika eneo la Masota Shengejuu, mtoto huyo alikatisha ghafla na dereva kushindwa kumkwepa ndipo alipomgonga na kupoteza maisha papohapo. Kamanda Shekhan alidai kwa sasa wanamshikilia dereva wa gari hilo, Omar Mohamed Abdalla (34), mkazi wa Pondeani, Chake Chake kwa ajili ya uchunguzi zaidi wa tukio hilo.

Alisema dereva huyo alikuwa akiendesha gari aina ya Suzuki Scord lenye namba za usajili SMZ 895 A na wanaendelea kumhoji ili kujua kama ajali ya kawaida au kuna uzembe kabla ya kumfikisha mahakamani.

Kutokana na ajali hiyo, Waziri Simbachawene alilazimika kukatisha ziara yake na kwenda moja kwa moja hadi nyumbani kwa familia ya mtoto huyo kutoa pole. Baba wa mtoto huyo, Suleiman Omar, alisema tukio hilo ni mipango ya Mungu, hivyo hana sababu ya kuwa na kinyongo na mtu yeyote.

Alieleza kuwa mtoto wake huyo alikuwa anasoma Dar es Salaam na alirejea Pemba mwezi huu kwa ajili ya mapumziko ya mwishoni mwa mwaka.




## Washtakiwa mauaji ya Dk. Mvungi waijia juu Jamhuri

Na Hellen Mwango

WASHTAKIWA wa kesi ya mauaji ya aliyekuwa Mjumbe wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba, Dk. Sengondo Mvungi, wameujia juu upande wa Jamhuri kwa kucheleweshà upelelezi wa kesi yao kwamba wanateseka kukaa mahabusu.

Walitoa malalamiko hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi, Vick Mwaikambo, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam.

Awali Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo haujakamilika aliiomba mahakama kupanga tarehe nyingine ya kutajwa.

Hata hivyo, mshtakiwa Longishu Losindo, aliomba ruhusa ya kuzungumza mahakamani na alipokubaliwa, alidai kuwa kwanini kesi hiyo inakwama kuendelea wakati walishafikishwa Mahakama Kuu na wakafutiwa mashtaka, lakini baadaye walifunguliwa upya mashtaka.

"Mheshimiwa Hakimu, kesi hii ilifika Mahakama Kuu, lakini ilifutwa kwa kifungu cha 91 ikaletwa tena hapa Kisutu, tunashangaa kusikia kila tunapokuja kwamba upelelezi bado tunaomba tuelezwe kile wanachokipeleleza ni nini miaka saba sasa tupo mahabusu," alidai Losindo.

Akijibu hoja hizo, Wankyo alidai kuwa hawezi kuelezea masuala ya kiupelelezi kwa kuwa haujakamilika, na kwamba mpaka awasiliane na askari anayepeleleza.

Alidai, wiki ijayo watakuwa na ziara ya kutembelea mahabusu gerezani, hivyo majibu ya maswali yao yote watayapata huko.

Hakimu alisema kesi hiyo itatajwa Desemba 31, mwaka huu na kuamuru washtakiwa wote warudishwe mahabusu.

Washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni, Msigwa Matonya, Mianda Mlewa, Paulo Mdonondo, Juma Kangungu na John Mayunga.

Katika kesi ya msingi, washtakiwa hao kwa pamoja wanakabiliwa na shtaka la mauaji ambapo inadaiwa Novemba 3, mwaka 2013 walifanya kosa la mauaji ya kukusudia kinyume cha kifungu cha 196 cha sheria na kanuni ya adhabu sura ya 16 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2002.

Ilidaiwa kuwa siku hiyo ya tukio, katika eneo la Msakuzi Kiswegere, Wilaya ya Kinondoni, washtakiwa hao walimuua kwa kukusudia Dk. Mvungi, ambaye alikuwa mjumbe wa kamati kuu ya NCCR-Mageuzi.

HABARI KITAIFA

# Bonite yazawadia washindi wake

**Na Moshi Lusonzo**

WASHINDI 45 wamekabidhiwa zawadi mbalimbali na kampuni ya vinywaji ya Bonite ikiwamo pikipiki na televisheni katika droo ya mwisho ya kuwashindanisha wafanyabiashara wanaonunua bidhaa ya maji ya Kilimanjaro.

Hafla ya kukabidhi zawadi hizo ilifanyika jana jijini Dar es Salaam na kufanya jumla ya wafanyabiashara 90 walionufaika katika shindano hilo la wiki nane lililoanza Oktoba 7, mwaka huu.

Akizungumza kabla ya kutoa zawadi, msimamizi wa mauzo na masoko wa Kampuni ya Bonite inayozalisha bidhaa za vinywaji, Joseph Semali, alisema wameamua kutoa zawadi hizo kwa wanunuzi wakubwa wa maji ya Kilimanjaro kama njia ya kutoa shukrani kwa jamii.

"Kampuni ya Bonite ambayo inazalisha maji ya Kilimanjaro na vinywaji jamii ya Cocacola, imefurahi kuona imetimiza jukumu lake la kuwa pamoja na wateja wake na kurudisha shukrani kwa kuwapatia zawadi mbalimbali. Naamini kutokana na shindano hili tumekuwa karibu na jamii," alisema Semali.

Adha, alisema katika shindano hilo washindi walipatikana 15 katika makundi matatu, na walikabidhiwa pikipiki na kisasa, seti moja ya televisheni na maji katoni 50.

"Kila kundi walipata zawadi zao husika, tunachokifanya kwa walioshinda pikipiki tunabadilisha kadi ya umiliki kisha tutawapelekea katika maeneo yao ya biashara haraka iwezekanavyo," aliongeza.

Jaqueline Kasanda, ambaye alikabidhiwa pikipiki, alisema kitendo cha kampuni hiyo kuwakumbuka wateja wake ni jambo zuri, na kwamba umewapa ari ya kufanya kazi kwa juhudi kubwa.

"Nafurahi sana kuona Bonite kutukumbuka kwa kutupatia chombo hiki cha usafiri, biashara yangu itazidi kupanuka kwa kuongeza nguvu ya kuwafikia wateja wangu kwa haraka," alisema Jaqueline.

Naye Magili, ambaye alipata TV, alisema pamoja na chombo hicho kuboresha maisha yake na familia kwa ujumla, imesaidia kutambua umuhimu wake kwa kampuni hiyo katika suala la ujasiriamali.

# Simanzi maziko ya wanandoa

**Na Gurian Adolf, KATAVI**

VILIO, majonzi na simanzi jana vilitawala katika makaburi ya Nsemulwa Manispaa ya Mpanda mkoani Katavi wakati wa maziko ya wanandoa Noel Mswanya (39) na mkewe Stella Noel(37) walipokuwa wakizikwa baada ya kuuawa kwa kuchinjwa na watu wasiojulikana.

Wanandoa hao waliuawa kikatili kwa kuchinjwa na watu hao waliovamia nyumbani kwao usiku wa Desemba 15, wakiwa wamelala.

Wanandoa hao walizikwa katika makaburi tofauti, huku mamia ya wakazi wa mtaa wa Migazini na kitongoji cha Nsemulwa wakiwa wamejitokeza kuwasindikiza katika safari yao ya mwisho duniani.

Wakati wa mazishi hayo, baadhi ya waombolezaji akiwamo Maria Kilesha, mkazi mkazi wa mtaa wa Mgazini, alisema tukio hilo limeacha hofu kubwa kwa kwao kutokana na lilivyotokea, ambapo watuhumiwa walitumia muda mrefu kutekeleza tukio hilo bila kuwa na hofu.

Alisema anaviomba vyombo vya ulinzi na usalama kuwa makini muda wote kuhakikisha kuwa vinadhibiti vitendo hivyo ambavyo vikiachwa kuendelea kujitokeza vitasababisha watu kukata tamaa na kuwa na hofu zaidi.

Naye John Kaswaya, mmoja wa watu waliohudhuria maziko hayo, aliliomba Jeshi la Polisi kuwasaka watu waliofanya mauaji hayo ya kinyama ya wanandoa hao ili sheria ichukue mkondo wake kwani hata kama kulikuwa kuna suala la kulipiza kisasi, walichofanyiwa hakivumiliki.

Kwa mujibu wa Kaimu Kamanda wa Polisi mkoani Katavi, Leonard Makona, wanandoa hao wakiwa wamelala nyumbani kwao ndipo watu wasiojulikana walivunja mlango wa nyumba kwa kutumia jiwe kubwa maarufu kwa jina la 'Fatuma' na kufanikiwa kuingia ndani katika chumba walichokuwa wamelala kisha kuanza kuwachinja wanandoa hao.




Msimamizi wa Mauzo wa Kampuni ya Bonite Bottlers Ltd, Joseph Semali, akimkabidhi Hyness Amasonu funguo za pikipiki baada ya kushinda katika droo ya shinda pikipiki na maji ya Kilimanjaro katika sherehe za kuwazawadia washindi jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**




# Mkemia Mkuu atoa ushahidi kortini kesi 68 nyanda za juu

**Na Augusta Njoji, MBEYA**

MAMLAKA ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, imekusanya sampuli 2,580 na kuzifanyia uchunguzi na kutoa ushahidi mahakamani kwenye kesi 68 katika miaka minne ya serikali ya awamu ya tano.

Kati ya sampuli hizo, 221 zilikuwa za vinasaba (DNA) ambazo zililenga masuala ya kibinadamu ya utambuzi.

Kauli hiyo ilitolewa jana na meneja wa kanda hiyo, Gaspar Gerald, alipozungumza na waandishi wa habari waliofuatana na maofisa habari wa taasisi zilizoko chini ya Wizara ya Afya katika kampeni ya 'Tunaboresha Sekta ya Afya' inayolenga kuangalia mafanikio yaliyopatikana kwa kipindi cha miaka minne ya serikali ya awamu ya tano.

Meneja huyo alisema sampuli hizo 2,580 ni za kimazingira, makosa ya jinai, vinasaba, chakula na dawa.

Alisema katika ukanda huo kwa kipindi cha miaka minne wametoa ushahidi kwenye kesi 68, akifafanua kwamba siyo kila sampuli zinazopimwa zinatolewa ushahidi bali ni zile zinazohitajika kutolewa ushahidi mahakamani.

"Huu ushahidi ni pale mahakama inapohitaji ushahidi ndo tunaenda kutoa na ushahidi tunaotoa ni kile tulichokiona kwenye sampuli iliyoletwa kama vile dawa za kulevya, hivyo mkemia anatoa ripoti yake," alisema.

Akizungumzia kuhusu mafanikio mengine, Gerald alisema wamefanikiwa kujenga ofisi yao kwa gharama ya Sh. milioni 300, kukagua na kudhibiti kemikali na kuongeza ka wafanyakazi kutoka watatu hadi 18.

"Mwaka 2017, wafanyakazi waliongezeka kwa asilimia 80 na inatokana na juhudi za Rais John Magufuli kuhakikisha anatekeleza sera ya serikali ya kufikisha huduma kwa wananchi, ukanda huu kijiografia una mikoa sita, lakini kiutawala kwa mujibu wa Mkemia Mkuu wa Serikali ni mikoa mitano ya Njombe, Songwe, Mbeya, Katavi na Rukwa," alisema.

Alieleza kuwa huduma zinazotolewa ni pamoja na uchunguzi wa kimaabara, utekelezaji wa sheria ya mamlaka ikiwamo ya kemikali za majumbani na viwandani, vinasaba vya binadamu na Sheria ya Mkemia Mkuu.

Aliongeza kuwa ofisi hiyo imefanikiwa kusimamia kemikali na kudhibiti zinazoingia mipakani kupitia Mpaka wa Tunduma na Kasumulu na kutoa elimu kwa watu zaidi ya 150 wanaojihusisha na kemikali na watu 140 wanaotoka Jeshi la Polisi kwa ajili ya usimamizi wa sampuli za jinai.

Gerald alisema udhibiti wa kemikali awali hakuwa mzuri, lakini baada ya mamlaka hiyo kuanzishwa udhibiti, umekuwa mkubwa na wasafirishaji wamepewa elimu ili kufuata taratibu za kulinda mazingira na afya za watu.

Kuhusu DNA, meneja huyo alisema vinasaba vinapimwa kwa maana mbili ya utambuzi na masuala ya jamii au ya ndoa. "Kwenye Sheria ya DNA, imeanishwa mamlaka inayoomba kupimiwa DNA, ile mamlaka ndiyo inayoleta maombi kwa mkemia kuomba kupimiwa DNA, hakuna uoga, watu wanafuata taratibu. Kwa mfano, tukio la moto Morogoro pale mkemia aliingia kujua huyu ni nani," alifafanua.



## Waziri azibana halmashauri mgawo mapato ya tozo, faini

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Sima, amezitaka halmashauri zote nchini kugawa tozo na faini zote zinazopatikana kwenye mapato ya ndani kulingana na mpangokazi wa maofisa mazingira waliopo kwenye halmashauri husika.

Alitoa agizo hilo alipohudhuria maadhimisho ya wiki ya usafi wa mazingira na mkutano wa maofisa afya wa mikoa, halmashauri na wadau ulioandaliwa na Wizara ya Afya jijini Dodoma jana.

"Mgawanyo lazima uende kwenye usafi na mazingira na mgawanyo ambao hauendi kwenye usafi na mazingira, sisi tutatembea na kusimamia hili," alisema.

Aliongeza kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais ndiyo yenye jukumu la kulinda, kusimamia na kuhifadhi mazingira na kusisitiza kuwa wapo maofisa mazingira kuanzia ngazi ya kijiji na kamati za Mazingira.

Aliwataka maofisa afya kuwa na ushirikiano na kamati za mazingira zilizoko kwenye ngazi za chini za serikali za vijiji, kata na wataalamu wa mazingira walioko katika mikoa na wilaya.

Katika warsha hiyo, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, alisema ni muhimu kuhamasisha vijana kujenga vyoo bora katika kila kaya ili kulinda afya na kuepuka magonjwa mbalimbali na kulinda mazingira.

Aliwataka wataalamu wa eneo hilo katika halmashauri zote nchini kutimiza wajibu wa kujenga vyoo, akiitolea mfano Wilaya ya Njombe ambayo imepiga hatua kubwa katika ujenzi wa vyoo bora kwa kila kaya, ikiwa imefikia asilimia 96.

"Taarifa ya World Bank (Benki ya Dunia) inaonyesha watu wanapoteza saa 58 kwa mwaka sababu ya kutokuwa na vyoo. Hivyo basi, wananchi wanatakiwa kufikiria kupoteza hizo saa 58 badala ya kufanya shughuli za kujiingizia kipato na kuinua uchumi wa nchi yetu," alisema.

Waziri Ummy pia aliunga mkono mapendekezo ya Naibu Waziri Sima katika suala la ushirikiano kati ya maofisa afya na mazingira walioko katika halmashauri na miji.

# HESLB yatoa ufafanuzi wanufaika mikopo

**Na Mwandishi Wetu**

BODI ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) imewataka wanafunzi wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu ambao wanakutana na changamoto mbalimbali kuwasiliana na menejimenti za vyuo vyao ili ziwasilishwe HESLB na kupatiwa ufumbuzi wa haraka.

Bodi hiyo imetoa ufafanuzi huo kufuatia maoni na malalamiko yaliyotolewa na wanafunzi wa vyuo mbalimbali, kikiwamo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (CKD) kuhusu malipo ya fedha za vitabu na viandikwa na malipo ya chakula na malazi kwa wanafunzi waliobadilisha kozi.

Taarifa iliyotolewa na bodi hiyo jana na kusambazwa kwenye vyombo vya habari ilisema, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya HESLB, Prof. William Anangisye, alitoa ufafanuzi huo Jumatatu, jijini Dar es Salaam katika kikao cha pamoja kati yake, menejimenti ya HESLB, menejimenti ya CKD na wawakilishi wa viongozi wa wanafunzi wa CKD.

"Wanafunzi wote wa taasisi za elimu ya juu wanapokutana na changamoto wasisite kuziwasilisha kwa menejimenti za vyuo ambavyo vitaziwasilisha HESLB au kwa taasisi sahihi, hata nyie mlipaswa kuanzia kwetu na tungeyafanyia yote kazi badala ya kutoa maelekezo ya saa 72," alisema Prof. Anangisye ambaye ni Makamu Mkuu wa CKD.

Kikao hicho pia kilihudhuriwa na Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abdul-Razaq Badru, Naibu Makamu Wakuu wa CKD, Prof. Killian Bernadetha (Utafiti), Prof. David Mfinanga (Utawala), wawakilishi wa serikali ya wanafunzi CKD na watendaji wengine wa CKD na HESLB.

Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Badru alisema kwa sasa HESLB inakamilisha malipo ya fedha za wanafunzi waliobadilisha kozi ambayo yamepokelewa na HESLB kutoka Tume ya Vyuo Vikuu (TCU), mwishoni mwa wiki na fedha hizo zitawafikia wanafunzi leo.

"Kuna kundi la wanafunzi waliobadilisha kozi wakiwa vyuoni na taarifa hizo zilikua hazijatufikia, tumezipokea mwishoni mwa wiki na tunakamilisha malipo yatawafikia siku mbili zijazo (Desemba 18)," alisema Badru na kufafanua:

"Kwa mujibu wa Badru, kundi jingine linahusu malipo ya vitabu na viandikwa, malipo ya awamu ya kwanza ya jumla ya Sh. bilioni 13.3 yameshafanyika na awamu ya pili ya Sh. bilioni 1.1 itawafikia wanafunzi Jumamosi ijayo, Desemba 21 kwa kuwa wataalamu wetu wanakamilisha uchambuzi," alisema.

Kwa upande wao, viongozi wa wanafunzi walioongozwa na Hamis Mussa, walishukuru kwa kupata fursa na kuwasilisha masuala yao na kupata ufafanuzi.

Hadi sasa, jumla ya wanafunzi 49,485 wa mwaka wa kwanza wameshapata mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 169.4 na kuvuka lengo la kutoa mikopo kwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza wapatao 45,000.

Kati yao, wanafunzi yatima waliopoteza mzazi au wazazi wote wawili ni 10,383, wenye ulemavu (397), waliofadhiliwa masomo ya sekondari (3,128) na wengine wahitaji 35,577.

Wanafunzi 78,337 wanaoendelea na masomo wamepata mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 272.1.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tuepuke simu barabarani kupunguza ajali sikukuu

**HUU** ni msimu wa sikukuu ambao kama taifa tunalazimika kuchukua tahadhari zote kuwaepusha wananchi na ajali zinazosababisha vifo, uharibifu wa mali na njia za usafiri.

Katika moja ya taarifa kubwa zilizochapishwa na gazeti hili Jumatatu wiki hii ni tahadhari kwa serikali na wadau wa usalama barabarani kuendelea kuchelewesha sheria ya matumizi ya simu barabarani.

Kwa mujibu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano (TCRA) idadi ya wanaotumia simu nchini ni takribani milioni 40 na pengine kati ya wote hao madereva huenda wanatumia simu.

Idadi hiyo ni kubwa mno na bila udhibiti wa kisheria kuna uwezekano wa idadi kubwa ya watu kuangamizwa kutokana na matumizi ya simu barabarani.

TCRA inaeleza kuwa matumizi ya simu yanateka akili za watumiaji kiasi cha kuvuka barabara, huku wakiendelea kusikiliza au kusoma ujumbe na wengine wameweka visikilizio masikioni. Matokeo yake ni kupata ajali zinazosababishwa na gari au pikipiki na wengine kupoteza maisha.

Ndiyo maana sheria ya kudhibiti matumizi ya simu barabarani inahitajika haraka kwa lengo la kudhibiti, madereva, abiria na wanaotembea.

Kutokana na kutojali usalama na maisha imekuwa kawaida dereva wa basi anaendesha watu zaidi ya 50 kuongea na simu akiwa barabarani, kadhalika wa bodaboda na magari madogo naye hufanya hivyo.

Matokeo yake ni kusababisha ajali, ndiyo maana sheria ya udhibiti matumizi ya simu barabarani sasa ni lazima.

Kwa mataifa mengine kuna sheria za kutumia simu aidha kwa kuweka gari pembeni au kutoka nje ya gari na wakati mwingine kutumia kifaa kingine badala ya kuweka simu masikioni ambacho kwa kuendesha kwenye kiwango kidogo cha mwendo dereva anaweza kuzungumza.

Licha ya kwamba polisi wanasisitiza kuwa sheria iko mbioni na wamependekeza adhabu iwe Sh. 500,000 ikiwa dereva atakutwa anaendesha huku anatumia simu, ukweli ni kwamba Tanzania imechelewa kuandaa sheria hiyo.

Ni muhimu kuwa na sheria kali kwa kuwa matumizi ya simu hizo yamekuwa ni changamoto kubwa kwa kila mmoja hata wakati mwingine mlezi au mzazi anavuka barabara pamoja na watoto au mtoto lakini ameshikilia simu sikioni.

Si hivyo tu, wakati mwingine imetokea kuwa na misururu mirefu barabarani kutokana na watu kuchati na simu lakini wameweka visikilizio masikioni kiasi cha kuzuia kusikia hata honi au kelele nyingine zinazoendelea barabarani.

Tunapenda kuwakumbusha wadau kuwa msimu huu wa sikukuu ni hatari zaidi wakiwa barabarani na simu masikioni. Ni kwa sababu wapo wanaoendesha huku wanasikiliza muziki au kutizama picha, wapo wengine wanaoandika ujumbe, kupiga simu au kusaka namba za mawasiliano ndani ya vifaa hivyo.

Yote hayo ni hatari tena si kwao tu bali kwa wengine wakiwamo watembeao, wanaotumia vyombo vya moto, wenye ulemavu na watoto ambao huwa sehemu ya ajali hizo.

Kwa hiyo msimu huu wa sikukuu za Noeli na Mwaka Mpya ni wakati wa kukumbushana kwa kuweka ujumbe wa mabango barabarani wa kuwahimiza madereva kupunguza mwendo na kuachana na simu.


Tunaona kuwa ni vyema kuanza kukumbusha sasa kwa kuweka ujumbe huo kwenye mabango kwenye njia zote na pia kuwahimiza wanaotumia pikipiki kutumia kofia ngumu ili kuokoa maisha pale ajali zinapotokea.

Wakati mwingine ni vyema kuweka namba za polisi na TCRA ili abiria waripoti taarifa za uendeshaji mbaya unaoambatana na matumizi ya simu wakati mtu yuko kwenye usukani.

Kinga ni bora kuliko tiba. Tuanze sasa kukumbushana ili kuokoa maisha na kuepusha ajali.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Mkuu wa Mkoa Lindi ameanza, wengine je?



Na Sabato Kasika

**TANZANIA** imepiga hatua kwenye sekta ya elimu kwa kuweka mikakati mbalimbali ikiwamo kuanzisha na kuongeza shule za msingi na sekondari na serikali kugharamia elimu msingi hadi kidato cha nne.

Moja ya malengo ya kuwekwa kwa mikakati hiyo ni kutaka kila mtoto awe wa kike au wa kiume, kutoka katika familia maskini ama tajiri apate elimu.

Hayo yanafanywa, kutokana na ukweli kwamba katika dunia ya leo, ili mtu aweze kuboresha maisha yake ni lazima awe na elimu, kwani ndiyo inayompa kujitambua na kuendesha maisha yake.

Vilevile elimu inampa mamlaka ya kuzikabili changamoto zinazomsonga katika maisha yake ya kila siku na pia kuyatawala na kuyatumia mazingira yanayomzunguka, ili kuboresha maisha yake.

Hata hivyo, kumekuwapo na tatizo la mimba na ndoa za utotoni kwa wanafunzi wa kike, ambalo ni kikwazo kikubwa kwa maendeleo yao kielimu.

Mimba na ndoa hizo vinasababisha upatikanaji wa elimu kwa wote kukabiliwa na tatizo na huenda linazidi kuwa kubwa kwa vile jamii imejiweka pembeni katika vita ya kumaliza changamoto hiyo.

Lindi ni miongoni mwa mikoa inayokabiliwa na tatizo la mimba za utotoni ambalo, sasa mkuu wake wa mkoa, Godfrey Zambi, anawataka viongozi kuchukua hatua kuhusu tatizo la mimba za utotoni.

Katika kikao cha kujadili tatizo la mimba za utotoni kilichofanyika hivi karibuni, Zambi anasema, hadi kufikia Novemba mwaka huu, mkoa ulikuwa na mimba 151, huku 43 zikiwa za shule ya msingi na 108 za sekondari.

Wajumbe wa kikao hicho wanawataka wazazi kusimamia mienendo ya watoto wao kuanzia nyumbani, shuleni na katika jamii badala ya kuwaachia walimu na wanajamii ndiyo ifanye kazi hiyo na kusababisha watoto kukosa maadili.

Aidha, anaonyesha kukosa imani na mambo yanayofundishwa kwenye jando na unyago, na ameamua kabla ya unyago watoto wanaopelekwa wote waandikishwe kwa watendaji wa vijiji na mitaa.

Anasema kwamba msimamizi wa watoto hao afahamike, ili kumuona kama anafaa kukaa na watoto na kujua ni mambo gani wanakwenda kufundishwa na kufuatilia ufundishwaji wake, ili kama kutakuwa na upotoshaji yazuiwe.

Zambi anawaagiza viongozi katika ngazi zote mkoani humo kuwachukulia hatua wote wanaohusika na tatizo hilo na kuunda kamati za ulinzi wa mtoto kwa kila wilaya na kutoa elimu kwa wanafunzi kuhusu madhara ya mimba za utotoni na mambo mengine yanayoambatana na ngono utotoni.

Anawaagiza pia maofisa elimu na ustawi wa jamii kusimamia uanzishwaji wa klabu rika, katika shule na kwa shule ambazo klabu hizo zipo, basi ziimarishwe, ili kusaidia utoaji wa elimu rika kwa wanafunzi wa shule husika.

Hiyo ni baadhi ya mikakati ya kutokomeza mimba mkoani humo, halafu idadi hiyo ya mimba ni kwa mkoa mmoja tu, tatizo kama hilo hilo litakuwa la nchi nzima kutakuwa na wanafunzi wangapi wenye mimba? Nadhani kuna haja ya kuchukua hatua zaidi, ili kumaliza tatizo hili.

Ikumbukwe kuwa wasichana wanaokatisha masomo na kuharibu maisha yao, wamo ndani ya jamii na ni sehemu ya jamii, hivyo ni muhimu jamii ihusike katika kukomesha mimba na ndoa za utotoni.

Kwa hali ilivyo sasa, ipo haja kwa wazazi na walezi kuzungumza na kuwaelekeza, kuwafundisha maadili mema wakiwa wadogo ili yawe ngao yao ingawa inawezekana wakayaacha, lakini ni muhimu mzazi kutimiza wajibu.

Wazazi na walezi hawana budi kuwapa watoto elimu ya makuzi, kwani ni moja ya njia ya kuwaepusha tamaa, ambazo mwisho wa siku zinaweza kusababisha wapate mimba na kukatisha masomo bila kutarajia.

Suala hili la malezi linawagusa pia walimu, kwani wao ndiyo wanaokaa na wanafunzi muda mrefu na wanaona mabadiliko ya mwanafunzi kitaaluma, kitabia, kimwenendo na kimaadili.

Walimu wasiwe sehemu ya tatizo la mimba, kwani baadhi yao huwa wanatuhumiwa kufanya mapenzi na wanafunzi wao hali, ambayo ni kinyume na maadili ya kazi. Ni vyema kujirekebisha ili kuwa na mafanikio katika kampeni hii ya mkuu wa mkoa.

# HABARI PICHANI



Mabasi ya mwendokasi yakiwa yameegeshwa eneo la Magomeni Mapipa jijini Dar es Salaam, baada ya eneo la Jangwani kujaa maji.



Wananchi waliokwama kuvuka Mto Ng'ombe kuelekea Sinza Madukani wakiyaangalia maji ya mvua.



Wakazi wa eneo la Kigogo maarufu 'Kwa Dua Said', wakivuka barabara iliyojaa maji ya mvua na mengine kuingia majumbani mwao.



Wakazi wa Kigogo Mwisho wakitembea juu ya daraja baada ya kufungwa kwa muda magari kuvuka kutokana na mafuriko.



Sehemu ya ujenzi wa upanuzi wa barabara mpya ya Bagamoyo eneo la Bamaga likiwa limejaa maji ya mvua.



Foleni ya magari eneo la Magomeni Mapipa jijini Dar es Salaam iliyosababishwa na mvua kubwa iliyonyesha jana. **PICHA ZOTE SELEMANI MPOCHI**

HABARI KITAIFA

# Kiwanda noti bandia chanaswa

Na Anaeli Mbise

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, linawashikilia watu watatu kwa tuhuma za kuendesha kiwanda cha kutengeneza noti bandia, wakidaiwa kukutwa na noti zenye thamani ya Sh. milioni 500 zilizokuwa tayari kuingizwa kwenye mzunguko.

Akizungumza na waandishi wa habari jana kwenye mkutano ambao pia ulihudhuriwa na Gavana wa Benki Kuu (BoT), Prof. Florence Luoga, Kamanda wa Polisi wa kanda hiyo, Lazaro Mambosasa, alidai watuhumiwa hao walikamatwa katika eneo la Chanika, Temeke jijini.

Kamanda Mambosasa alidai kiwanda hicho kilikuwa kinatengeneza note za dola za Marekani, shilingi za Tanzania, kwacha za Malawi na DRC na fedha za Msumbiji.

"Tulipata taarifa kutoka kwa wasamaria wema na tukafanyia kazi taarifa hizo zilizofanikisha kuwakamata watuhumiwa hao ambao walikuwa wanahujumu uchumi wetu," Mambosasa alidai.

Alidai upatikanaji wa taarifa ya kiwanda hicho ulianza siku chache baada ya Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, kukamata zaidi ya Sh. milioni 11 ambazo zilikuwa za bandia.

Kamanda Mambosasa alidai watuhumiwa hao walikuwa wakitumia nyumba ya kuishi na hawakuruhusu watu wafike katika eneo hilo na kuona kitu kilichokuwa kinaendelea ndani ya nyumba hiyo.

"Mmoja wa watuhumiwa alikuwa anatumia gari la familia kutoka ndani na kwenda nje ili mtu asijue kitu ambacho kilikuwa kinaendelea ndani ya nyumba hiyo na lengo lake lilikuwa kufanya kazi zake kuwa siri," alidai. Kamanda huyo pia aliwaonyesha waandishi wa habari mashine ambazo watuhumiwa hao wanadaiwa walikuwa wakizitumia kutengenezea noti hizo ikiwa ni pamoja na mashine ya kuchapisha na kutolea nakala.

Hata hivyo, kamanda huyo hakuzungumzia muda ambao kiwanda hicho kimefanya kazi za kazi na idadi ya noti ambazo kimefyatua hadi wanawakamata watuhumiwa.

Awali, Gavana wa BoT, Prof. Luoga, alisema benki hiyo inajitahidi kupambana na kuzuia fedha bandia zisiingie katika mzunguko kwa kuwa itakuwa ni hatari kwa uchumi wa nchi.

"Hili ni kosa kubwa na kwa sababu sheria za Tanzania hazijawa kali sana, lakini hili ni hatari maana anayeumia ni mtumiaji wa chini kabisa," alisema.

Gavana huyo pia alisema watashirikiana na Jeshi la Polisi na vyombo vingine vya ulinzi ili kuelimisha umma juu ya masuala ya hayo.




Mkuu wa Kitengo cha T-PESA, Lulu Mkudde (kulia), akisaini hati ya makubaliano ya ushirikiano kibiashara na Mkuu wa Kitengo cha Biashara wa Halopesa, Magesa Wandwi (kushoto), jana jijini Dar es Salaam. Kwa makubaliano hayo hivi sasa wateja wa T-Pesa wataweza kutuma pesa kwenda mtandao wa Halopesa na vile vile wa Halopesa kutuma kwenda T-Pesa.

INATOKA UK 2

# Dar yasimama

Nipashe ilishuhudia askari polisi wakiwa wametanda upande wa Magomeni Mapipa na Fire kuzuia magari na watu wanaotumia Barabara ya Morogoro kukatiza eneo hilo.

Mabasi yaendayo kasi yanayotoka Kimara yalielekezwa kuishia Kituo cha Magomeni Mapipa na kisha kushusha abiria kabla ya kurudi mahali yalikotoka na yale yaliyotoka Kivukoni na Kariakoo yaligeuzia kituo cha Fire.

"Haturuhusu chombo chochote cha moto wala mtu kupita eneo hili," alisikika askari polisi akitoa maelekezo kwa watu waliotaka kupita kukatisha katika utepe mwekundu uliowekwa katika eneo la Magomeni Mapipa.

**TEMEKE NI VILIO**

Mafuriko pia yameyakumba maeneo mbalimbali ya Manispaa ya Temeke na kusababisha wakazi walioathirika kukaa nje ya nyumba zao.

Maeneo yaliyoripotiwa kuathiriwa na mvua hizo ni Temeke Sokota, Mtoni kwa Azizi Ali na watu wanaoishi katika ukingo wa Mto Kizinga na Mzinga.

**BIASHARA ZASIMAMA**

Maeneo ya kibiashara kama Kariakoo, Posta na Mwenge yalionekana kukimbiwa na wateja na baadhi ya maduka yalikuwa yamefurika maji na baadhi ya wamiliki walionekana wakitoa maji kwa ndoo kutoka kwenye maduka yao.

**ILIVYOKUWA MBAGALA**

Wakazi wa Mbagala Rangi Tatu walisema tabu waliyoipata ni katika kusaka usafiri kutokana na barabara nyingi kujaa maji, hivyo kutopitika huku sehemu zao za kufanyia biashara zikiwa zimeathiriwa kwa baadhi ya vibanda kusombwa na maji ya mvua.

Pia, maduka mengi katika mitaa ya Sinza yalikuwa yamefurika maji na kusababisha wamiliki wa maduka hayo kushindwa kuendelea na shughuli zao.

TAHADHARI TMA

Wakati huo, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), imetoa tahadhari kwa wananchi kufuatia mvua inayoendelea kunyesha katika maeneo mbalimbali nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini jana, Meneja wa Kituo Kikuu cha Utabiri wa mamlaka hiyo, Samuel Mbuya, alisema wananchi wanatakiwa kuchukua tahadhari ikiwa ni pamoja na kuepuka kukaa chini ya miti na kando ya mito.

Kwa mujibu wa mamlaka hiyo, mvua hiyo ni matokeo ya kuimarika kwa ukanda wa mvua Tanzania, uliosukumwa kaskazini kutokana na mkondo wa baridi katika ncha ya kusini ya Bara la Afrika.

Aliyataja maeneo mengine yaliyofikwa na mvua hiyo kuwa ni pamoja na Dodoma, Singida, Tanga, Pwani, kasikazini mwa Mkoa wa Morogoro na Visiwa vya Unguja na Pemba.

**KAULI YA POLISI**

Akizungumza na Nipashe, Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, alisema kuwa hadi jana jioni, hakukuwa na taarifa ya kifo cha binadamu kutokana na mvua hiyo.

Mambosasa alisema jeshi hilo lilijipanga vyema kuhakikisha katika maeneo yote hatarishi kunakuwa askari wake wanaofuatilia nyendo na kuzuia watu kwenda kwenye maeneo hatarishi.

"Jeshi linaendelea kufanya tathmini ya athari za mvua hii, tunawataka wazazi wahakikishe wanazuia watoto wao kukaribia madimbwi ya maji na mito iliyofurika," alisema.

***Imeandikwa na Juster Prudence na Moshi Lusonzo***

# Watetezi wa mtoto wajadili mimba za utotoni

Na Mwandishi Wetu

WATETEZI wa mtoto wa kike, viongozi wa dini na wabunge wamekutana jijini Dar es Salaam kujadili ndoa na mimba za utotoni, huku wakipendekeza Sheria ya kumlinda mtoto kabla haijapelekwa bungeni, makundi katika jamii yapewe fursa ya kutoa maoni yao ili kuwe na muafaka utakaokuwa na umoja.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti kwenye mkutano huo jana wadau hao walisema licha ya wanaharakati kushinda mahakamani kuhusu Sheria hiyo iliyokuwa ikiruhusu mtoto wa kike kuolewa chini ya miaka 18, lakini bado ipo haja Katiba nayo kubadilisha vipengele vyake kwenye eneo la mila na desturi ambazo ndizo changamoto inayosababisha baadhi ya familia kuoza watoto.

Mkurugenzi wa Miradi wa Shirika la Plan International, Peter Mwakabwale, alisema kwenye Katiba mama ilitakiwa ianze kwa kuzuia hilo.

"Uganda na Malawi Katiba zao zimeandikwa rasmi, suala hili likiwekwa kwenye Katiba yetu, litasaidia kuzifunga mila na desturi potofu zinazoruhusu mtoto wa kike kuolewa na umri chini ya miaka 18," alisema.

Pia alisema hata katika Sheria inaweza kuweka katazo na jamii kupewa elimu ya kutosha.

"Matarajio yetu katika kikao kijacho cha Bunge watapitisha sheria yenye katazo," alisema.

Kuhusu takwimu alisema zinaonyesha Shinyanga inaongoza kwa asilimia 59 ikifuatiwa na Tabora asilimia 57 kwa watoto kuozwa chini ya miaka 18.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria, Mohamed Mchengerwa, alisema ni jukumu lao suala hilo likifikishwa bungeni kulifanyia kazi kama mahakama itakavyoagiza.

"Kuhusu mila na desturi, msingi wa jambo hili ni kubwa linahitaji kuhusisha jamii ambayo ndiyo wanaotekeleza ikiwamo imani za dini.

"Hili siyo jambo dogo kama ambavyo watu wengine wanavyoweza kulichukulia, ni jambo kubwa linalotakiwa kufanyiwa utafiti, kuhusisha viongozi wa dini na wa kimila ili waridhie kule tunataka kwenda.

"Zipo sheria mbalimbali zinazokinzana na Katiba zipo zilizoweka utaratibu uliopo ambazo mahakama imeuona uboreshwe, ili kuweza kuzuia kwa mujibu wa Katiba yapo mambo mengi yanatakiwa kufanyika."

Mchengerwa alisema lazima utafiti ufanyike ili kuona namna gani wanaweza kuliepusha jambo hilo lisimuumize yeyote.

HABARI KITAIFA

## Daktari ataja mwarobaini magonjwa yasioambukiza

**Na Mwandishi Wetu, PEMBA**

JAMII kisiwani Pemba imeshauriwa kufanya mazoezi ili kuziweka afya zao sawa na kujiepusha kupata maradhi yasiyoambukiza ikiwamo shinikizo la damu na kisukari.

Ushauri huo ulitolewa na daktari mwenye dhamana Hospitali ya Chakechake, Ali Omar Khalifa, alipokuwa akizungumza na gazeti hili.

Alisema ufanyaji wa mazoezi unampa mtu fursa ya kuongeza muda mrefu bila kupata maradhi hayo.

Alifahamisha maradhi ya kisukari na presha yanawapa mzigo mkubwa wananchi kwa kupata ulemavu na hata kusababisha vifo, hivyo wakifanya mazoezi yatapunguwa kasi.

Alisema, maradhi hayo huchangiwa na mfumo wa maisha ya kujiendekeza ambao watu wamejiwekea maisha yao, ikiwamo ya kula sana bila ya kufanya mazoezi ambapo mfumo huo sio sahihi.

Alifahamisha kuwa mrundikano wa vyakula hatarishi mwilini ikiwamo mafuta mengi, sukari, chumvi pamoja na vinywaji kama pombe vinaathiri zaidi maisha ya watu.

"Idadi ya wagonjwa hawa imekuwa ikiongezeka siku hadi siku katika hospitali hii ya Chakechake na kwa mwezi hupata wagonjwa wapya wa kisukari watatu hadi wanne na kwa wagonjwa wa presha ni watano hadi sita," alisema.

Alisema, ufanyaji wa mazoezi si jukumu la mtu mmoja pekee bali ni la wote kwani maradhi hayo yanapompata mtu husababisha upofu, maradhi ya moyo, figo, kiharusi na kusababisha ulemavu.

Akizitaja dalili za maradhi hayo, alisema ni pamoja na kuumwa na kichwa, moyo kupiga sana, kizunguzungu, kichefuchefu, mwili kuwa mlegevu, kukosa usingizi wakati wa usiku, kula sana, kuona kiu na kukojoa mara kwa mara.

Baadhi ya wagonjwa waliishukuru serikali kwa kuwapatia dawa za maradhi hayo ambayo yanawasumbua walio wengi.

# TPA Ziwa Tanganyika yajipanga kifaida

**Na Elizabeth Zaya, KIGOMA**

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) kupitia bandari zake zilizopo katika Ziwa Tanganyika, imesema inatarajia kujiendesha kwa faida zaidi kufikia Juni mwakani kwa kukusanya mapato zaidi Sh. bilioni 7 kwa mwaka.

Hayo yalibainishwa na Meneja wa Bandari za Ziwa hilo, Percival Salama, wakati akizungumza na waandishi wa habari juu ya utendaji wa bandari zilizopo katika ziwa hilo kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita.

Alisema kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita kuanzia mwaka 2014/15 hadi 2018/19 bandari za ziwa hilo zimetengeneza faida ya mapato ya Sh. bilioni 18.

"Mwaka 2014/15 mapato yalikuwa Sh. bilioni 2.09, 2015/16 Sh. bilioni 2.66, 2016/17 Sh. bilioni 4.14, 2017/18 Sh. bilioni 5.69, mwaka 2018/19 Sh. bilioni 4.148, lakini mwaka 2019/20 tumepanga kukusanya Sh. bilioni 7.6 ambayo faida itakuwa Sh. milioni 400 na mpaka sasa tunaendelea vizuri," alisema Salama.

Alisema katika mwaka huu wanatarajia kuongeza wingi wa mizigo wanayoihudumia hadi kufikia tani 210,000 kutoka tani 199,831 ambazo zilihudumiwa mwaka 2018/19 na tani 100,000 zilizohudumiwa mwaka 2014/2015.

Alitaja mikakati ambayo wameweka ya kuwafikisha katika lengo la kujiendesha kwa faida kuwa ni kuongeza kasi ya kuhudumia shehena, kupunguza tozo za shughuli mbalimbali za kibiashara zinazofanyika katika bandari hizo.

"Zamani tulikuwa tunatumia muda mwingi kutoa mizigo katika meli hadi kufikia siku tatu, lakini kwa sasa tumejipanga, meli ikifika siku moja hiyo hiyo tunaihudumia kwa muda mfupi na mizigo yote inatoka," alisema.

Alisema mkakati mwingine wa kufikia lengo hilo ni kupitia uboreshaji mkubwa wanaoufanya katika bandari zake zote katika ziwa hilo.

Alisema zaidi ya Sh.bilioni 120 zimetengwa kwa ajili ya uboreshaji wa bandari zote zilizopo katika ziwa hilo.



Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri (kushoto) na Meneja Uhusiano na Mawasiliano wa JTI Leaf Services, Bright Kiwia, wakishuhudia namna Mkuu wa Wilaya ya Uyui, Gift Msuya, anavyootesha mti wakati wa kilele cha kampeni ya kampuni ya tumbaku ya upandaji miti kwa vyama vya msingi na wakulima mkoani Tabora kwa msimu wa kilimo wa 2019/20. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kampeni JTI upandaji miti yapokelewa vyema Tabora

**Na Mwandishi Wetu**

ZAIDI ya miti milioni tano imeoteshwa kwa ukamilifu katika Mkoa wa Tabora kupitia kampeni ya Kampuni ya JTI Leaf Services ya kuhamasisha upandaji wa miti kwa maeneo yanayolima zao la tumbaku mkoani hapo.

Kampeni hiyo imefanikishwa na Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, aliyeongoza vyama vya msingi 43 vya tumbaku na wakulima mbalimbali kuotesha miti hiyo milioni tano.

Akizungumza katika vijiji vya Maswanya na Migungumalo, alipongeza Kampuni ya JTI Leaf kwa kuwa mstari wa mbele katika kulinda miti asili ambayo iko katika hatari ya kuangamia kwani imekuwa ikikatwa ovyo katika matumizi ya kukausha tumbaku.

"Wametufundisha kuotesha aina ya miti ambayo haiungui haraka wakati wa kukausha tumbaku kwa hivyo nishati inayotumika ni ndogo mno," alise Mkuu huyo wa Mkoa ammbaye alikuwa ameongozana na Mkuu wa Wilaya ya Uyui, Gift Msuya na viongozi wengine pamoja na wanachama wa vyama mbalimbali vya msingi.

Aliipongeza JTI Leaf pia kwa kuhimiza kuhusu kupanda miti mapema kabla ya Desemba 16 na 17 kila mwaka ili kuhakikisha kuwa miti inayooteshwa haifi.

Mwanri aliongoza kwa vitendo kwa yeye na mkuu wa wilaya kuotesha miti huku wakionya kuwa hakuna mtu yeyote ataruhusiwa kufanya kilimo cha tumbaku bila kupanda miti.

Maeneo mengine ambako ilipandwa miti ni pamoja na kusimamiwa na mkuu huyo wa wilaya ni Usindi katika Wilaya ya Kaliua na Imalakoye katika Wilaya ya Urambo ambako aliongozana na wakuu wa wilaya hizo.

Miti hiyo pia ilipandwa katika kijiji cha Ugunga kilichopo Kaliua, Kasele katika Wilaya ya Urambo na Ndono Wilaya ya Uyui ambapo zoezi hilo lilisimamiwa na wakuu wa wilaya.

Zoezi hilo pia lilifanyika katika Vijiji vya Itobolo na Nonwe, Wilaya ya Ushetu Mkoa wa Shinyanga ambako JTI Leaf pia hununua tumbaku.

Kwa Desemba 16, zoezi hilo lilifanyika katika mashamba ya JTI Leaf na siku iliyofuatia ilikuwa zamu ya mashamba ya vyama vya msingi.

Meneja Uhusiano na Mawasiliano wa JTI Leaf Services, Bright Kiwia, alisema kampuni hiyo itaendelea kushirikiana na serikali katika masuala mbalimbali ikiwamo utunzaji wa mazingira.

Alisema kwa msimu uliopita, kampuni hiyo iliweza kubadilisha majiko 7,000 na kuweka ya kisasa mbayo hayatumii kuni nyingi na msimu huu wameshabadilisha majiko 4,500 hadi sasa na lengo ni kufikia idadi ya 7,000 kama msimu uliopita.

Meneja Misitu wa JTI Leaf Services, Alfadhil Makengo, alitoa pendekezo kwa serikali ya mkoa kuridhia Desemba 16 na 17 ziwe ndio tarehe za mwisho za kupanda miti katika maeneo yanayolima tumbaku, jambo ambalo lilipokewa vyema na MKuu wa Mkoa.

# Afa kwa kuonja sumu ya kuulia wadudu

**Na Gurian Adolf, SUMBAWANGA**

KIJANA Stanlaus Romano (17), mkazi wa Tarafa ya Laela wilayani Sumbawanga mkoani Rukwa, amefariki dunia baada ya kuonja sumu ya kuulia wadudu kwenye mahindi ili aone kama itaweza kumuua.

Kijana huyo alifariki dunia Desemba 14 majira ya usiku katika Kituo cha Afya Laela wakati akiendelea kupatiwa matibabu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Kamanda wa Polisi mkoani Rukwa, Justine Masejo, kijana huyo alikuwa shambani akipulizia dawa ya kuua wadudu kwenye mahindi, na alipoona kama wadudu hao hawafi, ndipo alipoamua kuijaribu ubora wake kwa kuinywa.

Kamanda huyo alisema kwamba baada ya kumaliza kazi aliyokuwa anafanya, alirejea nyumbani, wakati wa usiku akiwa amelala aliamka na kuwaambia wazazi wake kuwa tumbo linamuuma sana.

Aliwaeleza kuwa aliijaribu ubora sumu ya kuulia wadudu kwa kuinywa, ndipo walipompeleka katika kituo hicho cha afya kwa ajili ya matibabu.

Akiwa anaendelea kupatiwa matibabu, alifariki dunia kutokana na maumivu makali ya tumbo aliyokuwa akiyahisi kutokana na kunywa sumu hiyo.

Kamanda Masejo alisema kuwa hakuna mtu anayeshikiliwa na polisi kutokana na tukio hilo, na kufafanua kuwa mwili wa kijana huyo ulikabidhiwa kwa wazazi wake kwa ajili ya kufanya maziko.

**Aliwaeleza kuwa aliijaribu ubora sumu ya kuulia wadudu kwa kuinywa, ndipo walipompeleka katika kituo hicho cha afya kwa ajili ya matibabu**

# Wanawake wahamasishwa kugombea uongozi mwakani

**Na Mwandishi Wetu, PEMBA**

WANAWAKE wametakiwa kujitokeza kwa wingi kugombea nafasi mbali mbali za uongozi, ili waweze kujikomboa na hali duni ya maisha na kuacha kutegemea waume zao.

Akizungumza na wananchi wa Kisiwa cha Kojani Wilaya ya Wete, Mratibu wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania-Zanzibar (TAMWA) tawi la Pemba, Fathiya Mussa Said, alisema muda umefika kwa wanawake wote kushirikiana katika kujiletea maendeleo.

Alisema wanawake wana nafasi kubwa ya kugombea nafasi mbalimbali za uongozi katika serikali pamoja na jumuiya zisizo za kiserikali.

Aidha, aliwataka wanaume kuwaunga mkono kinamama wanapojitokeza kuchukua fomu za kugombea uongozi.

Omar Mjaka, Mbunge mstaafu CCM, alisema kugombea nafasi za uongozi kwa kinamama ni haki yao, hivyo aliwasisitiza kuitumia fursa hiyo kugombea kwa wingi, ili kutetea haki zao.

'Tukiangalia asilimia kubwa tunaona kuwa wawakilishi, wabunge na hata madiwani wengi waliopo ni wanaume na hawana mchango wowote ambao wanatusaidia, hivyo muda utakapofika tujitokezeni kwa wingi kufuchukua fomu za uongozi," alieleza Omar.

"Pia ninawaomba kinababa kuwaunga mkono wanawake kwani wao ndio wenye kazi... matatizo mengi na kazi nyingi hasa suala zima la malezi wakati mkizingatia hivi sasa dunia imebadilika na kugubikwa na wimbi la udhalilishaji," alisema Omar.

Omar alisema Tanzania ina vyombo vya kutunga sheria ikiwa Zanzibar ni Baraza la Wawakilishi huku Tanzania Bara ni Bunge, hivyo kinamama wawe mstari wa mbele kugombea nafasi za uongozi, ili waweze kujiletea maendeleo.

Mapema Omar aliwaeleza wananchi hao kuwa bado Kojani inahitaji mabadiliko ya aina mbalimbali, hivyo washirikiane katika kuijenga.

Naye Mohammed Hassan kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulia vijana, aliwataka wanawake kudai haki zao pamoja na kuwalea watoto wao katika malezi bora.

Alieleza kuwa, kwa upande wa dini zote duniani haikumkataza mwanamke kugombea nafasi za uongozi, hivyo ni wajibu wao kugombea nafasi hizo kwa mwenye uwezo.

Alipongeza Tamwa kwa kuunda tume ya wanaume mawakala wa mabadiliko ambao huwahamasisha kinamama katika suala zima la kugombea nafasi za uongozi katika maeneo yao.

Naye mwananchi Haji Idarous Bakar, mkazi wa Kojani, aliwataka wakazi wa eneo hilo kuwasomesha watoto wao ili waweze kuleta maendeleo.

Idarous alieleza kuwa, matatizo yaliyopo katika Kisiwa hicho ni taaluma ndogo, hivyo aliwataka viongozi wa Tamwa kufika Kisiwani humo kutoa elimu kwa wananchi.

Mradi wa kuwahamasisha wanawake kugombea nafasi za uongozi unaotekelezwa na Tamwa, unafadhiliwa Kitengo cha Wanawake cha Umoja wa Mataifa(UN-WOMEN).



Naibu Waziri wa Tamisemi na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mwita Waitara, akimshuhudia Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, Jokate Mwegelo (katikati), akihesabu sehemu ya mifuko ya saruji 200 iliyotolewa na kampuni ya GSM Group kwa ajili ya ujenzi wa mabweni ya wanawake kwa shule za sekondari, ikiwa ni kampeni ya Mkuu wa Wilaya hiyo ya Tokomeza Ziro, ambapo taasisi na mashirika mbali mbali yamekuwa yakichangia. Kulia ni Meneja Masoko na Mawasiliano wa kampuni ya GSM, Matina Nkurlu. **PIC HA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakulima wapewa angalizo moto kusafishia mashamba

**Na Said Hamdani, LINDI**

WAKULIMA katika Mkoa wa Lindi, wameonywa kuacha mara moja tabia ya kutumia moto kama nyenzo muhimu ya kusafishia mashamba yao.

Wameonywa kuwa utaratibu huo unaharibu mazingira na kuhatarisha usalama wa bomba la kusafirishia gesi asili kutoka mkoani Mtwara kwenda Dar es Salaam.

Katibu Tawala mkoani hapa, Rehema Seif Madenge, ndiye aliyetoa onyo hilo, wakati akifunga mkutano wa kwanza wa Jumuiya Wanachama Wakulima wa Korosho (TARUCHINA) wa mitaa na kata nne kati ya 20 zilizopo katika Halmashauri ya Manispaa ya Lindi.

Mkutano huo uliojumuisha wakulima 130 wapya na zamani wa korosho wa mitaa na kata za Tandangongoro, Ruaha, Chikonji na Nandambi, zilizopo Manispaa ya Lindi.

Madenge alisema kitendo cha wakulima kugeuza moto kuwa ni nyenzo muhimu za kusafisha mashamba yao sio kizuri kwani kinaharibu misitu jambo ambalo linahatarisha mkoa na Taifa kugeuka jangwa, hali itakayochangia kukosekana kwa mvua.

Madenge alisema athari za uchomaji moto katika Mkoa wa Lindi ni kubwa, hivyo kuchangia uharibifu mkubwa wa mazingira ya misitu iliyopo.


"Kukithiri kwa hii tabia uongozi wa serikali mkoa ulishatoa onyo na leo naendelea kusisitiza tena ni marufuku wakulima kugeuza moto kama nyenzo za kusafishia mashamba," alisisitiza Madenge.

Alisema licha ya kuharibu mazingira na mazao ya watu wengine, pia mkoa huo umepitiwa na bomba la kusafirishia gesi asili kutoka Mtwara kwenda Dar es Salaam, hivyo moto unapochomwa ovyo unaweza kusababisha maafa kwa wananchi wa vijiji na maeneo husika lilikopitia.

Pia aliwataka wakulima kutotumia nguvu nyingi kulima zao moja la korosho, badala yake wazielekeze pia kulima mazao mengine ya chakula ili mkoa na wao wenyewe wawe na uhakika kwa mwaka mzima.

Awali akitoa taarifa mwenyekiti wa mpito wa jumuiya hiyo, Muhidin Muro, alisema lengo la kuanzishwa kwake ni kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazowakabili wakulima wa zao hilo, ikiwamo upatikanaji wa pembejeo kwa wakati, masoko ya uhakika na bei zinazokidhi gharama za wakulima mashambani hadi kuuza kwa korosho.

Alisema wakulima wamekuwa wakikabiliwa na changamoto nyingi, lakini wanashindwa kuzipatia ufumbuzi kutokana na kukosa chombo imara cha kuwasimamia, ikiwamo kuzifikisha kunakohusika kwa lengo la kuzitafutia ufumbuzi.



## HABARI ARUSHA

# Gambo alia na dawa za kulevya

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, ameomba wakuu wa polisi wa mikoa ya Kanda ya Kaskazini kuongezea nguvu ya kudhibiti dawa za kulenya katika mikoa hiyo.

Akitoa ombi hilo juzi kwenye kikao kazi cha wakuu wa polisi wa mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara na Tanga, Gambo alisema kuna umuhimu wa wakuu hao kukaa pamoja na kubadilishana uzoefu jinsi ya kukabiliana na dawa hizo.

"Lipo tatizo la kushamiri dawa za kulevya katika mikoa yetu hii hasa mirungi na hii inatokana na nchi ya jirani Kenya kuruhusu dawa hizi, lakini hapa kwetu Tanzania haikubaliki, sasa lazima tuongeze juhudi za kupamabana na dawa hizi," alisema.

Gambo alisema ili kudhibiti dawa hizo, ni lazima kusaka mtandao wa wake ili kukomesha biashara hiyo.

Pia aliomba wakuu hao kuhakikisha wanaimarisha ulinzi katika kipindi cha sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya, ili wananchi washerehekee kwa amani na utulivu.

"Kweli haitapendeza na wala sitafurahi kuona au kusikia wananchi wamepata shida ya kuporwa au kuvamiwa na wahalifu wakati tuna askari," alisema.

Naye Kamanada wa Polisi Mkoa wa Arusha, Jonathan Shana, alisema suala la kukomesha uhalifu lipo ndani ya uezo wao, na sikukuu zitapita kwa amani na utulivu.

"Sisi Jeshi la Polisi tumejipanga na yeyote anayetaka kujaribu kuvunja amani atakiona cha moto kwani tunataka wananchi wote washerehekee sikukuu hizi kwa amani," alisema.

Aliomba wananchi kutoa taarifa za wale wote wanaojihusisha na matukio ya uhalifu ili wachukuliwe hatua.



**"Kweli haitapendeza na wala sitafurahi kuona au kusikia wananchi wamepata shida ya kuporwa au kuvamiwa na wahalifu wakati tuna askari," alisema.**

# Nassari aja kiuwekezaji tanzanite

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

ALIYEKUWA Mbunge wa Arumeru Mashariki mkoani Arusha, Joshua Nassari (Chadema) na wawekezaji 10 raia wa China juzi wametembelea migodi ya madini ya tanzanite Mji mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro mkoani Manyara, kwa lengo la kuwekeza.

Hata hivyo, Nassari baada ya kutembelea machimbo hayo juzi na wawekezaji hao, hakutaka kuzungumza kwa undani juu ya ziara hiyo.

"Sipo tayari kuzungumza kwa undani juu ya ziara hii, kwani hawa ni wageni kutoka China na wamefika kutembelea maeneo mbalimbali nchini kwa lengo la kuwekeza," alisema Nassari.

Mjiolojia wa Tume ya Madini Mirerani, Selemani Hamis, ambaye aliongozana na wageni hao, alisema wametembea migodi miwili ya madini ya tanzanite iliyopo kitalu D.

Hamis alitaja migodi miwili ya kampuni ya Flanoni na Edward Mollel waliotembelea ili kuona shughuli za uchimbaji wa tanzanite zinavyofanyika.

Alisema serikali imewapa ushirikiano wa kutosha wageni hao, ili waone migodi ya tanzanite na shughuli zinazofanyika, pamoja na kuwakaribisha kwa uwekezaji.

Mmoja kati ya wawekezaji hao, Tao Xiangyang, alisema kundi lao limehusisha wawekezaji wa sekta mbalimbali, hivyo wametembea vivutio mbalimbali nchini ili wawekeze katika eneo watakalopenda.

Xiangyang alisema kundi lao la wawekezaji 10 wapo wenye kuhitaji kuwekeza kwenye sekta mbalimbali ikiwamo madini, hoteli na ujenzi wa majengo makubwa.

Mfanyakazi wa mgodi wa Kampuni ya Flanoni, Aminiel Munuo akizungumza na wawekezaji hao, alisema wanafanya shughuli za uchimbaji madini kitaalamu kwa kutumia vifaa vya kisasa.

Munuo alisema wachimbaji tanzanite hivi sasa wanatumia teknolojia ya kisasa ikiwamo mashine na siyo kama miaka iliyopita, walipokuwa wanazama migodini kwa kutumia kamba pekee.



Katibu wa Itikadi na Uenezi CCM Taifa, ambaye ni mlezi wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Arusha, Hamphrey Polepole, akiongea katika Mkutano Mkuu maalumu wa uchaguzi wa mwenyekiti wa CCM Mkoa, uliofanyika katika ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa AICC. **PICHA NA WOINDE SHIZZA, ARUSHA**

# DC ataka kasi usajili wa laini za simu

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

MKUU wa Wilaya ya Arusha, Gabriel Daqarro, ameiomba Mamlaka ya Vitambulisho ya Taifa (NIDA), kuongeza uhamasishaji wa watu kusajili laini za simu zao hadi siku za Jumapili ili kufikia laini milioni 47 zilizolengwa kusajiliwa.

Akizungumza jana kwenye tamasha la uzinduzi wa kampeni ya uhamasishaji wa watumiaji wa simu za mkononi jijini Arusha kujiandikisha, Daqqaro alisema, hadi sasa laini zilizosajiliwa ni milioni 19 nchi nzima, idadi ambayo ni ndogo ikilinganishwa na idadi iliyotarajiwa ya milioni 47.

"Kutokana na idadi ya waliojiandikisha kuwa ndogo, natoa hamasa kwa Nida kuongeza juhudi na kufanyakazi hadi siku ya Jumapili kuandikisha watu ili kuwafikia wananchi," alisema.

Daqqaro alisema usajili kwa njia ya alama za vidole gumba, utasaidia kuwa na kanzi data yakujua takwimu za watumiaji wa mitandao ya simu kila mkoa na kupunguza wimbi la utapeli na uhalifu wa mitandao pamoja na kuimarisha usalama.

"Zoezi hili ni nyeti sana na mtu anapofanya usajili wa laini yake analazimika kutumia kidole chake ili kupata taarifa muhimu na pale anapofanya uhalifu atajulikana, hivyo kwa kiasi itapunguza uhalifu," alisema.

Aidha, alisema katika uzinduzi huo wananchi wengi wamejitokeza kusajili laini zao, lakini changamoto inayojitokeza baadhi ya wananchi kutokuwa na vitambulisho vya Nida.

"Lakini sisi kama serikali naahidi tutaongeza mashine ili kuondoa msongamani huu ninaouona wa wananchi ili wapate huduma haraka, na kwenda kuendelea na shughuli za uzalishaji mali," alisema.

Alizitaka kampuni za simu zinazotoa huduma katika viwanja hivyo kuhakikisha zinasogeza huduma kwenye maeneo ya soko na mikusanyiko ya watu ili kuwafikia watu wengi.

Awali baadhi ya wananchi waliohudhuria kampeni hiyo, Huruma Juma na Sophia Ismail waliomba Nida kupunguza urasimu eneo la Kisongo na kufanya kazi siku za Jumapili ili kuondoa msongamano wa kusajili laini zao.





# Bibi afanikiwa kurejeshewa shamba alilodhulumiwa

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

MJANE Renalda Malewo (80), mkazi wa Kyomu katika Kata ya Kahe Mashariki, Wilaya ya Moshi, ambaye alidhulumiwa shamba lenye ukubwa wa ekari 10 na mtoto wa kaka yake, amefanikiwa kurejesha ardhi hiyo baada ya mmoja wa wasaidizi wa kisheria kuingilia kati.

Licha ya kulirejesha mikononi mwake, pia mjane huyo aliyeachiwa familia ya watoto tisa pamoja na wajukuu, tayari amefanikiwa kulipima shamba hilo na kulikatia hati ya ardhi.

Katika mahojiano maalum jana na Nipashe kuhusu ushindi huo, mjane huyo ameeleza namna ndugu wa familia walivyolimega shamba hilo na kuuza viwanja kutoka ekari 10 hadi kufikia 8.5.

Malewo alisema: "Namshukuru Mungu kwa kumtumia huyu Para Legal (Msaidizi wa Kisheria) anayeitwa Getrude Terry kusaidia wanyonge kama sisi wajane tunaoonewa na kunyanyaswa.

"Mimi shamba nililoachiwa na marehemu mume wangu, nilidhulumiwa nikahangaika kwa miaka mingi lakini hatimaye nimefanikiwa kulirejesha mikononi mwangu. Niliteseka kwa zaidi ya miaka 10 bila kupata haki yangu, lakini leo nina furaha moyoni, nawashukuru watu hawa maana ni msaada mkubwa kwa wanyonge na wasio na uwezo wa kifedha."

Akieleza ugumu alioupata wakati wote akifuatilia haki yake, alisema alisuswa na ndugu wa marehemu na baadhi yao hawakutaka kumpa ushirikiano tangu alipopewa ushindi katika Baraza la Ardhi Kyomu na baadaye Mahakama ya Ardhi mkoa wa Kilimanjaro.

Alipotafutwa kueleza zaidi kuhusu kesi hiyo, Msaidizi wa Kisheria katika eneo hilo, Getrude Terry, alisema aliguswa kumsaidia mjane huyo kupata haki yake ya kumiliki ardhi, baada ya kuona dalili zote za ndugu kumdhulumu mama huyo ardhi aliyoachiwa na mumewe.

"Niliumia sana kuona haki yake inataka kupotea, nikaenda kuongea nae nyumbani kwake na kumshauri wapi atapata haki. Nikampeleka Baraza la Ardhi Kyomu na kesi ikasikilizwa akapewa ushindi. Kijana aliyekuwa anamdhulumu akakata rufani Mahakama ya Ardhi, nikaenda nae na kumsimamia kwa muda wote na akapata ushindi tena," alieleza Terry.

Baada ya ushindi huo, msaidizi huyo wa kisheria alimshauri kulipima na kutafuta hati ya ardhi na walipoelewana, Terry aliita Ofisa Ardhi wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi pamoja na mpimaji na wakafanya kazi hiyo.

Kwa mujibu wa Terry, mjane huyo, tayari mama huyo ameshakabidhiwa hati hiyo na mpaka sasa hakuna mwananchi aliyethubutu kuvamia tena eneo hilo.



Mkuu wa Wilaya ya Muheza mkoani Tanga, Mwanasha Tumbo (kushoto), akimkabidhi cheti mmoja wa wahitimu wa mafunzo ya Mgambo katika viwanja vya kijiji cha Kicheba juzi. **PICHA NA STEVEN WILLIAM**

# Kesi za ukatili 36 zashughulikiwa

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

RIPOTI ya mwaka ya mradi wa kukuza usawa kwa kutumia elimu ya haki za binadamu, inaonyesha kuwa mikoa ya Kilimanjaro na Arusha imefanikiwa kushughulikia kesi 36 za ukatili, huku kesi 24 kati yake zikihusu ukatili wa kingono dhidi ya watoto.

Kesi 12 ni migogoro ya familia na nne ni za wazazi kutelekeza watoto.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo iliyotolewa jana na Mratibu wa mradi huo, Consolatha Kinabo, katika mkutano mkuu wa nane wa Shirika la Kiraia la Tusonge linalotekeleza kazi hiyo, maeneo yaliyoguswa na kesi hizo ni Jiji la Arusha, Meru, Manispaa ya Moshi na Wilaya ya Siha.

Katika taarifa yake, alisema maeneo hatarishi yaliyofikiwa na mradi huo kwa mkoa wa Kilimanjaro ni kata za Bomambuzi, Njoro, Mabogini, Biriri na Ivaenyi.

Wakati Mkoa wa Arusha maeneo yaliyoguswa na mradi huo ni Sokoni One, Elerai na Maruvango.

"Kimsingi huko tulipofanya mikutano na wananchi na kuibuliwa kesi nyingi za ukatili wa kijinsia hasa Sokoni One (Arusha) na Bomambuzi (Moshi Mjini).

Zaidi mratibu huyo alieleza: "Malengo yetu yalikuwa ni kujenga uwezo wa wanawake na wasichana katika kukuza usawa kwa kijinsia katika jamii."

Mradi huo ulioanza kutekelezwa mwaka 2019, utafikia ikomo wake mwaka 2024.

Mpaka sasa walengwa wa mradi huo waliofikiwa ni wananchi 574 ambao wanawake ni 164, wanaume 123,wazee ambao ni wanaume 78 na wanawake wenye umri mkubwa 96, vijana wa kiume 45 na wa like 68.

## Vipigo dhidi ya wanaume sasa vyaibua mapya

**Na Godfrey Mushi, SIHA**

WAKAZI wa Kata ya Kirua katika Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro wameeleza masikitiko yao kuhusu ukatili ulioanza kuchipua wa wanawake wenye kipato kujigeuza mabondia na kuwashushia kipigo waume wanaotegemea mahitaji yote ya familia kufanywa na wake zao.

Wanaharakati wanawake wanaopambana na masuala ya ukatili wa kijinsia, walifichua aina hiyo mpya ya ukatili jana, wakati wa mafunzo ya mradi wa nguvu ya pamoja.

Mradi huo wa majaribio wa mwaka mmoja unatekelezwa na Shirika la kiraia la Kwieco kwa ufadhili wa WFT.

Akieleza kuhusu matukio hayo kuchipua kwa kasi katika Kata ya Kirua, Victoria Mmbando, alisema wanaume ambao wanategemea kipato cha wake zao katika eneo hilo, hivi sasa wanahofu kutokana na kukithiri kwa vipigo.

"Jamani huu ukatili wa kijinsia hivi sasa wanaume ndio wamegeuka waathirika, wanapigwa vibaya na wake zao na kuumizwa hasa huko kwetu Kirua. Unakuta mwanaume hafanyi kazi, anatoka nyumbani anaenda kijiweni kucheza kamari, drafti na kulewa pombe akija nyumbani hana kituo, anachoambulia ni kibano cha kutosha, hebu tuwateteeni jamani," alisema Mmando.


Akichangia hoja kuhusu mjadala huo, Mwenyekiti wa Jukwaa la vuguvugu la ukombozi wa Mwanamke Kimapinduzi (Tapo), Wilaya ya Siha, Christina Kavishe, alisema hatua ya kwanza inayopaswa kuchukuliwa ni kuwapa elimu wanaume na hasa vijana wafanye kazi halali ya kuwaingizia kipato na wasitegemee kulishwa na kuvishwa na wanawake wenye kipato.

Kwa upande wake, Victoria Malisa alisema inashangaza kuona hivi sasa katika wilaya hiyo vijana hawataki tena kuoa wanawake wa rika lao na wanakimbilia kuolewa na wa mama wenye umri mkubwa.

"Jamani wanaume hawataki kufanya kazi na kutekeleza majukumu yao kama baba wa familia, hadi sadaka wanapewa sasa hivi. Hivi wataachwa kupigwa kweli? Kutwa nzima wako vijiweni ni kucheza kamari, makorokoro na kula miraa," alisisitiza Malisa.

Akijibu maoni ya wanaharakati hao, Wakili Dorice Kinyoa ambaye ni mwezeshaji wa mafunzo hayo, alithibitisha malalamiko ya vijana kuolewa na kinamama wenye umri mkubwa yanajitokeza karibu kila wilaya, hivyo elimu zaidi inahitajika hasa Wilaya ya Siha.

**"Jamani wanaume hawataki kufanya kazi na kutekeleza majukumu yao kama baba wa familia, hadi sadaka wanapewa sasa hivi. Hivi wataachwa kupigwa kweli? Kutwa nzima wako vijiweni ni kucheza kamari, makorokoro na kula miraa," alisisitiza Malisa.**



Ukurasa 20

**Museveni alivyowateua, kuwatumbua mawaziri**

Azaveli Lwaitama sauti mpya inayonena mema Chadema



Ukurasa 18



Ukurasa 19

**Viongozi mitaa wasiwe kuku wa 'kutaga' matatizo kwa wananchi**


# siasa

JUMATANO DESEMBA 18, 2019

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe




Ukurasa 15

**Uchaguzi wa kihistoria Uingereza, wamuibua Mzanzibari**

# Uongozi mpya Chadema ulete agenda ya kuomba kura

**Na Sabato Kasika**

ULAZIMA wa kuchagua viongozi wa vyama ni takwa la demokrasia ambalo safari hii linafanywa na wanachama wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), wanaokusanyika Dar es Salaam kupata safu ya juu ya uongozi akiongozwa na mwenyekiti.

Wajumbe kwa takribani wiki mbili wanaendelea na kutimiza matakwa hayo ya demokrasia ambayo katika hatua waliyofikia yanaelekeza kumchagua Mwenyekiti wa Taifa wa Chama, nafasi inayotegemewa kuzibwa wakati wowote kuanzia sasa. Kila la heri.

Kikubwa katika uchaguzi huo unaofanyika miezi michache kabla ya uchaguzi mkuu ni kuwaletea wanachama na wananchi ajenda mpya ya kuomba kura kwa wananchi kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka ujao.

Historia inaonyesha kuwa chama hicho kilianzishwa

**INAENDELEA UK.16**



Mwenyekiti wa pili kuiongoza Chadema, Bob Makani, enzi za uhai wake. **PICHA: MTANDAO**

**Wabunge wakongwe kuwanoa wagombea wapya** Ukurasa 14

# Wabunge wakongwe kuwanoa wagombea wapya

• Mkakati ni maandalizi ya wasichana kuongozi



Katibu Mkuu wa CUF, Magdalena Sakaya. Ni miongoni mwa wanawake wachache wanaoongoza vyama vya siasa.



Margaret Sitta, Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania (TWPG). **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA jitihada za kuwapanga, kuwapika na kuwaandaa wabunge vijana wanawake kuingia kwenye siasa, wabunge wakongwe na wagombea wapya wanaotarajia kujitosa uchaguzi mkuu mwakani wanaanza mikakati ya kimaandalizi ya kuwajengea uwezo, kujiamini na kuthubutu.

Hatua hii inakuja huku ikidhihirika kuwa kwa kipindi cha miaka 25 tangu uchaguzi wa kwanza wa mfumo wa vyama vingi ufanyike, kumekuwa na mwamko wa wanawake kushiriki, kugombea na kushinda nafasi za uongozi.

Pamoja na ukweli kwamba, safari ni ndefu ya wanawake hususan kuwa wabunge wa majimbo yao, bila kusubiria viti maalumu inahitajika nguvu ya pamoja inayotoka ndani ya jamii. Hadi sasa ni asilimia tisa ya wabunge wote ni wabunge wanawake wa kuchaguliwa majimboni.

Katika kuelekea uchaguzi mkuu mwaka 2020, ikiwamo maandalizi ya kumuinua mwanamke, Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), umewakutanisha wanawake viongozi kutoka vyama mbalimbali ikiwamo CUF, ACT-Wazalendo na CCM kupanga mikakati.

Mkurugenzi wa TGNP, Lilian Liundi, akifungua mkutano huo, anasema ushawishi wa wanawake kuingia kwenye vyama na kuwania, kutaongeza idadi yao.

> “Kuna changamoto ya kupata ubunge. Walikuwa wabunge 45 mwaka 1995 na sasa tunafikia wabunge wanawake 145, ukichanganya mifumo mitano ya kupata ubunge.

Anasema uchaguzi wa mwaka 2015 ulionyesha mwanga baada ya mwanamke pekee Anna Mghwira kuwania kiti cha urais kupitia chama cha ACT-Wazalendo na hivi sasa yupo Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, mwanamke wa kwanza katika historia ya Tanzania kushika wadhifa huo ni mambo yanayowapa wanawake ari na hamasa ya kuingia.

Liundi anaeleza kuwa majadiliano ya pamoja kujengeana uwezo, uzoefu miongoni mwa wabunge wazoefu na wagombea wapya wanaotarajia kujitosa uchaguzi mwakani, ni nguvu pekee ya kuongeza ujasiri na uthubutu kwa wagombea watarajiwa.

“Tuna wabunge wanawake wenye majimbo 25 tu, madiwani wanaotoka kwenye kata ni asilimia tano achilia mbali asilimia sita ya madiwani wenyeviti wa halmashauri. Idadi ya wanawake viongozi watatusaidia kuzijadili na kuzingatia kutatua changamoto za wanawake kwenye afya, elimu na maji,” anasema Liundi.

**WABUNGE MIKAKATI**

Katika mkutano huo baadhi ya wabunge wanaoshiriki wanatoa hamasa kwa wanawake, ili kuingia kwenye siasa na uongozi, huku wakipanga mkakati wa kuwanoa wasichana kujiandaa kuwa viongozi tangu wakiwa shuleni.

Mbunge wa Urambo(CCM) na Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania (TWPG), Margaret Sitta, anasema maandalizi kwa wasichana katika uongozi ambao si bungeni tu ni muhimu.

Vilevile anasema wanawake ili washiriki ngazi mbalimbali za uongozi ni lazima maandalizi yaanze tangu wakiwa shuleni.

“Uongozi uwe mbunge hata nyadhifa za sekta tofauti, wanawake tuna nafasi, tuwaandae watoto wa kike kujiamini, kuwa majasiri na uwezo wa kujieleza ili wamudu uongozi,” anasema Sitta.

Mbunge wa viti maalumu (CCM), Zainabu Vullu, anasema pamoja na fedha kuwa kati ya changamoto katika kufikia uongozi, zipo ambazo zinaweza kutatuliwa na wanawake wenyewe.

“Tuvae mavazi yanayozingatia maadili, sio mgombea unavaa mavazi ambayo hayaendani na unachokiwania, tujijengee uwezo wa kujieleza, nina imani mwanamke ana ujasiri tangu alipoanza malezi ya mtoto siku ya kwanza alipojifungua,” anasema Vullu.

Amina Mollel, mbunge viti maalumu (CCM), anasema wanawake wenye ulemavu wana changamoto ikiwamo kujiamini na jamii kuwanyanyapaa.

“Fikiria mwanamke kama tayari ana changamoto sasa jumlisha na mwanamke mwenye ulemavu, kutokana na jamii niliyotoka nilionekana laana kuwa mlemavu. Zamani baadhi ya wajawazito niliopishana nao barabarani walijitemea mate kifuani, ili wasijifungue watoto wenye ulemavu kama mimi,” anasema Mollel.

Catherine Ruge, mbunge wa viti maalumu (Chadema), anasema mfumo dume, kutojiamini ni dhana potofu miongoni mwa jamii ambayo inawarudisha nyuma wanawake.

“Baadhi ya wanawake hudhani kuwa wakitoa rushwa ya ngono watashinda, ukijiamini unaweza utaweza,” anasema Ruge.

**HALI HALISI**

Makamu Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania (TWPG), Susan Lyimo, anasema uchaguzi wa mwaka 2010 wabunge wenye majimbo walikuwa 18 na uchaguzi wa mwaka 2015, umeongeza idadi hiyo na kufikia 25.

Anasema kati ya vyama vya siasa 19 nchini ambavyo vimesajiliwa ni kimoja pekee cha SAU kinachoongozwa na mwanamke.

“Vyama vya siasa vinavyoongozwa na wanaume vitambue kwamba wanawake wana umuhimu wa kuongoza vyama hivi pia, kuna vikwazo vinajitokeza, wanajitokeza kuwania wakifika kwenye kamati wanakatwa,” anaonya Lyimo.

Makamu Mwenyekiti anaeleza kuwa katika uongozi bado kuna safari ndefu na kwamba kati mawaziri 21 wanawake ni wanne pekee, licha ya takwimu za sensa zikidhihirisha kuwa wanawake ni wengi wakifikia asilimia 51 wakati wanaume ni 49.

“Tuone ni jinsi gani wanawake tuliopata fursa kusaidia namna ya kuongeza wenzetu kuwa viongozi, tumekuwa tukipigania masuala ya maji, afya, elimu lakini sauti za wachache hazitoshi,”.

Anaeleza kwamba kwa asilimia 70 wanawake ni wakulima, wazalishaji waliojiajiri na kutegemewa kiuchumi na familia zao mijini na vijijini.

“Kuelekea uchaguzi 2020 tunataka wanawake na uongozi tufikie asilimia 50, na si 30 iliyowekwa. Tunapaswa kufanya kazi zaidi mara mbili au nne ya wanaume, ili tuinuke,” anasisitiza Lyimo.

Anabainisha kuwa mfumo dume uliopo utaondolewa na wanawake na kwamba wakatae kudhalilishwa na kuepuka rushwa ya ngono, wakidhani watapitishiwa ushindi.

Anasema kwa uzoefu wake wa miaka 15 bungeni, ameshuhudia asilimia 60 hadi 70 ya wabunge huwa hawarudi baada ya uchaguzi, kutoka na sababu tofauti hasa ushindani.

“Kuna changamoto ya kupata ubunge. Walikuwa wabunge 45 mwaka 1995 na sasa tunafikia wabunge wanawake 145, ukichanganya mifumo mitano ya kupata ubunge,” anasema Lyimo.

Anasema wabunge hao wamepatikana kupitia wakuteuliwa na rais, kutoka baraza la wawakilishi, waliochaguliwa majimboni na viti maalumu ambao ni asilimia 36.

Anafafanua kuwa changamoto zinazowakwamisha wanawake ni pamoja na kukosa uthubutu, fedha, mifumo ya uchaguzi ndani ya vyama na kwamba vyama viandae miradi ya kifedha ili kujiimarisha.

Anawakumbusha wapigakura kuwa wanawake wanayo haki ya kuwania nafasi za uongozi, kupiga na kupigiwa kura.

UCHAMBUZI

# Uchaguzi wa kihistoria Uingereza...

## • Wamuibua Mzanzibari, Leba taabani

Na Mwandishi Wetu



Mbunge mpya Munira akiwa na kiongozi wa zamani wa jimbo la Twickenham , Vince Cable ambaye ni mstaafu. **PICHA: MTANDAO**

UCHAGUZI wa Uingereza, uliofanyika wiki iliyopita, unaelezwa kuwa umemuibua Mzanzibari, Munira Wilson kuwa mbunge.

Munira anaelezwa na mitandao ya hapa nchini kuwa ni mtoto wa Sherali Hassan, aliyekuwa akiishi Malindi na mama yake ni Fatma mkazi wa Mji Mkongwe, Unguja.

Hata hivyo, taarifa za Munira kwenye mtandao zinazozungumzia kuchaguliwa kwake, zinaeleza kuwa ni raia wa Pakstani.

Munira ni mbunge jimbo la Twickenham lililoko London na anaingia bungeni kwa tiketi ya chama cha Liberal Democrats

Anachukua kiti hicho kutoka mbunge wa chama cha Liberal Democrats -Vince Cable ambaye amestaafu.

Mbunge huyo mteule awali alikuwa diwani Twickenham, anapinga mpango wa Brexit na atetea uwekezaji kwenye huduma za kijamii kama shule, usalama na maslahi bora ya polisi na ulinzi mazingira kutokana na kitisho cha mabadiliko ya tabia nchi.

### USHINDI WA JOHNSON

Katika uchaguzi huo, kiongozi wa chama cha Conservative ambaye ni Waziri Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson, amepata ushindi wa kishindo kwenye uchaguzi mkuu wa wiki iliyopita, hatua iliyomtambulisha kuwa ni mwanasiasa maarufu mno nchini humo.

Mbunge wa zamani wa Conservative Sir Alan Duncan, ambaye amekuwa mkosoaji mkubwa wa Boris Johnson, anasema kwamba Waziri Mkuu huyo sasa ndiye mwanasiasa mwenye umaarufu mkubwa Uingereza na kwamba uchaguzi huo umethibitisha hilo.

Anaiambia BBC "sasa tutaweza kutawala kwa wingi wa kura".

Hata hivyo uhalali huo unamaana moja tu kuwa Waingereza wamempatia tena rasmi jukumu la kufanikisha mchakato wa Brexit na kuiondoa Uingereza katika Muungano wa Ulaya (EU).

Kwa upande wake Johnson anawashukuru wapiga kura wa Uingereza kwa kushiriki kwa wingi katika uchaguzi wa Disemba na kuviambia vyombo vya habari muda mfupi baada ya chama chake kushinda zaidi ya viti 326, kwamba hatua hiyo inaipatia serikali mpya fursa ya kuheshimu maamuzi ya kidemokrasia ya raia wa Uingereza ili kuliimarisha taifa hilo.

Chama cha Johsnon kilihitaji kujipatia viti 326 ili kutangazwa kuwa mshindi lakini kimepata viti zaidi ya 364. Kiongozi huyo anaona kwamba uamuzi huo unampatia jukumu la kufanikisha mchakato wa Brexit na kuiondoa Uingereza katika Muungano wa Ulaya (EU).

"Zaidi ya yote nataka kuwashukuru watu wa taifa hili kwa kujitokeza kupiga kura ya Desemba ambayo imebadilika na kuwa ya kihistoria, ambayo inatupatia sisi kama serikali mpya fursa ya kuheshimu uamuzi wa kidemokarsia wa raia wa kulibadilisha taifa hili na kuonyesha uwezo wa raia wa taifa hili".

### KUFANIKISHA BREXIT

Huu ni uchaguzi wa Uingereza wa tatu chini ya miaka mitano na wa kwanza kufanyika Desemba katika kipindi cha miaka 100 . Kwanza ulitanguliwa na kura ya maoni ya mwaka 2016 ya kuondoka katika Muungano wa Umoja wa Ulaya.

> Chama cha Conservative kina wabunge 365 na Leba wapo wabunge 203, vyama vingine kama SNP kina viti 48, Liberal Democrats 11 huku chama cha DUP kikijipatia wabunge nane.

Johnson ambaye kwenye kampeni aliangazia ujumbe mmoja- kuhakikisha Brexit inafanikiwa na anaahidi kuiondoa Uingereza katika EU kufikia Januari 31, 2020 iwapo angepata wingi wa kura.

Waziri Mkuu baada ya uchaguzi anasema kwamba atafanya kazi 'usiku na mchana' ili kuwalipa wapiga kura waliomuonyesha uaminifu baada ya kukisaidia chama chake cha Conservative kupata ushindi wa kihistoria.

Akizungumza mjini London, Waziri Mkuu Johnson anasema kwamba ni jukumu lake kuindoa Uingereza katika Muungano wa EU, akiongeza "Raia wanataka mabadiliko," "hatuwezi kuwavunja moyo na hatutawavunja "

### BREXIT KABLA KRISMASI

Anaungwa mkono na Waziri wa Mambo ya Ndani wa chama cha Conservative Priti Patel, anayeahidi kuwa serikali itahakikisha kwamba Brexit inafanyika kwa haraka kabla ya Christmas kupitia kuwasilisha miswada.

Hatua hiyo inajiri muda mchache baada ya mpinzani mkuu wa Boris Jonson Jeremy Corbyn, kusalimu amri na kusema kwamba hatokiongoza tena chama hicho katika uchaguzi mkuu ujao.

Uamuzi huo wa kiongozi wa Leba unajiri huku chama hicho kikikabiliwa na matokeo mabaya zaidi ya uchaguzi katika miongo kadhaa.Chama cha Conservative kimeshinda baadhi ya viti katika ngome za chama cha Leba.

Chama cha Leba kimepoteza viti kaskazini mwa Uingereza, Midlands na Wales yakiwa ni maeneo yaliyopiga kura ya Brexit katika kura ya maoni ya mwaka 2016. Leba ilitarajiwa kushinda viti 61 ikiwa ni chini ya viti ilivyoshinda 2017 ilidaiwa.

Baadhi ya maeneo ya bunge kama vile Darlington ama Workington , kaskazini mwa Uingereza yataongozwa na mbunge wa Chama cha Conservative kwa mara ya kwanza katika miongo kadhaa- ama katika matukio ya Bishop Auckland na Blyth Vally kwa mara ya kwanza tangu viti hivyo kubuniwa.

Lakini Leba kimeshinda kiti cha eneo bunge la Putney, kusini magharibi mwa London kutoka kwa Conservative.Chama cha Skotiland cha kitaifa kimepata ushindi wake wa kwanza eneo bunge la Rutherglen na Hamilton magharibi kutoka kwa chama cha Leba na Angus kutoka kwa Conservative.

Chama cha Conservative kina wabunge 365 na Leba wapo wabunge 203, vyama vingine kama SNP kina viti 48, Liberal Democrats 11 huku chama cha DUP kikijipatia wabunge nane.

Mgogoro ulikuwa tayari umezuka katika chama cha Leba kuhusu ni nani anayefaa kulaumiwa katika kile kinachotarajiwa kuwa uchaguzi wake mbaya zaidi katika miongo kadhaa.

Mwenyekiti wa Leba Ian Lavery, ambaye alihifadhi kiti chake kwa uchache wa kura alizopata awali anasema kwamba amesikitishwa akisema kwamba wapiga kura katika ngome za chama cha Leba wanaomboleza kuhusu msimamao wa Brexit wa chama hicho.

Chansela kivuli John McDonald, anaiambia BBC kwamba matokeo ya kura yasio rasmi yalikuwa yanasikitisha kwa Leba."Nilidhania ushindani utakuwa wa karibu mno", anasema na kulaumu kile anachokitaja kuwa uchaguzi wa Brexit, wakati Leba ilitarajia kwamba masuala mengine yatachipukua.

Anamwambia mwandishi wa BBC Andrew Neil kwamba uamuzi utafanywa kuhusu kiongozi wa chama hicho Jeremy Corbyn katika siku za usoni wakati matokeo rasmi yatakapotolewa.

Baadhi ya wagombea wa Leba wamekosoa uongozi wa Corbyn , kwa mfano Gareth Snell, anasema kwamba alitarajia kupoteza kura ya Stoke Central kwa chama cha Conservative na alimtaka Corbyn na McDonald kuondoka lakini pia akawalaumu wanachama wa chama hicho wanaopinga Brexit kwa kukisukuma sana chama hicho.

### MAWAZIRI

Ofisi ya Waziri Mkuu katika taarifa yake imeahidi kuwa iwapo Johnson anarudi madarakani kutakuwa na mabadiliko machache ya baraza la mawaziri, muswada wa makubaliano ya kujiondoa utakaorahisisha kuondoka kwa Uingereza EU ifikapo Januari 31, utasomwa kwa mara ya pili katika bunge hilo keshokutwa Desemba 20.

Mabadiliko makubwa ya baraza la mawaziri yatafanyika mwezi Februari, baada ya Uingereza kuondoka EU huku taarifa ya bajeti ikitolewa mwezi Machi.

Chama cha Leba kilifanya kampeni ya kuongeza matumizi katika huduma za umma mbali na katika vituo vya afya.

Chama cha Liberal Democrats kiliahidi kufutilia mbali Brexit iwapo kiongozi wake Jo Swinson angechaguliwa kuwa Waziri Mkuu, lakini kura ya maoni ilitabiri kwamba ufuasi wao utapungua wakati wa kampeni. **BBC**

# Uongozi mpya Chadema ulete agenda ya kuomba kura 2020



Mwenyekiti wa Chadema anayemaliza muda wake, Freeman Mbowe, kwenye moja ya mikutano ya kamati kuu ya chama hicho. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**INATOKA UK.13**

mwaka 1992, kikiwa chini ya uenyekiti wa aliyewahi kuwa Gavana wa Benki Kuu Tanzania (BOT) Edwin Mtei.

Kiliundwa kikiwa na falsafa ya nguvu ya umma, kikiamini kuwa sehemu ya serikali inayotoa ridhaa ya maamuzi na ruhusa ya mfumo wowote huku itikadi ikiwa ni mrengo wa kati unaoamini katika soko huria lenye kusimamiwa na kudhibitiwa.

Baadaye mwaka 1998 nafasi ya Mwenyekiti wa Chadema Taifa ilichukuliwa na Bob Makani ambaye alishika wadhifa huo hadi mwaka 2003 alipomaliza muda na kuamua kuendelea na kazi zake kama mwanasheria wa kujitegemea.

Aidha, alibaki kuwa kiongozi na mshauri wa chama hadi alipofariki dunia huku nafasi ya mwenyekiti wa chama taifa ikiwa tayari imeshachukuliwa na Freeman Mbowe ambaye sasa anatetea nafasi hiyo.

Mbowe anawania tena wadhifa wa Mwenyekiti wa Chadema Taifa ili kukiongoza tena kwa miaka mingine mitano, huku akichuana na Mbunge wa Ndanda mkoani Mtwara, Cecil Mwambe.

Mara ya mwisho Chadema ilifanya uchaguzi wa viongozi wake mwaka 2014 huku Mbowe akiibuka na ushindi wa kura 789, dhidi ya mpinzani wake Gambaranyere Mwangateka aliyepata kura 20.

> Safari hii ya siasa ni ndefu na yenye milima na mabonde, ambayo imesababisha baadhi ya vyama kutoweka na kubaki 19 tu katika daftari la Msajili wa Vyama vya Siasa nchini.

### KUJIIMARISHA KISIASA

Kwa mara nyingine chama hicho kinafanya uchaguzi mkuu wa viongozi wake kikiwa kinaendelea kujiimarisha tangu kiliposhiriki uchaguzi mkuu wa kwanza ndani ya mfumo wa vyama vingi uliofanyika mwaka 1995.

Kumbukumbuku zinaonyesha kuwa katika uchaguzi mkuu wa mwaka 1995 chama hicho kilipata wabunge wanne na madiwani 42 na kisha uchaguzi wa mwaka 2000 kikapata wabunge watano na madiwani 75.

Uchaguzi mkuu wa mwaka 2005, chama hicho kiliendelea kuongeza idadi ya wabunge wakafikia 19, huku madiwani wakiwa ni 103, na uchaguzi wa mwaka 2010 kilipata 24, na mwaka 2015 kikavuna wabunge 34.

Idadi hiyo yote ya wabunge ni wa kuchaguliwa katika majimbo, ambao wameendelea kuongezeka kila mwaka wa uchaguzi, hali inayoosha kuwa chama hicho kinazidi kuwa imara.

Hata hivyo licha ya wabunge kadhaa na madiwani kuhamia CCM, chama kimeendelea kusimama na kutimiza majukumu yake kidemokrasia.




Muasisi wa Chadema, mzee Edwin Mtei.

### KIONGOZI IMARA

Licha ya kuongeza idadi ya wabunge na madiwani kila mwaka wa uchaguzi, Chadema ni chama ambacho bado kinahitaji kuwa na kiongozi imara anayetimiza wajibu wake bila kutetereka.

Hivyo wakati huu, ambao chama hicho kiko kwenye uchaguzi wa viongozi wake wa taifa, upo umuhimu wa kuliona hilo na hatimaye kuchagua viongozi, ambao watakivusha na kukifanya kisonge mbele zaidi.

Kwa kawaida vyama vya upinzani huchukuliwa kama jicho la pili, katika kushauri na kukosoa serikali, pale inapoonekana kuna mambo ambayo hayaendi kama inavyotakiwa lengo likiwa ni kwa ajili ya maendeleo ya nchi na ustawi wa raia wote.

Chadema inaweza kuendelea kuaminiwa na Watanzania iwapo itachagua viongozi imara wanaosimamia na kutimiza wajibu wao bila kuyumbishwa na wanachama au kundi kutoka nje ya chama.

Ukiangalia tangu uchaguzi wa kwanza ndani ya mfumo wa vyama vingi, chama hicho kimeendelea kuongeza idadi ya wabunge na madiwani, hivyo hatua hiyo ni ya kulinda na kukiwezesha kuongeza wengine zaidi.

### KUJIIMARISHA MATAWINI

Wanachama wa chama chochote cha siasa wapo ngazi ya chini kuanzia kwenye mashina na matawi, hivyo ili chama kiwe na nguvu, hakina budi kujiimarisha huko kwanza ili kupata uhakika wa kuwa na wanachama wengi.

Hivyo chama hicho kinatakiwa kuwa na viongozi wanaoliona hilo na kulifanyia kazi kwa vitendo, vinginevyo kinaweza kuwa na mashabiki tu bila kuwa na wanachama ambao kimsingi ndiyo mtaji wa chama.

Wagombea wanaowania nafasi hiyo ya mwenyekiti, ni wakati muafaka kwao kuweka mbele maaslahi ya chama ili kiwe katika mazingira na mazuri ya kuendelea kutimiza malengo yake.

Ushindani wa kuwania uenyekiti wa chama hicho usizae mgogoro ambao unaweza kukigawa na kujikuta kikiyumba, bali lengo lao liwe moja la kukiimarisha kiweze kuendesha shughuli za kisiasa inavyotakiwa.

Si vyema vyama kulenga kushika dola tu bila kushughulika na wananchi, kwa maana ya kujiimarisha ngazi ya chini, ambako kimsingi ndiko waliko wapigakura, vingi hujikuta vinakwama.

> Si vyema vyama kulenga kushika dola tu bila kushughulika na wananchi...

### SAFARI NDEFU

Tangu mfumo wa vyama vingi vya siasa uliporejeshwa nchini mwaka 1992, ni baadhi ya vyama vilivyoanzishwa wakati huo vilishajifuta na vingine kufutwa na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa.

Safari hii ya siasa ni ndefu na yenye milima na mabonde, ambayo imesababisha baadhi ya vyama kutoweka na kubaki 19 tu katika daftari la Msajili wa Vyama vya Siasa nchini.

Lakini kwa Chadema ambacho kiliwahi kutabiriwa na Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere kuwa huenda kikaleta upinzani, kimeendelea kuongeza idadi ya wawakilishi uchaguzi mkuu unapofanyika.

Kwa hiyo mchakato wa uchuguzi wa viongozi wa juu wa chama hicho unaweza kutoa picha halisi ya uimara wake na kukifanya kizidi kuaminiwa na wanachama na hata na mashabiki wa mambo ya siasa nchini.

## Rais Pervez Musharraf wa Pakistan ahukumiwa kifo




Jenerali Pervez Musharraf

JENERALI Pervez Musharraf (76), kiongozi wa zamani wa kijeshi nchini Pakistan, amehukumiwa kifo katika mahakama maalum mjini Islamabad, jana.

Mahakama hiyo ya majaji watatu ilimhukumu kifo kwenye kwa kesi ya kiwango cha juu cha uhaini baada ya kuahirishwa tangu mwaka 2013.

Jenerali Musharraf alichukua mamlaka katika mapinduzi ya kijeshi yaliyofanyika mwaka 1999 na akahudumu kama rais wa taifa hilo kutokea mwaka 2001 hadi 2008.

Kwa sasa kiongozi huyo, anayeishi Dubai baada ya kuruhusiwa kuondoka nchini humo kwa matibabu 2016. Mashtaka hayo yanahusiana na hatua ya Jenerali Musharraf ya kuahirisha katiba 2007, wakati alipoweka utawala wa dharura uliolenga kuongeza muhula wake.

Kiongozi huyo alitoa kanda ya video akiwa katika kitanda chake hospitalini mapema mwezi huu , akielezea kwamba kesi hiyo dhidi yake haina msingi wowote.

Jenerali Musharraf ni mtawala wa kwanza wa kijeshi kufanyiwa kesi nchini Pakistan kwa kusimamaisha katiba. Uamuzi huo ulitolewa jana huku watatu hao wakipiga kura mbili kwa moja ili kumhukumu.

Mnamo mwezi Novemba 2007, Jenerali Musharraf alifutilia mbali katiba na kuweka utawala wa dharura - hatua iliyozua upinzani na vipingamizi vikali , hata hivyo alijiuzulu 2008 ili kuzuia tisho la kushitakiwa

Wakati huo, Nawaz Sharif, mpinzani wake ambaye alimpindua mwaka 1999 alichaguliwa kuwa Waziri Mkuu 2013, alianzisha kesi ya uhaini dhidi ya Jenerali Musharraf na mwezi Machi 2014, alishtakiwa kwa uhaini.

Musharraf alisema kesi hiyo ilichochewa kisiasa na kwamba hatua alizochukua 2007 zilikubaliwa na baraza la mawaziri.Lakini hoja yake ilifutiliwa mbali na mahakama na kushutumiwa kwenda kinyume cha sheria.

Kulingana na katiba ya Pakistan, mtu yeyote anayepatikana na kiwango cha juu cha uhaini anaweza kukabiliwa na hukumu ya kifo, ambayo ndiyo aliyohukumiwa.

Kiongozi huyo amekuwa akiishi Dubai tangu 2016 na amekataa kujiwasilisha mbele ya mahakama hiyo, licha ya maagizo kadhaa. **BBC**

# Azaveli Lwaitama sauti mpya inayonena mema Chadema



Mhadhiri mstaafu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dk. Azaveli Lwaitama. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**Na Ani Jozeni**

KUNA jambo jipya katika chama cha Chadema ambalo ni kujiunga au kujitokeza hadharani licha ya kuwa ni hadhara ya ndani, ya mikutano ya uchaguzi, Dk. Azaveli Lwaitama, mhadhiri mstaafu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ambaye amefundisha na anaendelea kuhudumia vyuo vikuu vingine vingi.

Dokta Lwaitama (pichani), anafahamika zaidi kama mwanaharakati na mchambuzi wa masuala ya siasa katika vipindi vya redio za ndani na za kimataifa na hushiriki makongamano tofauti kwa miaka mingi.

Ni mtaalamu wa lugha, aliyefanya masomo ya uzamivu (PhD) akiangalia matumizi ya lugha na mtiririko wa kujieleza katika hotuba za Mwalimu Nyerere wakati huo akiwa Rais.

Sauti aliyoingiza Dk. Lwaitama katika Chadema na hata yeye binafsi kuona hitaji la kufanya hivyo na siyo kuitakia mema harakati ya chama hicho akiwa pembeni unaweza kusema inahitajika ndani ya chama hicho kwa wakati huu.

Na kinachohitajika katika chama cha siasa chenye umati wa watu au wafuasi wake wakikusanywa pamoja ni jambo ambalo pia linahitajika nchini, hivyo ni somo kuhusu mpangilio au mfumo wa siasa za Tanzania.

Jambo hilo ni kujipambanua kwa kuchukua nafasi ya wazi hadharani kwa swali la hatima ya chama.

Hatima ya chama katika mfumo wa siasa ni kile inachohitaji kufanya kwa wakati huo, kiendane na mahitaji ya hali halisi yenyewe, kusukuma mbele gurudumu la historia na kujihakikishia nafasi katika historia hiyo kwa upande wa pili.

> “Ni rahisi zaidi kutumia mfananisho wa gari, liwe barabarani na siyo limewekwa pembeni vile hatuna kazi na ‘tuvyama,’ kama wasemavyo CCM.



Mwenyekiti wa Chadema Taifa, Freeman Mbowe.

Ni swali ambalo kila mwanaharakati na hasa kila kada wa chama inabidi ajiulize, au kwa upande mwingine, kila msomi na kwa kina zaidi kila mwanaharakati anajiuliza swali hilo kuhusu nchi, na akipata jibu ajipambanue kwa jawabu analolitoa. Ni swali linalojirudia katika maandishi ya wanaharakati na hasa wanamapinduzi.

Msomi mbobezi Lwaitama hakusema kuwa amekwenda Chadema au amejitokeza hadharani kuokoa jahazi, anachoeleza waziwazi ni kuwa hataki nafasi yoyote ya uongozi, ila tu kutoa mchango kwa chama hicho au kwa umma au wengine waliokuwa wanafuatilia kwingine. Anachokifanya ni kuweka mkazo ulazima na umuhimu wa ‘Programu Chadema’ kwa kuipatia hisia, taswira na hata ‘uhalali’ mpya, kuwa ni ‘jahazi’ la kuhakikisha maendeleo ‘ambayo ni pacha na demokrasia.’ Nje ya hapo ni maendeleo ya vitu na siyo ya watu, kwa ufafanuzi huo.

Kwa wanaomfahamu Dk. Lwaitama katika ujana wake, na labda hawajafuatilia vya kutosha aliyokuwa anasema katika makongamano ya UDSM na mijadala redioni au katika televisheni, kuna sura mpya.

Baadhi ya waandishi wa historia maisha ya watu (biography) wangesema kuna ukomavu wa kifikra au utu uzima na taswira au ujumbe wa kisiasa ambao ni rahisi kueleweka na unaokidhi mahitaji ya harakati, yaani kama mpango wa kupelekwa mbele ya wananchi kuombewa kura.

Labda haijakidhi kila kitu ila inafaa kuwa msingi wa programu ya Chadema, kama ‘kianzio’ cha kupambanua mwelekeo wa kiitikadi hivi sasa. Nje ya hapo, kuorodhesha matatizo ya bajeti, au mikataba itakuwa tatizo na si ajenda ya kuushawishi umma.

Kwa wanaofahamu historia ya fikra za siasa, mchango wa Dk. Lwaitama ni kielelezo cha fikra ya kipindi cha majonzi, cha mtu aliyejeruhiwa, ndiye anayepata nafuu kimawazo akija mtu mpole, mpatanishi, anayetaka jema siyo kwa kuchukua madaraka ila kuwepo nafasi ya fikra tofauti kuishi, na kutoa mchango katika kutathmini kinachoendelea. Ni mazingira tofauti kabisa na kipindi kilichotangulia ambako chama hicho kilikuwa kinapanga mipango (ikiwa hasa ndiyo maana ya’kutunga sera’) jinsi ya kuchukua madaraka wakati ukifika. Ni mazingira ambako dhana nzima ya demokrasia haikuthaminiwa, na viharatishi vya kuchezewa kwake vilipuuzwa.

Ipo kanuni katika maisha ya kawaida ambayo ni moja ya mihimili ya fikra ya uchumi, ile ya ‘law of diminishing returns,’ yaani unavyozidi kuwa na wingi wa kitu fulani ndivyo unavyozidi kuchoshwa na kitu hicho.

Utakuta kuna sababu lukuki za kuanzisha machafuko katika jamii kwa maandamano yasiyoisha, na ukichunguza unaona kuna aina fulani ya ‘kudeka,’ kwani mfumo wa demokrasia pana unalemaza hisia kwa kiwango fulani.

Mtu akijisikia vibaya kwa jambo fulani anakuwa na uwezo wa kulikuza liwe ndiyo mada kuu, iwe katika siasa au hata unyumba.

Hayo siyo anayoyasema Dk. Lwaitama, na wala yasingeleta utulivu na matumaini Chadema endapo angekwenda na hisia kama hizo, ila kutetea kile wanachokifanya, na tuseme alichokifanya ni kutetea ile nembo, akisisitiza kuwa jahazi hilo ‘libaki barabarani.’ Licha ya kuwa alipata shida kidogo kuoanisha dhana ya jahazi na barabara katika fani yake ya lugha, kimsingi alieleweka, kwani jahazi hilo hatuwezi kusema limetia nanga mahali na sasa linatakiwa liondoke, kwani ni dhana mchanganyiko.

Ni rahisi zaidi kutumia mfananisho wa gari, liwe barabarani na siyo limewekwa pembeni vile hatuna kazi na ‘tuvyama,’ kama wasemavyo CCM.

Dokta Lwaitama ameonyesha ulazima wa demokrasia kwa maendeleo halisi na kwa jumla hisia zake hazina tofauti na zile za Mwalimu Nyerere, ila Mwalimu hakutetea demokrasia kama ilivyo na tofauti yake alikuwa akitetea ‘uhuru’ wa wananchi, au wa watu na taifa kwa jumla.

Dk. Lwaitama aligusa huko, akishangazwa na ombi lililotolewa hadharani hivi karibuni na mmoja kati ya wale wanaotoa maswali wakati Rais John Magufuli, akiwa katika ziara zake mikoani.

Mkazi huyo alimsihi Rais ‘arudishe fedha mitaani.’ Dk. Lwaitama hakujadili kama fedha zilipotea kwa vipi, ila nafasi ya ‘ombi’ miaka 58 baada ya uhuru, kuwa mtu huyo ’amenyong’onyeshwa,’ na mamilioni wengine.

# Viongozi mitaa wasiwe kuku wa ‘kutaga’ matatizo kwa wananchi



Viongozi wa serikali za mitaa washirikiane na Tarura kubadilisha barabara mbovu mijini na vijijini. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Gaudensia Mngumi**

UCHAGUZI wa serikali za mitaa umekwisha baada ya viongozi wa mitaa, vijiji na vitongoji kuapishwa na kuanza kazi kufuatia uchaguzi ambao ulisusiwa na baadhi ya vyama vya upinzani.

Kwa hiyo kinachotazamiwa sasa ni kuona kiongozi wa shughuli za mitaani, vijijini au vitongoji akifanyakazi kwa uadilifu na kuwajibika kutatua matatizo ya wananchi, na cha msingi sasa ni kuanza na mikutano ya wananchi.

Tofauti na miaka ya nyuma, ambako kulikuwa na viongozi wa serikali za mitaa waliokuwa na mrengo wa kichama na kufanya kazi kwa misingi ya kile, ambacho chama chao kilikuwa kinawaelekeza, safari hii walio wengi ni CCM hivyo ni matarajio ya wananchi kuwa watatekeleza masuala muhimu, ambayo serikali inayasimamia.

Watanzania wanatarajia kuona mabadiliko siyo kuficha ukweli, kulumbana kuhusu miradi ya maendeleo na wanataka kuona viongozi wanaoshughulikia matatizo ya watu na wanaowajibu maswali na hoja zao wanapozifikisha kwenye ofisi iwe ya mtaa, kitongoji na kijiji.

Wale waliopiga kura ni wazi walichoshwa na mazoea ya kuona viongozi wa serikali za mitaa wakitembea na mihuri ili kupata asilimia 10 ya mauzo ya viwanja.

Wengi walikuwa wanakerwa na mazoea ya baadhi ya viongozi kuwaambia walipie gharama za kuchapishiwa barua za utambulisho ili wakafungue akaunti benki au wakaripoti polisi wanapopotelewa na mali zao hasa wale ambao hawana vitambulisho vya taifa.

> Kwenye serikali za mitaa wananchi wanategemea kuona watu na siyo wakiwajibika kuwa wabishi ambao hata kama wamekosea wanasubiri hadi kuondolewa madarakani na mamlaka za juu.

Timu ya viongozi hawa wapya inasubiriwa ionekane ikiwajibika kutatua tatizo la ukosefu wa maji kwa maeneo mengi ya mijini na vijijini, kusaidia wananchi hasa kina mama na watoto wanaonyanyaswa kijinsia, kudhibiti ndoa za utotoni na kuzuia ukeketaji na mila zinazoongeza magonjwa na athari kwa wanawake.

Wanatarajiwa kuwasiliana na Mamala ya Maji Vijijini kutatua changamoto za maji, lakini pia kuwabana na kuwashirikisha viongozi wa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (Tarura) kujenga na kuboresha miundombinu ili wakulima wasafirishe mazao yao na pia kufikia masoko.

Lakini si hivyo viongozi hawa wanategemewa kusaidia kumaliza tatizo la ukosefu wa ajira kwa kushirikiana na vijana pamoja na wamachinga kutoa mapendekezo yanayowezesha kundi hili kupata kazi za kufanya na kujikimu maisha yao.

Pamoja na hayo wananchi wanatarajia kuona viongozi wa serikali za mitaa wakiwajibika kikamilifu wakifikiria na kutekeleza mikakati kuhusu mbinu za kuboresha maisha ya wananchi, mathalani jijini Dar es Salaam kuna uchafu wa kupindukia mambo hayo yapatiwe ufumbuzi.

Maeneo mengi yamejaa taka za nyumbani na taka ngumu kama magurudumu na viti vya plastiki wahakikishe kuwa wanawake utaratibu wa kuzoa takataka na kuufanya mji uwe safi.

Kwa upande wa vijijini viongozi hao wawahamasishe na kufuatilia wanawake kwenye vijiji na vitongoji waende kujifungua kwenye vituo vya afya, hospitalini na kufuata maelekezo ya wataalamu ili kuepusha vifo vya wazazi, wajawazito na watoto wadogo.

Ni wakati wa kutoa majibu ya changamoto hizo, ambazo kwa karibu miaka mingi zinawasumbua wananchi hasa katika ngazi za chini na si kusubiri hadi ujio wa viongozi wa juu na kulalamika kwa kuwabebea mabango.

Viongozi wanaotarajiwa ni waadilifu na wanaoendana na kasi ya ‘hapa kazi tu’ na kuhudumia wananchi tena walio mstari wa mbele kupambana na rushwa hasa rushwa ya ngono ambayo imeota mizizi kila mahali.

Ni muhimu kusaidia kuondoa usumbufu kwa wananchi ili wafikie huduma za kijamii na kupunguza malalamiko na umaskini ambao wakati mwingine unachangiwa na kukosa watu wa kuwaongoza wananchi.

Ikumbukwe kuwa awamu hii matatizo ya wananchi hayapuuzwi kwa mfano hospitali nyingi zina dawa muhimu, bima ya afya ya jamii imeboreshwa hivyo ni jukumu la viongozi kuwahamasisha wananchi kujitambua na kuchangamkia huduma hizo ili kubadili maisha yao.

Viongozi hao wapya wanawajibika pia kuwasaidia wakulima kupata pembejeo hasa mbolea yenye rutuba, mbegu hai zinazoota na kuzaa na kuwasaidia dhidi ya matatizo yanayohusiana ujanja unaotokana na viongozi wa vyama vya ushirika vya msingi ambao si waadilifu.

Kwenye serikali za mitaa wananchi wanategemea kuona watu wakiwajibika na siyo kuwa wabishi ambao hata kama wamekosea wanasubiri hadi kuondolewa madarakani na mamlaka za juu.

Viongozi kama walivyo mawaziri kwenye baraza la mawaziri wanatarajiwa kufanya mambo yenye kuzingatia maslahi ya taifa kama kuandaa mikataba ya kushirikisha wananchi yanapokuja masuala ya kuuza ardhi za vijiji.


Viongozi wa vijiji mara nyingi wametuhumiwa kuwa wanapindisha sheria ili kujinufaisha wenyewe kwa kuuza mali za vijiji kwa wageni jambo ambalo linalinda maslahi yao badala ya kutetea ulinzi na maliasili za wananchi vijijini.

Viongozi wengine wanatuhumiwa kuwa fedha za madarasa na michango ya wananchi jambo linalowakatisha tamaa na kurudisha nyuma maendeleo yao.

Viongozi hao wasiwe kuku wa kutaga na kutotoa matatizo yanayoongeza umaskini katika vitongoji na mitaa. Ni vyema pia viongozi hao wakaachana na kuendekeza udugu, kulinda maslahi ya jamaa zao na kutetea maslahi binafsi.

Kwa hiyo wawajibike kwa wananchi waliowachagua na wale, ambao hawakupiga kura kwa sababu jukumu lao ni kuwaongoza Watanzania bila kujali kuwa ni wa CCM, Chadema au CUF.

# Museveni alivyowateua, kuwatumbua mawaziri



Rais Yoweri Museveni wa Uganda. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Mashaka Mgeta**

WIKI iliyopita, Rais Yoweri Museveni wa Uganda alitangaza Baraza la Mawaziri baada ya kulifanyia mabadiliko kadhaa.

Katika mabadiliko hayo aliyoyatangaza jioni ya Jumamosi, mawaziri saba walitumbuliwa huku sura mpya tisa zikichomoza kwa uteuzi.

Gazeti la kila siku linalochapishwa nchini Uganda la The New Vision, linaandika makala haya yaliyotafsiriwa, likieleza uteuzi wa kwanza wa Baraza la Mawaziri katikati ya kipindi cha miaka 33 ya utawala wa Rais Museveni (pichani). Rais huyo ameshafanya mabadiliko kadha wa kadha ya mawaziri, wakati mwingine akiongeza idadi yao kwa kuunda wizara mpya.

Januari 29, 1986, Rais Museveni alikula kiapo cha kuwa Rais wa Uganda na kwa mara ya kwanza, akaunda baraza la mawaziri. Kwa mujibu wa gazeti hilo, baraza hilo lilikuwa na wajumbe wafuatao:-

> Kwa takribani miaka 14 akiwa katika Serikali ya Museveni, Kanali Besigye aliandika waraka wa kuishutumu serikali ya NRM. Rais alipendekeza afikishwe kwenye mahakama ya kijeshi.

**DK. PAUL KAWANGA SSEMOWOGERE**

Rais wa zamani wa chama cha Demokrasia (DP) aliteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani wa kwanza wa utawala wa Museveni, baadaye kuhamishiwa Wizara ya Mambo ya Mambo ya Nje katika serikali ya National Resistance Movement (NRM).

Baada ya kuwamo ndani ya serikali ya NRM kwa miaka nane, Ssemwogerere alijiuzulu, akaenda kuwania urais katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 1996. Baada ya hapo alishindwa, alistaafu kutoka katika chama hicho na kwenda kufanya shughuli binafsi.

**DK. RUHAKANA RUGUNDA**

Ni Waziri Mkuu wa sasa katika serikali ya Rais Museveni. Alikuwa miongoni mwa watu wa kwanza kuwamo kwenye Baraza la Mawaziri la kwanza la Museveni, akitumikia nafasi ya Waziri wa Afya mwaka 1986.

Dk. Rugunda alitumikia pia wizara mbalimbali kabla ya kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa akitokea Uganda. Wakati wa mzozo wa Museveni na aliyekuwa Waziri Mkuu, Amama Mbabazi, Dk. Rugunda alirejea Uganda na kuteuliwa kushika wadhifa huo wa Waziri Mkuu.

**PROFESA SHEM MASABA**

Huyu alijulikana kama 'waziri mtukutu' akitumikia Wizara ya Kilimo na Mifugo kwa kipindi cha mwaka mmoja, yaani kati ya 1986 na 1987.

Anakumbukwa kwa jinsi alivyokuwa akiwatuhumu mawaziri wenzake dhidi ya rushwa, mbele ya bunge.

"Mawaziri wote ni wala rushwa kwa sababau wanaishi maisha mazuri yasiyolingana na mishahara yao," kuna wakati alikaririwa akitamka bungeni. Baada ya kuondoka wizarani hapo alirejea kufundisha Chuo Kikuu cha Makerere, akastaafu na kujishughulisha na mambo binafsi.

**PROFESA EDWARD KAKONGE**

Alikuwa Waziri wa Serikali za Mitaa katika uteuzi wa mwaka 1986 na mwaka 1989, kama ilivyotokea kwa waliokuwa mawaziri wengi, alikwenda kuwania ubunge na akashindwa. Baada ya hapo alirejea kufundisha katika Chuo Kikuu cha Makerere.

**KANALI KIZZA BESIGYE**

Mwaka 1986, aliteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Kamisaa wa Siasa. Pia Kanali Besigye alitumikia nafasi mbalimbali serikalini na katika Jeshi la Wananchi wa Uganda (UPDF) ikiwamo Mkurugenzi wa Lojistiki.

Pia aliwahi kuwa kamanda wa batalioni maalum ya kijeshi ya Kasijajirwa huko Masaka.

Kwa takribani miaka 14 akiwa katika Serikali ya Museveni, Kanali Besigye aliandika waraka wa kuishutumu serikali ya NRM. Rais alipendekeza afikishwe kwenye mahakama ya kijeshi.

Aliepuka kufikishwa mahakamani hapo, badala yake 'akabadili gia' na kutangaza mpango wake wa kuwania urais mwaka 2000.

Pia aliunda vuguvugu la kisiasa la Agenda ya Mageuzi lililosababisha kuanzishwa kwa Chama cha Forum for Democratic Change.

Dk. Besigye amekuwa mgombea urais 'tisho' kwa Rais Museveni katika uchaguzi mkuu wa 2001, 2006, 2011 na 2016.

**KAPTENI GERTRUDE NJUBA**

Alikuwa Naibu Waziri Ustawi wa Jamii. Hata hivyo, alishika wadhifa huo kwa muda mfupi ingawa alibaki kuwa mwanasiasa maarufu serikalini. Hivi sasa, Njuda anaongoza Idara ya Ardhi katika Ofisi ya Rais.

**ISRAEL KAYONDE**

Kayonde alikuwa mmoja wa wanachama wa National Resistance Council (NRC) iliyounda bunge la nchi hiyo. Baadaye Kayonde alistaafu na kujishughulisha na masuala binafsi.

**ROBERT KITARIKO**

Kitariko aliteuliwa kuwa Waziri wa Kilimo katika baraza la kwanza la Museveni. Baadaye alirejea kwenye chama chake, ingawa si kwa ushiriki mpana, hadi mwaka 2001alipoteuliwa kuwa Kamishna wa Tume ya Uchaguzi.

Kitariko aliyekuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Democratic Party (DP) pia aliwahi kuwa Waziri wa Utumishi wa Umma. Alifariki mwaka 2016.

**SEBANA KIZITO**

Ni kiongozi wa zamani wa chama cha DP na mgombea urais. Alikuwa Waziri wa Tawala za Mikoa wa kwanza katika serikali ya NRM. Aliwahi pia kuwa Waziri wa Ushirika na Masoko.

Alichaguliwa kuwa Meya wa Jiji la Kampala mwaka 2001, kisha akawania urais katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2006 alishindwa na kuamua kustaafu siasa za jukwaani.

**AMANYA MUSHEGA**

Alikuwa Naibu Waziri wa Ulinzi aliyeteuliwa pia kushika nafasi mbalimbali ikiwamo uwaziri.

Mushenga aliachana na siasa za ndani ya Uganda baada ya kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa kwanza wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) iliyofufuliwa na makao makuu yake kuwa Arusha.

Baada ya kumaliza muda wa utumishi wake katika EAC, Mushega alirejea Uganda na kuendelea na siasa za majukwaani katika chama chake cha FDC.

**KAHINDA OTAFIIRE**

Alianza kama Naibu Waziri wa Serikali za Mitaa, na akatumikia wizara nafasi mbalimbali, kabla ya kutakiwa kujiuzulu siasa kutokana kumwonyeshea bastola mke wa mmoja wa mawaziri mwenzake kwenye hoteli ya Fairway. Rais Museveni 'alimtumbua' kutoka kwenye uwaziri mwaka 1999.

Baada ya kutumbuliwa, Otafiire alizungumza na vyombo vya habari vya Uganda, akielezea kutoridhishwa kwake na hatua hiyo.

Hivi sasa ni Waziri anayeshughulikia Jumuiya ya Afrika Mashariki, akitokea Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba.

**MAYANJA NKANGI**

Kwanza aliteuliwa kuwa Waziri wa Elimu mwaka 1986, kisha akatumikia katika wizara mbalimbali ikiwamo Wizara ya Fedha. Baada ya kuondoka kwenye uwaziri, aliteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Tume ya Ardhi akafanyakazi kwa miaka 10.

**KIRUNDA KIVEJINJA**

Alikuwa Waziri wa kwanza wa ustawi wa jamii. Baadaye, akiwa wa usafirishaji, alijiuzulu alipokuwa katika 'tanuru' la kushughulikiwa na bunge akihusishwa na upotevu wa maelfu ya lita za mafuta kutoka shirika la reli la nchi hiyo.

**JOHN NTIMBA**

Mwaka 1986, Ntimba aliteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Elimu ya Juu. Ni mtumishi wa umma mwandamizi ambaye hakutumikia katika wizara nyinginezo. Baada ya kutoka kwenye uwaziri, aliteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Uteuzi ya Chuo Kikuu cha Makerere.

**DK. CRISPUS KIYONGA**

Alianza kwa kuwa Waziri wa Ushirika na Masoko mwaka 1986, kisha akahamishiwa Wizara ya Fedha kuchukua nafasi ya Profesa Ponsiano Mulema aliyefariki dunia. Dk. Kiyonga alikuwa nje ya uwaziri kwa miaka kadhaa, baadaye alirejeshwa akiwa Waziri wa Afya. Hivi sasa ni Balozi wa Uganda nchini China mwenye makazi yake jijini Beijing.

**VICTORIA SEKITOLEKO**

Alianza kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Kilimo na baadaye alipanda kuwa Waziri kamili katika wizara hiyo.

Baadaye, Sekitoleko alikwenda kufanya kazi Umoja wa Mataifa (UN) akiwa Mkuu wa Shirika la Umoja wa Taifa la Chakula na Kilimo (FAO) Kanda ya Afrika ya Kati, akiwa jijini Harare, Zimbabwe.



# Ufisadi wamchefua Jafo ujenzi kituo afya

Na Nebart Msokwa, CHUNYA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, amekerwa na ufisadi uliofanywa na baadhi ya wasimamizi wa serikali kwenye ujenzi wa Kituo cha Afya cha Mtande katika Halmashauri ya Wilaya ya Chunya.

Kituo hicho ni miongoni mwa vituo 14 vya afya ambavyo vinajengwa na serikali kwa kushirikiana na wananchi mkoani Mbeya kupitia mfumo wa akaunti ya dharura (Force account) ambao unahamasisha matumizi ya mafundi wa mitaani badala ya makandarasi.

Akizungumza na watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya juzi, Jafo aliagiza vyombo vya dola kuwashughulikia ipasavyo wote watakaobainika kuhusika na ufisadi huo baada ya timu iliyoundwa na Mkuu wa Mkoa kuchunguza mradi huo kukamilisha kazi.

Alisema taarifa zinaonyesha kuwa kuna vifaa vingi vya mradi huo vimechakachuliwa, hivyo kusababisha uchelewa kukamilika na hata ubora wake unatia shaka tofauti na vituo vingine vilivyojengwa mkoani humo kikiwamo cha Chalangwa.

"Nilitaka niunde timu ya Tamisemi kuja kuchunguza mradi huo, lakini kwa sababu Mkuu wa Mkoa ameshaunda tume yake nataka iendelee na kazi na ikishamaliza vyombo vya dola wakiwamo Takukuru washughulike na watu hao ikiwamo kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria," alisema Waziri Jafo. Alisema mafisadi hao walitumia mwanya wa kilipo kituo hicho kutofikika mara kwa mara na viongozi kutokana na umbali, kuhujumu mradi ambapo alisema umbali wa zaidi ya kilomita 90 kutoka Chunya mjini.

Aidha, alimpongeza Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila kwa kushirikiana na viongozi wa juu wa Wilaya ya Chunya kwa kushtukia mchezo mapema na kuamua kuunda Tume kwa ajili ya kuchunguza.

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa miradi ya vituo vya afya katika Wilaya ya Chunya, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Chalamila alisema vituo viwili kati ya 14 vinavyojengwa Mbeya vipo Chunya.

Alisema Kituo cha Chalangwa tayari kimekamilika isipokuwa hicho cha Mtande ambacho kinanuka ufisadi ndio bado na hivyo akaahidi kuendelea kushirikiana na wasaidizi wake kushughulikia tatizo lililopo.

Aidha, alimwomba Waziri Jafo kusaidia kufuatilia ahadi iliyotolewa na Rais Dk. John Magufuli wakati wa ziara yake katika Wilaya hiyo aliyoahidi kutoa Sh. milioni 200 kwa ajili ya upanuzi wa Hospitali ya Wilaya ya Chunya na Sh. milioni 200 zingine kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Makongolosi.

"Wilaya hii imegawanyika katika kanda mbili ambazo ni ukanda wa madini na ukanda wa kilimo na kuna ongezeko kubwa la watu, sasa tunaomba utusaidie ahadi ya Rais kwa ajili ya kuboresha miundombinu hii ya afya ili kuendana na mahitaji," alisema Chalamila.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Mariam Mtunguja, alipendekeza Hospitali ya Wilaya ya Chunya iendelee kuwa kituo cha afya na uanzishwe mradi mpya wa hospitali ya wilaya kwa maelezo kuwa hospitali hiyo haina hadhi.

Alisema eneo la hospitali hiyo ambalo ni ekari tano halitoshi ni ikiwezekana fedha alizoahidi Rais zitumike kwenye uanzishwaji wa mradi mpya wa hospitali.

Alisema endapo wilaya hiyo itapata Sh. bilioni 1.5 kama ilivyokuwa kwa Halmashauri za Mbarali, Mbeya na Busokelo, kuna uwezekano wakajenga hospitali kubwa na yenye hadhi ya wilaya.

Hata hivyo, Waziri Jafo alikiri hospitali hiyo kutokuwa na hadhi ambapo alisema baadhi ya majengo yake ni ya zamani na hayana sifa.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, akizungumza na watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya juzi (kulia kwake ni Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila na Katibu Tawala wa Mkoa huo, Marian Mtunguja. Kulia ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, Bosco Mwanginde. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# RC ahamasisha kujiunga bima ya vifurushi

Na Mwandishi Wetu, MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, amewataka Watanzania kujikatia bima ya afya kwa mpango wa vifurushi na kuwapuuza baadhi ya watu wanaohusisha siasa na mpango huo ulioletwa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) ili kuwafikia Watanzania wengi zaidi.

Chalamila aliyasema hayo juzi wakati wa uzinduzi wa kampeni ya kuhamasisha wananchi kujiunga na vifurushi vya bima ya afya katika mkoa wa Mbeya, uzinduzi ambao ulifanyika katika kituo cha daladala cha Kabwe jijini Mbeya.

Alisema kuwa nchi yoyote ili iweze kujipatia maendeleo katika sekta zote ni muhimu kwa wananchi kuwa na afya bora na ndio maana serikali imeendelea kuwekeza katika sekta hiyo ikiwamo kuja na vifurushi vya bima ya afya ili kila mwananchi achaguwe ambacho anaona kinamfaa.

"Ndugu zangu afya haina siasa, afya ni uhai tusidanganywe, tujitenge na siasa za kupotoshwa juu ya mfumo huu wa bima, awali kwa mtu mmoja ilikuwa ni lazima uwe na zaidi ya milioni moja ili kuwa na bima ya afya, lakini kwa utaratibu huu wa vifurushi sasa unapata kadi ya bima ya afya kwa sh. 192,000 pekee," alisema Chalamila.

Aliongeza kuwa ugonjwa hauna hodi ni vizuri kila Mtanzania kufanya maamuzi ya kujikatia bima kwani wapo watu wengi wamekuwa wakipoteza maisha kutokana na gharama kubwa za matibabu, hivyo mfumo huu wa vifurushi ni suluhisho kwa changamoto hiyo.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, Anne Makinda, alisema kuwa tangu kuzinduliwa kwa mfuko huu mwitikio wa Watanzania umekuwa ni mkubwa.

Pia Makinda aliwataka watoa huduma kubadilika na kuwahudumia vizuri wananchi waendapo kupata huduma za afya kwani mfuko hautotoa kibali kwa hospitali yoyote ambayo itanyanyasa wanufaika wa bima. Kaimu Mkurugenzi wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, Christopher Mapunda, alisema uanzishwaji wa vifurushi ni fursa kwa wananchi kujiunga na bima ya afya kuanzia kiwango cha Sh. 192,000 na kuwawezesha kupata huduma ya uhakika ya matibabu hasa kutokana na kuongezeka kwa gharama za matibabu siku hadi siku.

# Mashauri 1,500 ardhi yatatuliwa

Na Grace Mwakalinga, MBEYA

MASHAURI 1,564 yanayohusu ardhi na ndoa yametatuliwa katika kipindi cha mwaka 2018, huku mashauri mengine 514 yakikatiwa rufani.

Rufani hizo zimepelekwa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS) hatua ambayo imesaidia wananchi kupata huduma za kisheria kwa urahisi kupitia kwa wasaidizi wa kisheria.

Hayo yalisemwa na Mratibu wa Shirika lisilokuwa la kiserikali linalotoa huduma ya msaada wa kisheria mkoani Mbeya (Mbepace), Laiki Ndagile, wakati wa kuhitimisha mafunzo ya kisheria kwa wanafunzi 21 kutoka wilaya mbalimbali mkoani humo.

Ndagile alisema shirika hilo ambalo lengo lake ni kutoa huduma ya kisheria pamoja na mafunzo kwa wananchi, limekuwa chachu ya kuleta mabadiliko kupitia elimu wanayoitoa kwenye jamii kuhusiana na masuala mbalimbali ikiwamo, ndoa, ardhi na unyanyasaji wa kijinsia.

"Tumeweka utaratibu wa kuwafundisha wananchi masuala ya kisheria kutoka kila kata na wakihitimu siku 15 wanakuwa na sifa ya kutoa huduma ya msaada wa kisheria, lengo ni kupunguza gharama na usumbufu kwa wananchi wasio na uwezo kuwafikia mawakili wa kijitegemea," alisema Ndagile.

Alisema idadi ya mashauri 1,564 ambayo yalitatuliwa kabla ya kufika ngazi za juu za mahakama inatoa picha kuwa wasaidizi wa kisheria wamekuwa na mchango mkubwa kwenye utoaji wa huduma ya kisheria licha ya kuwa bado zipo changamoto zinazowakabili katika kutekeleza majukumu yao.


Alisema hadi sasa Mkoa wa Mbeya una jumla ya wasaidizi wa kisheria 81 hitaji likiwa ni zaidi ya 150 ili kutoa huduma bora kwenye kila kata na kwamba wananchi 21 waliohitimu wataenda kupunguza changamoto ya uhaba huo.

Mmoja wa wanafunzi waliohitimu mafunzo ya msaada wa kisheria kutoka Kata ya Kongoro Mswisi wilayani Mbarali, Rehema Mwapasi, alisema kupitia elimu hiyo atakwenda kuihudumia jamii yake bila gharama yoyote ili haki itendeke.

Isabela Kapufi kutoka Kata ya Igawilo jijini Mbeya, alisema elimu hiyo itamsaidia kushughulikia migogoro mingi kwenye mabaraza ya ardhi ya kata ambako wanawake wengi hunyimwa haki zao.

Katibu Tawala Msaidizi anayesimamia mipango na miradi mkoani Mbeya, Conrad Millinga, aliwashauri wasaidizi hao wa kisheria kujiendeleza kielimu ili wawe wabobezi katika masuala ya sheria.

Alipongeza hatua ya Shirika la Mbepace kutoa mafunzo ya msaada wa kisheria kwa wananchi na kwamba hatua hiyo imesaidia kuziba mwanya wa uhaba wa wanasheria katika kuwahudumia wananchi.





## 330 wasajiliwa CHF Dodoma

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imesajili jumla ya wanachama 330 katika utekelezaji wa zoezi maalum la uhamasishaji wananchi kujiunga na bima ya afya ya jamii iliyoboreshwa (CHF) iliyofanyika katika kata ya Chang'ombe.

Akizungunza baada ya zoezi hilo mratibu wa CHF iliyoboreshwa, Patrick Sebyiga, alisema zoezi hilo limeanza kwa mafanikio makubwa katika kata hiyo ya Chang'ombe.

Sebyiga alisema kuwa idadi ya kaya zilizosajiliwa ni 55, zenye jumla ya watu 330 kwa maana hiyo Kata ya Chang'ombe imetoa picha halisi kuwa zoezi la usajili linatakiwa kuendelea kwenye maeneo mengine ya Jiji la Dodoma.

"Timu yangu ya wataalamu na wahamasishaji imeendelea kuwaelimisha wananchi tofauti ya CHF ya awali na CHF hii iliyoboreshwa na baada ya kuelewa wananchi wamekuwa wakijiunga," alisema mratibu huyo.

Akiongelea tofauti baina ya CHF ya awali na iliyoboreshwa, alisema CHF iliyoboreshwa huduma zake zimeboreshwa na ndiyo maana wananchi wamechangamkia kujiunga.

"CHF ya awali ilikuwa usajili unafanyika kwa kujaza fomu na baada ya hapo unasubiri mwezi mmoja ndiyo uanze kupata huduma ya matibabu, lakini kwa CHF iliyoboreshwa ni ya kidigitali ambayo usajili na kadi yako unapewa papohapo na huduma ya matibabu kuanza mara moja," alisema Sebyiga.

Tofauti nyingine aliitaja kuwa CHF iliyopita, walengwa wengi hawakuwa wanapata huduma ya tiba na dawa katika vituo vya afya. "Sasa huduma zimeboreshwa zaidi," alisema.

Alisema hivi sasa matibabu hutolewa kuanzia ngazi ya zahanati. Pale ambapo mgonjwa anahitaji rufani basi utaratibu wa rufani hufanyika kwenda kituo cha afya, hospitali ya wilaya hadi hospitali ya rufani ya mkoa.

"Hii yote ni kuunga mkono juhudi za Rais John Magufuli za kumhakikishia mwananchi huduma bora za matibabu. Matibabu sasa ni nchi nzima katika vituo vya afya na hospitali za serikali," alisema Sebyiga.

Alisema zoezi la uhamasishaji ni endelevu litakalofanyika katika kata zote 41 za Halmashauri ya Jiji la Dodoma.

# Mkakati wa pili wazinduliwa kuendeleza zao la mpunga

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

SERIKALI imezindua mkakati wa taifa wa awamu ya pili wa miaka 10, wa kuendeleza zao la mpunga nchini ili kuhakikisha wanafikia hekta milioni moja ifikapo mwaka 2025.

Hayo yalibainishwa jana na Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, ambapo alisema lengo ni kuona wanaongeza uzalishaji wa zao la mpunga ifikapo 2030, kusiwe na njaa pamoja na kuongezeka kwa biashara ya zao hilo.

Alisema amefarijika kusikia Tanzania imeshika nafasi ya nne kuzalisha mpunga, lakini atafarijika zaidi kusikia imeshika nafasi ya kwanza au ya pili.

"Sijafurahi sana kuona tunapitwa na Misri na Madagascar wakati wao hufanya kilimo cha mpunga cha umwagiliaji, nahitaji kuona tunakuwa juu yao hapo baadaye, " alisema Hasunga.

Alisema kuna kila sababu ya kusonga mbele katika zao hilo hasa ukizingatia ni zao pendwa na kila mtu, na kwamba nchi inaweza kutoa mchele safi na bora ambao utauzwa nje. Alisema mkakati huu wa miaka 10 wa awamu ya pili unaonza 2019 -2030, ukawe chachu ya maendeleo ya wakulima wa zao hilo nchini.

Alisema wizara yake itatekeleza uongezekaji wa mbegu bora, kuongeza eneo toka milioni 1.1 hadi 2.2 ifikapo 2030, kuongeza thamani ya mpunga.

Aidha, alisema bado sekta za fedha hazijawekeza katika kilimo, pia uwekezaji bado haukidhi mahitaji ya kilimo.

Kadhalika, Hasunga alisema bado kuna uhaba wa mbegu nchini, ambapo mahitaji ni taji 186,000 wakati zinazopatikana kwa sasa ni tani 57,000.

Alisema wakulima wamekuwa wakilima kilimo cha hasara, na kuwa kwa sasa mikakati ni kuhakikisha wengi wanalima kilimo cha biashara.

Alisema bado kuna uhaba wa mbegu nchini ambapo mahitaji ni taji 186,000 wakati zinazopatikana kwa sasa ni tani, 57,000 pekee.

Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Methew Mtigumwe, alisema mkakati huo uliozinduliwa ni mwendelezo wa matokeo ya utekelezaji wa mkakati wa awali wa kuendeleza zao la mpunga NDRS I ambapo ili kuongeza kiwango cha uzalishaji uliowekwa, ni lazima kupanua maeneo yanayofaa kwa kilimo cha mpunga kwa umwagiliaji na yanayotegemea mvua.

" Tanzania tumedhamiria kuongeza uzalishaji wa mpunga mara mbili zaidi kutoka tani 2.2 kwa sasa hadi tani 4.5 ifikapo 2030, na hili litafanikiwa kwa kutumia kilimo cha umwagiliaji, mbegu bora, mbolea, dawa zinazofaa na zana bora za kilimo ikiwamo kupunguza upotevu kabla na baada ya mavuno," alisema Mtigumwe.



Wanachama wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa (TALGWU), wakimsikiliza Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga (hayupo pichani), wakati alipokuwa akifungua mkutano mkuu wa kazi wa miaka miwili na nusu uliofanyika mkoani Dodoma jana. **PICHA PETER MKWAVILA**

# Magonjwa yanayotafuna fedha NHIF haya

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

MFUKO wa Bima ya Afya wa Taifa (NHIF), umesema ugonjwa wa saratani ndio unaoongoza kutumia fedha nyingi kumtibu mgonjwa kwa siku, ikifuatiwa na kipimo cha MRI ambacho nacho kina gharama kubwa.

Aidha, NHIF imesema mpaka sasa inahudumia wastaafu 473, 393 katika mfuko huo ambao walikuwa watumishi wa umma.

Akizungumza katika semina ya wanahabari Meneja Masoko wa NHIF, Hipoloti Lelo, alisema magonjwa hayo yanatumia fedha nyingi kwa mwaka tofauti na magonjwa mengine.

Lelo alisema kutokana na hilo ndio maana wameamua kuanzisha mfumo huo wa vifurushi vipya vya Timiza, Najali na Wekeza ili kila mwananchi aweze kujipimia anachotaka ili apate matibabu haraka pale anapopata maradhi.

"Tunaomba wananchi muelewe hivi vifurushi sio biashara bali vina lengo la kutaka kumfikia kila Mtanzania aweze kupata matibabu," alisema Lelo.

Akitolea mfano ugonjwa wa figo alisema kusafisha kwa siku ni Sh. 300,000 na unakuta mtu anafanyiwa mara nne kwa siku ambapo ni sawa na Sh. 1,200,000 katika hali ya kawaida bila bima mtu hawezi kumudu," alisema Lelo.

Kutokana na hilo, alisema kuna kila sababu ya wananchi kujipimia na kuchagua kifurushi ambacho ni saizi yako ili ujiwekee kinga kabla ya kuugua.

Alisema wao NHIF lengo lao ni kuona elimu ya watu kuwa na bima ya afya ya NHIF inawafikia nchi nzima.


Akitolea ufafanuzi aina ya vipimo vya maabara ambavyo vinapatikana alisema katika kifurushi cha Najali Afya jumla ya vipimo 162 vinapatikana ikiwamo X-RAY, ECHO na EEG, na Ultrasound, wakati cha Wekeza Afya vipimo 197 vya maabara vinapatika, hivyo vitatu ambavyo vimeainishwa, huku kifurushi cha Timiza vipimo 223 vya maabara vinapatikana.

Alisema hakuna ssbabu ya kurudi nyuma kila mmoja anapaswa kukata bima ya afya ambayo itamsaidia kujikinga wakati anapofikwa na maradhi.

Akizungumzia suala la huduma kwa wastaafu, alisema idadi wanayoihudumia ndio hiyo ilioainishwa hadi sasa.

Naye Meneja Uhusianao wa NHIF, Angella Mziray, aliwataka wanahabari kwenda kutoa elimu ya kutosha kupitia kalamu zao ili wananchi wapate uwelewa kuhusu kutumia bima ya afya.

Alisema moja ya mikakati waliojiwekea NHIF ni kuhakikisha wananchi wote vijijini na mijini wanakuwa na uwelewa wa matumizi ya bima ya afya.



# Ajali barabarani zaendelea kuwa tishio

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WATU 12 wamefariki dunia kwa Novemba mwaka huu kutokana na ajali za barabarani Zanzibar.

Akiwasilisha takwimu za ajali na makosa ya barabarani kwa waandishi wa habari, mtakwimu kutoka kitengo cha makosa ya jinai, madai na jinsia Asha Mussa Mahfoudh, alisema kuwa watu hao 12 waliofariki dunia ni miongoni mwa ajali 33 zilizotokea mwezi huo.

Alisema katika ajali hizo waathirika ni 105 kati ya hao 64 ni wanaume na 21 ni wanawake na waliojeruhiwa ni 93.

Pia alisema mlinganisho wa idadi za ajali za barabarani kwa mwezi uliopita zimeongezeka kutoka ajali 32 kwa mwezi wa Oktoba , 2019 hadi 33 Novemba 2019.

Alisema makundi yaliyoathirika katika ajali hizo ni pamoja na waendao kwa miguu, madereva, waendesha baskeli, pikipiki na abiria.

Alieleza kuwa makosa yote hayo ya barabarani yamefanywa na madereva wanaume kwa sababu mbalimbali ikiwamo uzembe.

"Tunawapongeza sana madereva wanawake maana kwa mwezi wa Novemba hakuna ajali iliyosababishwa na wao," alisema mtakwimu huyo.

Alisema Wilaya ya Mjini, Magharibi 'A' na Magharibi 'B' Unguja zinaongoza zaidi kwa makosa ya kushindwa kuvaa sare na beji kwa utingo na dereva wa gari za abiria, kutofuata miongozo na kanuni za usalama barabarani.

Aidha, alisema makosa mengine ni pamoja na kuendesha chombo cha moto bila ya leseni, bima na leseni ya njia, kuendesha chombo cha moto bila ya kuvaa kofia ngumu na kuzidisha idadi ya abiria na mizigo.




Waziri wa Utumishi wa Umma na Utawala Bora Zanzibar, Haroun Ali Suleiman, akimkabidhi Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, tuzo maalumu kwa kutambua mchango wake mkubwa katika kukuza utawala bora nchini. **PICHA: MARTIN KABEMBA.**

# Dk. Shein ajivunia utawala bora

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amesema kuwa serikali imefanya bidii kuhakikisha misingi ya utawala bora inafuatwa ili kukuza uchumi na kujenga jamii yenye imani, upendo na mshikamano.

Akizungumza wakati wa maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu yaliyofanyika katika ukumbi wa Sheikh Idrisa Abdul Wakili,

Kikwajuni mjini Zanzibar, aliitaja misingi hiyo kuwa ni ushirikishwaji wa umma, utawala wa sheria, haki na usawa kwa watu wote, uwazi katika kuendesha shughuli za maendeleo pamoja na uwajibikaji katika utendaji na uadilifu.

Alieleza kuwa hatua mbalimbali zilizochukuliwa na serikali kuona kwamba utawala bora unaimarika ikiwa ni pamoja na kupitisha sera ya utawala bora ya mwaka 2011, ambayo utekelezaji wake unasaidia katika kuyafikia malengo ya mkataba wa haki za binadamu na mapambano dhidi ya rushwa.

Alieleza kuwa Tanzania ni nchi ya kwanza kuanzisha Wizara ya Utawala Bora katika nchi za Afrika, hatua ambayo imeijengea sifa kubwa ndani na nje ya Afrika.

Alieleza katika msingi wa ushirikishwaji wa umma, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ imeainisha mfumo wa ugatuzi kwa kuzingatia umuhimu wa utekelezaji wa sheria namba 7 ya mwaka 2014 ili kukasimu baadhi ya madaraka kwa wananchi.

Alisema kwa madhumuni ya kuzilinda haki za watoto, serikali imewajengea watoto mazingira mazuri ya kutoa ushahidi kwa kuanzisha mahakama za watoto katika mikoa yote mitano ya Zanzibar.

Aidha, alisema kwamba kuwako kwa utekelezaji wa haki sawa kwa kila binadamu na utawala bora ni miongoni mwa misingi ya utawala bora.

Alisema harakati za usimamizi na ulinzi wa haki za binaadamu Zanzibar zilianza zamani kabla ya Mapinduzi ya Januari 12, 1964, ambapo katika hatua hiyo Rais wa mwanzo wa Zanzibar, Hayati Mzee

Abeid Amani Karume baada ya mapinduzi alipiga marufuku utaratibu wa mikopo ya fedha kwa njia ya kuweka vitu rehani (pawn).

Alieleza kuwa katika kuhakikisha haki na usawa vinatekelezwa kwa wote, serikali imeanzisha tume ya utumishi serikalini katika jitihada za kuhakikisha haki za wananchi zinalindwa, utendaji wa kazi unafanywa na vitendo vya unyanyasaji vinaondoka sehemu za kazi.

Hata hivyo alisema serikali imekuwa ikiongeza nafasi za uongozi kwa wanawake na kutolea mfano kuwa katika Baraza la Wawakilishi la mwaka 2015-2020 la hivi sasa idadi ya wajumbe wanawake imefika 32 ikilinganishwa na wajumbe 26 wa Baraza la Wawakilishi la mwaka 2010-2015 na lile la 2015-2010 ambalo lilikuwa na wajumbe 20.

Alisema miongoni mwa wajumbe hao wanawake wapo watano wanaoongoza wizara mbalimbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na kuwapo kwa nafasi za makatibu wakuu, makatibu watendaji na wakurugenzi.

Naye Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, alimpongeza Dk. Shein kwa jitihada zake za kuimarisha utawala bora akiwa ni mwasisi wa wizara hiyo.

# Wito jamii kubadilika kimalezi

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MKUU wa Mkoa Mjini Magharibi, Hassan Khatib Hassan, ameitaka jamii kubadilika katika mfumo mzima wa makuzi na malezi ili kuwasaidia watoto kuepukana na vitendo vya udhalilishaji .

Aliyasema hayo alipofungua kongamano la wasaidizi wa sheria lenye lengo la kupiga vita udhalilishaji dhidi ya wanawake na watoto.

Alisema jamii iwe tayari kuanzisha mbinu shirikishi katika malezi na makuzi ya watoto wao kwa kuwa na uwezo wa kuwafuatilia nyendo zao kwa wakati wote ili kuwaepusha na vitendo hivyo.

Aidha, alisema malezi yaliyopo hivi sasa yemeweza kubadilisha mila, silka na tamaduni za Kizanzibar jambo ambalo linachangia udhalilishaji.

"Iwapo mzazi au mlezi anampeleka mtoto mdogo katika sherehe za harusi jambo hili ni kinyume cha maadili yetu tuliyoyazowea na inachangia vishawishi," alisema.

Alieleza kuwa utandawazi umeiharibu jamii kwa kuutumia vibaya, hivyo iko haja ya kukaa na watoto kuwapa mafunzo mema katika maisha yao ya baadaye ili kujielewa.

Alisema kuwa wakati umefika sasa kutazama chanzo cha tatizo la udhalilishaji dhidi ya wanawake na watoto.

Naye Mkurugenzi wa Jumuiya ya Wanasheria Wanawake Zanzibar, Jamila Mohamoud, aliwataka wasaidizi wa sheria kuisaidia jamii ili kuitetea haki ya mwanamke na mtoto kutokana na kukosa uelewa, jambo linalochangia kutokuwa na imani na mahakama.

Mwanasheria kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ramadhani Nasibu, alisema rushwa bado imekithiri katika ngazi zote, hivyo kuwa kikwazo kwa jamii kutetea haki zao.

Washiriki wa kongamano hilo walisema bado elimu inahitajika kwa jamii ili kuisimamia haki isipotee.

**"Iwapo mzazi au mlezi anampeleka mtoto mdogo katika sherehe za harusi jambo hili ni kinyume cha maadili yetu tuliyoyazowea na inachangia vishawishi," alisema.**

# Mimba shuleni sasa zapungua

**Na Elisante John, SINGIDA**

IDADI ya wasichana wanaopata mimba wakiwa shuleni imepungua kutoka 54 kwa kipindi cha mwaka jana (2018) hadi 18 mwaka huu (Novemba), katika shule za msingi na sekondari zilizopo katika mkoa wa Singida.

Kwa mujibu wa Ofisa Elimu Sekretarieti ya Mkoa wa Singida, Nelasi Mulungu, kwenye orodha hiyo wasichana wa shule za sekondari wapo 15, na wengine watatu wanatoka shule za msingi.

Akizungumza kwenye kikao cha Kamati ya Ushauri Mkoa (RCC), Mulungu alifafanua kuwa idadi hiyo safari hii imepungua kutokana na ushirikiano baina ya wazazi, jamii, walimu na wanafunzi.

Hata hivyo, aliitaka jamii kushirikiana na serikali ili kutokomeza tatizo hilo, na akawataka wasichana kujitambua na kujiona wana thamani kubwa siku za usoni katika kuchangia maarifa kwa ajili ya maendeleo ya familia na taifa kwa ujumla.

Aidha, Mulungu alizitaka halmashauri za wilaya kujenga hosteli ili kukabiliana na tatizo hilo pamoja na kuongeza kasi ya ujenzi wa vyumba vya madarasa, maabara na nyumba za walimu ili kuboresha mazingira ya utoaji na upatikanaji wa elimu bora.

Kuhusu upungufu wa walimu, alisema mahitaji bado ni makubwa, huku akibainisha kuwa serikali itaendelea kukabiliana na changamoto hizo kadiri fedha zitakapopatikana, lengo likiwa ni kuhakikisha elimu inakuwa bora zaidi.

Alitoa ufafanuzi huo, baada ya kutakiwa na wajumbe wa kikao aeleze hali halisi ya tatizo la mimba shuleni mwaka huu katika mkoa wa Singida ikilinganishwa na mwaka jana.

Katika hatua nyingine, Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi, alipiga marufuku majengo yaliyoezekwa kwa nyasi kwenye shule shikizi, zilizojengwa kwa nguvu ya wananchi, ambazo zipo wilayani Manyoni.

"Sikubaliani kabisa na hali hii, ninatoa muda wa miezi sita shule hizo zilizojengwa kwa nyasi ziwe zimefunikwa bati...haiwezekani Singida iwe na shule za aina hiyo, labda mikoa mingine, lakini siyo hapa Singida. Mkuu wa Wilaya, hakikisha unadhibiti tatizo hili," aliagiza.

Alitoa agizo hilo, baada ya kuelezwa kwenye kikao hicho kuwa kuna shule shikizi ambazo majengo yake yameezekwa kwa nyasi, hivyo kuchangia mazingira magumu kwa wanafunzi kujifunzia.

# Hakimu aonya rushwa wasaidizi kisheria

**Na Marco Maduhu, KAHAMA**

WAHITIMU 80 wa mafunzo ya awali ya sheria kutoka halmashauri sita za mkoa wa Shinyanga, wameonywa kutojihusisha na vitendo vya rushwa wanapokuwa wakitoa huduma ya kisheria kwa wananchi.

Lengo la mafunzo hayo ni kuwasaidia wananchi kupata haki zao na kutokomeza vitendo vya jinai katika jamii.

Onyo hilo lilitolewa na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Kahama, Evodia Kyaruzi, wakati akifunga mafunzo ya siku 15 ya wasaidizi wa kisheria, yaliyotolewa na Shirika lisilo la Kiserikali la Paralegal Aid Center Shinyanga (PACESHI).

Alisema kwenye jamii kuna matukio mengi ya jinai yanajitokeza, vikiwamo vipigo, ubakaji, mimba za wanafunzi, migogoro ya mashamba, mirathi, lakini kuna baadhi ya wananchi wamekuwa wakikosa kupata haki zao kutokana na kutozijua sheria, hivyo wasaidizi hao wa kisheria ndio wanawategemea kupata haki zao na wasiwaombe rushwa.

"Rai yangu kubwa kwenu nyie wasaidizi wa kisheria ambao mmepewa mafunzo na kuhitimu, nendeni mkatende haki kwa wananchi pale mnapokuwa mnatoa huduma kwao za sheria katika kupata haki zao, na msiende kutumia fursa hii ya sheria kuanza kuomba rushwa," alisema Kyaruzi.

"Katoeni huduma za kisheria vizuri kwa wnanachi wasiojiweza, wakiwamo wazee, watoto na wajane ambao haki zao zinaonekana kupokwa na watu wengine hasa wenye uwezo wa kifedha, ili waweze kupata masaada zaidi na kupata haki zao kwa mujibu wa sheria kupitia mahakama," aliongeza.

Naye Mkurugenzi wa Shirika la PACESHI mkoani Shinyanga, Perepetua Magoke, ambao wanajihusisha na utoaji wa msaada wa kisheria bure kwa wananchi mkoani humo, alisema wametoa mafunzo hayo kwa wasidizi hao 80, ili kuongeza nguvu ya kusaidia wanyonge kupata haki zao na kutomeza matukio ya jinai.

Alisema wasaidizi hao wa kisheria kutoka halmashauri sita za mkoa wa Shinyanga ambazo ni Msalala, Ushetu, Kahama mji, Kishapu, Manispaa ya Shinyanga na Vijijini, wamepewa mafunzo ya sheria mama ya msaada wa kisheria (Legal Aid Act No 1/2017), ili watambue mbinu mbalimbali za kuwasaidia wahitaji ili kupata msaada stahiki wa kisheria.

Nao baadhi ya wahitimu hao wa mafunzo hayo akiwamo Esther Enock kutoka Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama, alisema mafunzo hayo yamekuwa msaada mkubwa kwao kwa kuwa awali hawakuwa na uelewa kuhusiana na sheria, ambapo sasa watawahudumia wananchi wengi kwa haraka sana.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angellah Kairuki, akipata maelezo kutoka kwa mmoja wa viongozi waandamizi wa Kiwanda ya Kioo Ltd kuhusu uzalishaji unaofanywa na kampuni hiyo, wakati wa ziara yake ya kutembelea kiwanda hicho aliyoifanya juzi, jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mkongo wa Taifa waleta neema kwa vijana

**Na Mwandishi Wetu, ZANZIBAR**

KUIMARIKA kwa huduma za Mkongo wa Mawasiliano wa Taifa (ICT backbone) kumeleta neema kubwa kwa vijana kujiajiri zaidi katika sekta ya habari na mawasiliano visiwani hapa kwa kuchagiza shughuli za maendeleo ya uchumi.

Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Dk. Mzee Suleiman Mndewa, aliwaambia waandishi wa habari kuwa kupitia Tehama vijana wameweza kupata maarifa na kufanya biashara zao ndani na nje ya Zanzibar.

"Kupitia ushirikiano wetu na kampuni kubwa ya Kichina ya mawasiliano ya ZTE Corporation tumeweza kujifunza na kupata teknolojia ya hali ya juu katika suala zima la Tehama," alisema Dk. Mndewa.

Alisema siku za mwanzoni neno mkongo wa mawasiliano wa taifa ulikuwa msamiati mpya sana, lakini kutoka na ushirikiano kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Kampuni ya Mawasiliano ya ZTE, vijana wengi wameweza kunufaika kupitia mashirikiano hayo na kuwa vinara katika ya Tehama.

Akizungumza na waandishi wa habari waliotoka Tanzania Bara kwenda kujifunza jinsi Zanzibar ilivyopiga hatua katika matumizi ya Tehama na kuwa kichocheo kikubwa katika sekta za mbalimbali za uchumi visiwani hapo, Dk. Mndewa alisema mkongo wa mawasiliano wa taifa umekuwa muhimili mkubwa katika kufanikisha mageuzi ya kiuchumi na kijamii.

Alisema jumla ya vijana 18 wa Zanzibar wamapata mafunzo ya hali juu namna ya kuzambaza teknolojia ya mkongo wa mawasiliano wa taifa, huku wakiwa kazini kupitia Chuo Kikuu cha ZTE cha China.

"Awamu ya kwanza ya mradi ilianza mwaka 2012 na sasa hivi tunaongelea mwaka wa sita. Kampuni ya ZTE imekuwa ikitekeleza uwekaji na mtandao na kuhakikisha upatikanaji wake," alisena na kuongeza kuwa wamekuwa wadau muhimu sana katika sekta ya Tehama.

Alisema Tehama haiwezi kupanuka kama kuna miundombinu tu bila ya kuwapo kwa uhamasishaji kama nyenzo kuu ya kuchochea ukuaji wa sekta nyingine mbalimbali za kiuchumi na kijamii.

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatoa elimu kwa wananchi kupitia vituo vya kijamii kuwa Tehama ni daraja muhimu sana kati ya watu wa vijijini na mjini," alisema Dk. Mndewa ambaye ni mbobezi katika masuala ya Tehama.

Alisema serikali imeshajenga kituo katika hatua ya jumuiya na vituo hivyo vimewekwa kompyuta ambazo zinatumika kuwafundishia masuala ya Tehama katika wilaya mbalimbali visiwani humo.

UCSAF imejenga vituo hivyo kama sehemu ya kupunguza (gap) utofauti wa uelewa wa Tehama kati ya watu wa vijijini na mjini.

# Google, Microsoft kushtakiwa vifo DRC

**KINSHASA,** Congo

KAMPUNI za teknolojia ya mitandao Apple, Google, Tesla na Microsoft zimetajwa katika kesi ya madai ya fidia kwa kusababisha vifo na majeraha ya wachimbaji watoto katika migodi nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, DRC.

Kesi hii ilifunguliwa na mawakili wa kimataifa wa haki za binadamu kwa niaba ya familia 14 kutoka nchini humo.

Kampuni hizo zinashutumu kwa kununua madini aina ya kobalti yanayotumiwa katika bidhaa zao, huku wakijua yanatokana na ukiukwaji wa sheria kwa kuwaruhusu watoto wadogo kuchimba.

**DRC inazalisha asilimia 60 ya kobalti inayosambazwa duniani kote.**

DRC inazalisha asilimia 60 ya kobalti inayosambazwa duniani kote.

Madini hayo yanatumiwa kutengenezea betri aina ya lithium-ion zinazotumika kuwasha magari ya umeme, kompyuta mpakato na simu janja.

Lakini, hatua za uchimbaji zimekuwa zikizua wasiwasi kuhusu uchimbaji haramu na ukiukwaji wa haki za binadamu na ufisadi.

Kesi hii iliyofunguliwa nchini Marekani inadai kuwa kampuni hizo za teknolojia zilikuwa na uelewa wa kutosha kuwa kobalti inayotumika katika bidhaa zao inaweza kuhusishwa na kufanyishwa kazi kwa watoto kinyume cha sheria.

Wanasema wameshindwa kudhibiti mifumo ya usambazaji wa bidhaa zao na badala yake kufaidika kutoka kwa utumikishwaji wa watoto hao.

Kampuni zingine zilizotajwa katika kesi hiyo ni pamoja na Dell na kampuni mbili za uchimba madini za Zheijang Huayou Cobalt na Glencore, ambao wanamiliki migodi ambayo kwa mujibu wa familia za waathirika wanasema ndipo watoto hao walipokuwa wanafanyia kazi.

Glencore iliiambia gazeti la Telegraph la Uingereza kuwa hainunui, kusindika wala kufanya biashara yoyote ya madini yaliyochimbwa na wachimbaji wadogo. **BBC**

# China, Misri, Saudia vinara vifungo vya waandishi

**BERLIN,** Ujerumani

NCHI za China, Misri na Saudia Arabia zinaongoza kwa kukandamiza vyombo vya habari kwa kuwaweka gerezani waandishi wanaoonekana kukosoa serikali.

Kulingana na shirika la waandishi wa habari wasio na mipaka RSF, takribani nusu ya waandishi wa habari 400 waliofungwa duniani kote wapo katika mataifa hayo matatu.

Akizungumza kabla ya kuchapisha ripoti ya kila mwaka ya shirika hilo kuhusu uhuru wa habari mjini Berlin, msemaji wa Bodi ya RSF, Michael Rediske, ameeleza kuwa, serikali za mataifa hayo zimeongeza mbinyo kwa watu wanaofanya kazi katika vyombo vya habari.

China pekee imeripotiwa ina wanataaluma wa habari 120 waliofungwa gerezani. Zaidi ya asilimia 40 ni waandishi wa habari raia wa taifa hilo, ambao pamoja na kuwepo kwa udhibiti mkali, wamejaribu kusambazia habari kupitia mitandao ya kijamii.

Idadi ya waandishi wa habari 49 na wataalamu wengine katika tasnia hiyo wameuawa ulimwenguni tangu mwaka huu uanze. **DW**



Msemaji wa Bodi ya RSF, Michael Rediske



Mwandamanaji akikimbia mbele ya gari linalowaka moto katika maandamano ya kupinga sheria mpya jijini Delhi, India. **PICHA: REUTERS**

# Boeing kusimamisha uzalishaji 737 Max

**WASHINGTON,** Marekani

KAMPUNI ya Boeing mwezi ujao itasimamisha kwa muda uzalishaji wa ndege zake zilizokumbwa na matatizo za 737 Max.

Utengenezaji wa ndege hizo ulikuwa ukiendelea licha ya ndege za chapa hiyo kuzuiwa kupaa kwa miezi tisa baada ya kuhusika katika ajali mbili zilizosababisha vifo vya mamia ya watu.

Zaidi ya watu 300 walipoteza maisha wakati ndege mbili za 737 Max zilipoanguka katika nchi za Indonesia na Ethiopia baada ya kuripoti matatizo katika mfumo wake mpya.

Boeing imekua ikitumaini kuwa ndege hizo zitarejea tena angani kufikia mwishoni mwa mwaka huu.

Hata hivyo wasimamizi wa safari za anga nchini Marekani wamesema wazi kuwa ndege hizo hazitapewa kibali cha kurejea angani katika siku za hivi karibuni.

Kampuni ya Boeing, yenye makao yake Seattle, Washington ni moja ya wauzaji wakubwa zaidi wa ndege duniani.

Kampuni hiyo imesema katika taarifa yake kwamba haitawafuta kazi wafanyakazi wanaofanya kazi na 737 Max, lakini kusimamishwa kwa utengenezaji wake kunaweza kuwaathiri wasambazaji na uchumi kwa ujumla.

"Kurejea kwa huduma salama za safari za 737 Max ni kipaumbele chetu cha juu," ilisema kampuni hiyo, "Tunafahamu mchakato wa huduma za 737 Max, masharti ya mafunzo yanayohitajika, lazima yatekelezwe kwa usahihi, kuhakikisha wasimamizi wetu, wateja na umma unaosafiri wana imani na 737 Max."

Wiki iliyopita kikao cha Bunge la Wawakilishi la Marekani kiliambiwa kuwa wasimamizi wa safari za anga nchini Marekani walikua wanafahamu kuwa baada ya ajali ya kwanza kutokea nchini Indonesia Oktoka 2018 kulikuwa na hatari ya kutokea kwa ajali nyingine zaidi. **BBC**

# Mkutano wa wakimbizi waanza nchini Uswisi

**GENEVA,** Uswisi

MKUTANO wa kimataifa wa kilele kuhusu wakimbizi umefunguliwa jana mjini Geneva, Uswisi.

Katika mkutano huo wito umetolewa kuchukuliwa hatua thabiti ili kusaidia idadi kubwa ya watu waliokosa makazi, na mataifa tajiri kutimiza majukumu yao. Mkutano huo unafanyika ikiwa imetimia mwaka mmoja tangu mkutano mkuu wa Umoja wa Mataifa, ulipopitisha mfumo unaolenga kuunda njia bora ya kuwasaidia wakimbizi na nchi zinazowahifadhi.

Dominique Hyde mkurugenzi wa kitengo cha mahusiano ya nje, ofisi ya Umoja wa Mataifa kuhusu wakimbizi amesema watu hukimbia kwa sababu tofauti ikiwamo vita na mizozo.

Hadi kufikia mwishoni mwa mwaka jana karibu watu milioni 71 hawakuwa na makazi kutokana na vita, machafuko na mateso, ikiwamo watu milioni 26 waliovuka mipaka kama wakimbizi. **DW**

# Maofisa ugani wapewa mwongozo wa huduma

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SERIKALI imekiagiza Chama cha Wagani Tanzania (TSAEE) kutumika kama chombo cha kuishauri serikali katika kuboresha utoaji wa huduma za ugani nchini pamoja na kuwa ni kiungo cha kuwaunganisha watoa huduma za ugani na wadau mbalimbali.

Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, ndiye aliyetoa agizo hilo jijini hapa wakati wa Mkutano Mkuu wa mwaka wa TSAEE.

Alikitaka chama hicho kusimamia weledi wa maofisa ugani katika kutekeleza majukumu yao. Aidha ili kuimarisha uhai wa chama, aliwataka wajumbe kukutana mara kwa mara ili kujadili mafanikio na changamoto zinazokabili utoaji wa huduma za ugani nchini, na kutoa ushauri kwa Serikali namna ya kutatua changamoto hizo.

Pia, aliwataka wajumbe, kwa kushirikiana na viongozi wa chama hicho kuongeza ubunifu katika kutafuta vyanzo vya mapato kwa ajili ya kuimarisha na kuendesha chama, huku akiwasisitiza kuwa wakati wa uchaguzi wahakikishe wanachagua viongozi makini watakaosimamia na kuongoza chama hicho ili kiwe imara na endelevu.

Kwa upande wa maofisa ugani kuimarisha utendaji wa majukumu yao ya kila siku na kuinua sekta ya kilimo nchini, Waziri Hasunga aliagiza kila ofisa kuwa na daftari la kilimo ambalo atalitumia kuweka kumbukumbu zote za muhimu kila atakapoenda kuwahudumia wakulima.

Alisema pamoja na taarifa nyingine za msingi, daftari hilo lionyeshe orodha ya wakulima anaowahudumia, ukubwa wa mashamba yao na aina ya mazao wanayolima.

Ameongeza kuwa ofisa ugani ni lazima awe na mpango kazi utakaoonyesha ni nini hasa amepanga kufanya kwa wakulima, ikiwamo kuainisha ratiba ya kazi kwa kipindi husika, huku akitaka kila ofisa kuwa na mashamba ya mfano au mashamba darasa ambayo atayatumia kuwafundishia wakulima katika kata/kijiji/mtaa wake.

Kadhalika, aliagiza kuwa ofisa ugani ni lazima awe na mwongozo wa kusimamia huduma za ugani na kuhakikisha anausimamia ipasavyo pamoja na kufahamu kanuni au mbinu bora za kilimo cha mazao makuu yote yanayolimwa katika eneo lake.



Meya wa Kinondoni, Benjamin Sitta (kulia), Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Bima ya Jubilee Insurance, Dipankar Acharya (katikati) pamoja na wafanyakazi wa kampuni hiyo wakifanya usafi wa mazingira ya soko la Makumbusho pamoja kituo cha daladala, Dar es Salaam jana, ikiwa ni sehemu ya majukumu yao ya kuisaidia jamii. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Mfanyakazi wa CRDB kortini uhujumu uchumi

**Na Hellen Mwango**

MFANYAKAZI wa Benki ya CRDB, Joseph Ndulu, amefikishwa mahakamani akikabiliwa na tuhuma za uhujumu uchumi ikiwamo, kuisababishia Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), hasara ya zaidi ya Sh. bilioni 5.119 pamoja na utakatishaji fedha hizo.

Mshtakiwa huyo amefanya idadi ya washtakiwa katika katika kesi hiyo kufikia saba baada ya kuunganishwa na wenzake sita.

Jana Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi ilisikiliza mashtaka dhidi ya Ndulu.

Mbali na Ndulu, washtakiwa wengine ni watumishi wa TPA Valentine Sangawe (40) mhasibu, Leticia Massaro (33) karani, Christina Temu (37), wafanyakazi wa benki ya CRDB, Eva Vicent (33) na Lenfrida Magawa (31).

Wakili wa serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kati ya Julai mwaka 2014 hadi Aprili 2015, akiwa na wenzake waliiba, kutakatisha na kuisababishià TPA hasara ya Sh. 5,119,839,758.28.

Ilidaiwa kati ya Oktoba mwaka 2014 hadi Novemba mosi mwaka huo, katika bandari kavu ya TRH jijini Dar es Salaam, aliiba Sh. 39,992,243 mali ya TPA. Pia mshtakiwa huyo anadaiwa kuiba Dola za Marekani 17,993.26 mali ya Mamlaka hiyo.

Katika shtaka lingine, mshtakiwa anadaiwa kati ya Oktoba 30 hadi Novemba mosi mwaka 2014, alighushi hati ya malipo yenye thamani ya Sh.39, 992,143 kwa manufaa ya kampuni ya Smart Clearing & Fowarding ,akionesha ni halali imetolewa katika mfumo wa malipo wa TPA wakati akijua si kweli.

Mshtakiwa huyo hakutakiwa kujibu chochote kwakuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo.

Upande wa Jamhuri ulidai upélelezi haujakamilika na kuomba tarehe nyingine ya kutajwa shauri hilo ambayo ilipangwa Desemba 30, mwaka huu.

# Wakala wa vipimo wajivunia mafanikio miaka 4 ya JPM

**Na Juster Prudence**

WAKALA wa vipimo (WMA) umeainisha mafanikio iliyoyapata katika miaka minne ya serikali ya awamu ya tano, ikiwa ni pamoja na kutoa gawio la Sh. milioni 12.539 kwa serikali.

Dk. Ludovic Manege, Ofisa Mtendaji Mkuu wa wakala huo, alisema jijini Dar es Salaam jana kuwa katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Rais John Magufuli, wakala umefanya mambo mengi mazuri ikiwa ni pamoja na kutoa gawio hilo kwa serikali kupitia kwa Msajili wa Hazina.

Kwenye sekta ya maji, Dk. Manege alisema serikali ya awamu ya tano katika kuhakikisha wananchi wanatumia maji na kulipia gharama sahihi kulingana na matumizi yao, iliupatia wakala Sh. milioni 500 zilizosaidia ununuzi wa kifaa cha kisasa (water meter test bench) cha kuhakikia dira za maji kabla hazijafungwa kwa wateja ili wananchi wapate thamani ya fedha zao kupitia huduma ya maji.

"Mpaka sasa tumehakiki jumla ya dira za maji 700,000. Kati yake, zilizopitishwa ni 570,000 na zilizokataliwa kutokana na kuwa na matatizo mbalimbali ni 130,000," alisema.

Kwenye sekta ya madini, alisema serikali imeanzisha utaratibu mzuri wa kuwa na masoko ya kuuza na kununulia vito na madini katika mikoa yote.

Alisema kwa kutambua umuhimu wa biashara hiyo katika kukuza uchumi wa nchi, serikali iliupatia wakala Sh. milioni 500 kwa ajili ya kununua vigezi vya kisasa gredi ya pili vinavyotumika kuhakiki mizani inayotumika kuuza na kununulia madini, hivyo serikali kutoza kodi kupitia mizani iliyohakikiwa na wakala na kupata mapato yanayostahili.

### MALORI YA MAFUTA

Dk. Manege alisema wakala pia umefanikiwa kukamilisha ujenzi wa kituo kikubwa na cha kisasa cha Misugusugu kilichoko mkoani Pwani kinachotumika kuhakiki ujazo wa malori yanayosafirisha mafuta.

Alisema kituo hicho kipya kinao uwezo wa kupima malori zaidi ya 60 kwa siku ikilinganishwa na kituo kilichokuwa kinatumika awali cha Dar es Salaam kilichokuwa kinapima malori manane kwa siku.

"Mpaka sasa, kituo cha upimaji cha Misugusugu kwa mwezi kinapima malori 400 na kuingiza kiasi cha Sh. milioni 300 kwa kila mwezi.

"Ujenzi wa kituo hiki umesaidia sana kupunguza msongamano wa malori ya mafuta ambapo tunahudumia na nchi za jirani kama vile Rwanda, Burundi, Congo na Zambia," alisema.

Sekta ya Kilimo

Kwenye sekta ya kilimo, Dk. Manege alisema wakala umefanikiwa kwa kiasi kikubwa kusimamia matumizi ya vipimo sahihi katika ununuzi wa mazao makuu ya kimkakati kama vile pamba, korosho, kahawa na ufuta.

Alisema mpaka sasa kesi 33 za wachezea mizani za kununulia mazao ya wakulima, zimeendeshwa na baadhi ya washtakiwa waliokutwa na hatia walilipa faini na wengine walihukumiwa kifungo na mizani zao kutaifishwa.

Aliongeza kuwa wakala pia umeongeza vitendea kazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na magari, akibainisha kuwa katika kipindi hicho cha miaka minne, umenunua magari 30 ambayo yamesambazwa katika mikoa mbalimbali kwa ajili ya kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi wa mjini na vijijini.

"Hii imesaidia kuongezeka kwa vipimo mbalimbali vilivyokaguliwa kutoka 660,000 kwa mwaka wa fedha 2016/2017 hadi vipimo 760,000 kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

"Wakala wa Vipimo unatoa shukrani za kipekee kwa serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Magufuli kwa kuendelea kutuamini na kutuwezesha katika kuhakikisha tunatimiza lengo lake kuu la kumlinda mlaji kupitia matumizi ya vipimo sahihi," alisifu.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KAZI /AJIRA

**Nafasi za kazi** ualimu masomo ya sst/diploma 0656490706/0784142792

## VIWANJA/MASHAMBA

**SHAMBA LINAUZWA,** SHAMBA EKA 40 MOROGORO. Linafaa kufuga na kilimo, limeshavunwa misimu 3, lina nyumba vyumba 2 na Gari inafika. Bei ml.25 zenye mjadala. Wasiliana 0718965491 078653304 0629478005.


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,

au piga simu: 0782253676


**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA

### TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **Alhamisi tarehe 19/12/2019** kampuni ya **ESTIM CONSTRUCTION COMPANY LTD** inatarajia kusafirisha mashine (Excavator) kutoka **DAR ES SALAAM** kuelekea **LUGOBA** kutumia barabara ya M**OROGORO, CHALINZE SEGERA kupitia VIGWAZA.** Gari hilo lenye namba za usajili: **T 235 CHW/ T 106 AYZ**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **20** |
| **Upana** | - | **mita** | **3.00** |
| **Kimo** | - | **mita** | **4.8** |

3. Njia itakayotumika: **MOROGORO, CHALINZE SEGERA, kupitia VIGWAZA hadi LUGOBA.** Gari zitasafiri muda wa mchana tu **(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)**

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

115559302

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI NA FILE LAKE**

**HASSAN RAMADHANI MSEMO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 852 DRF TOYOTA PREMIO**. Eneo ilikopotelea ni TUMBI KIBAHA. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **KBA/RB/8571/2019.**

115559802

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**Mahakama ya mwanzo DODOMA MJINI**
**wilaya ya DODOMA**
**MADAI NAMBARI 69/2019**
**MDAI PENDO DOMINICK MUSHI**
**MDAIWA ANDREW ANTHON MWAKATUNDU**

Kwa ANDREW ANTHON MWAKATUNDU
MPWAPWA - LUMUMA

Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba

TALAKA, KUGAWANA MALI NA MATUNZO YA WATOTO

Hivyo unahitajika kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya tarehe 24/12/2019 saa 2.30 asubuhi kwa kujibu madai, na kwa kuwa siku hiyo ya kuitwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

Na kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama tathibitisha kama umepokea kuitwa shaurini, hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa Amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 10/12/2019

115559402


Uza, Chenye Thamani

Kubwa Kwa

Kutangaza Nasi

Kwa Bei Poa

Tupigie 0782253676

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Tupigie 0782253676

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Tupigie 0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII


**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# NEUER, MULLER WAPANIA KULIPA KISASI CHELSEA UEFA

**MUNICH,** Ujerumani

MANUEL Neuer na Thomas Muller wanafikiri Bayern Munich inatakiwa kujiamini kuifunga Chelsea kwenye hatua ya mtoano wa timu 16-bora katika Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mabingwa hao wa Bundesliga watakutana na kikosi cha Frank Lampard ikiwa ni marudio ya fainali ya mwaka 2011-12, wakati Chelsea ikishinda kwa penalti baada ya sare ya bao 1-1 mjini Munich.

Neuer na Muller walikuwa katikati ya mafanikio ya Bayern, ambao walishinda taji hilo msimu wa 2012-13 kwa kuifunga Borussia Dortmund kwenye fainali iliyopigwa pale katika dimba la Wembley.

Huku Bayern ikiwa imerudi katika ubora wake tangu Hansi Flick achukue nafasi ya ukocha wa muda kutoka kwa Niko Kovac, hasa kwa mechi za Ulaya, Neuer anafikiri timu yake inaweza kuifunga Chelsea.

"Tunasubiria kwenda jijini London, ambako tuna uzoefu nako," alisema golikipa huyo akinukuliwa na tovuti ya klabu hiyo.

"Ni timu hatari, ambayo tunatakiwa kuwachukuliwa kwa umakini mkubwa. "Kwa uhakika tunataka kufuzu kwa raundi inayofuata. Nafikiri tunaweza kwenda kwenye mchezo huo tukiwa na afya ya kujiamini. Tuna furaha na droo: ni dhidi ya timu inayovutia na nzuri."

Muller alisema fainali ya mwaka 2012 "haina umuhimu" kwenye mchezo huo wa hatua ya mtoano wa timu 16, akiongeza:

"Ni wazi kwamba huwezi kupata timu ndogo kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16 bora. Kwa uhakika tunajiamini. Najisikia vizuri kuhusu droo hii.

"Chelsea ina wachezaji ambao wanaweza kutudhuru. Wana wachezaji wanaoweza kushambulia na wenye ubora wa hali ya juu.

"Lakini ni suala la kiwango cha mtu, si mchezaji mmoja mmoja. Hisia zangu kwa sasa ni furaha yangu juu ya timu nzuri tuliyonayo kwa sasa. Tunataka kuwa na nafasi kubwa."

# Valverde aihofia Napoli 16-bora

**BARCELONA,** Hispania

KOCHA wa Barcelona, Ernesto Valverde amesisitiza Napoli watakuwa wapinzani hatari kwenye hatua ya 16-bora katika Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Miamba hao wa Catalunya wamepangiwa kucheza na vijana hao kutoka kule Serie A katika droo iliyopangwa Jumatatu mjini Nyon, huku mchezo wa kwanza ukicheza kule kwenye dimba la San Paolo, Februari 25.

Napoli imekuwa na wakati mgumu msimu huu kwenye ligi ya nyumbani, wakipoteza 2-1 nyumbani dhidi ya Parma Jumamosi na kubaki wakiwa nafasi ya nane kwenye msimamo, wakipitwa pointi 18 na vinara wa ligi hiyo, Inter Milan na Juventus.

Licha ya kuwa na matokeo mabaya kwa ligi ya nyumbani, ambapo ilisababisha Carlo Ancelotti kutimuliwa na nafasi yake kuchukuliwa na Gennaro Gattuso, Napoli walimaliza hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya bila kufungwa kwenye Kundi E na ndio timu pekee iliyowafunga mabingwa watetezi, Liverpool kwenye mashindano hayo msimu huu.

Valverde anaamini Barca watahitaji kuwa kwenye makali yao kama watataka kufuzu robo fainali, ingawa timu yake iliibuka na ushindi wa mabao 4-0 zilipokutana kwenye maandalizi ya msimu mpya.

"Napoli ni timu hatari," alisema akiiambia televisheni ya Barca. "Kwa uhakika kabisa hawapo kwenye ubora wao kwa wakati huu. Wamebadilisha kocha na wanahitaji kurudi kweye ubora wao."





# Mikel Arteta, Arsenal wafikia patamu

**LONDON,** England

ARSENAL wapo kwenye mazungumzo na Manchester City juu ya uwezekano wa kumchukua kocha, Mikel Arteta.

Haijulikani kama Arteta mwenye umri wa miaka 37, amepewa ofa ya kuchukua mikoba ya Unai Emery, ambaye alifukuzwa Novemba.

Ofisa Mtendaji wa 'Washika Bunduki' hao, Vinai Venkatesham alipigwa picha akiwa nyumbani kwa raia huyo wa Hispania baada ya kichapo cha mabao 3-0 kutoka kwa Man City kwenye Uwanja wa Emirates Jumapili.

Kocha wa City, Pep Guardiola amesema hatamzuia Arteta kuondoka kama akiamua kufanya hivyo.

Inafahamika kwamba, Arteta ameiambia City kwamba ilikuwa ni mara ya pili kwake yeye kufanya majadiliano na klabu yake hiyo ya zamani na amekutana mara tatu na Josh Kroenke, mtoto wa mmiliki wa klabu hiyo, Stan.

Hata hivyo, Everton, walitajwa kumuwania Arteta baada ya kumfukuza Marco Silva Desemba 6, mwaka huu, ambaye alicheza mechi 209 pale Goodison Park kati ya mwaka 2005 na 2011.

Baada ya Arsenal kupata kichapo Jumapili, kocha wa muda, Freddie Ljungberg - ambaye ameshinda mechi moja kati ya tano tangu apewe jukumu hilo Novemba 29 ameitaka klabu hiyo kufanya uamuzi ya haraka kumteua kocha mpya.

Arsenal ipo nafasi ya tisa kwenye msimamo wa ligi, ikipitwa pointi saba na Chelsea iliyopo nafasi ya nne, baada ya kushinda mechi tano kati ya 17 msimu huu.

Arteta kiungo wa zamani wa Arsenal ambaye alicheza mechi 149 kati ya mwaka 2011 na 2016, alihusishwa kuchukua mikoba ya Arsene Wenger pale Emirates mwaka 2018 kabla ya kuteuliwa kwa Emery."

# Maradona ampeleka Pochettino Boca Juniors

**BUENOS AIRES,** Argentina

DIEGO Maradona anataka kocha wa zamani wa Tottenham, Mauricio Pochettino kuchukua mikoba ya kuinoa "timu kubwa duniani" Boca Juniors.

Pochettino amekuwa akihusishwa na mpango wa kutakiwa na Manchester United, Arsenal na Bayern Munich tangu alipofukuzwa kuwa kocha wa Tottenham mwezi uliopita.

Maradona ambaye ni kocha wa klabu ya Gimnasia y Esgrima La Plata inayoshiriki Ligi Kuu ya Argentina, Superliga, amemtaka Pochettino kurudi nyumbani na kuiongoza Boca, ambayo inatafuta kocha mpya baada ya kujiuzulu kwa Gustavo Alfaro.

Baada ya gwiji wa Boca na Argentina, Juan Roman Riquelme kurudi katika klabu hiyo kama makamu wa rais baada ya uchaguzi wa Desemba, Maradona aliulizwa kama atarudi kwa miamba hao baada ya misimu miwili.

"Sitakwenda Boca... kwa sababu narudia sikubaliani na wale wote watakaoingoza klabu," alisema Maradona akiiambia Ole.

"Rais (Jorge Amor Ameal) tayari alikuwa pale na yalikuwa majanga, amezungukwa na (makamu wa rais Mario Pergolini) ambaye anaamini kwamba anaweza kuiongoza klabu.

"Na Roman... hawezi kufanya lolote. Ni ngumu zaidi kuliko kuuzuia mpira, kutoa pasi au kupiga mpira wa adhabu ndogo.

"Boca inatakiwa kurudi kwenye ufundi na kucheza kama Boca iliyozoeleka. Si rahisi kukaa tu kwenye kiti.

"Lakini sasa sitakwenda, kuna wakati huwa inatokea. Lakini ningependa Mauricio Pochettino. Unatakiwa kumuita na kumshawishi kuiongoza timu kubwa duniani."

Maradona aliongeza: "Nataka kumaliza kwa staili bora. Kwanza nataka kuiokoa Gymnasia (kutoshuka daraja), halafu tutaangalia."

Boca ipo nafasi ya pili kwenye Superliga, ikipitwa pointi moja na Argentinos Juniors, huku Gimnasia ikiwa nafasi ya 21 katika msimamo wa timu 24.





# KLOPP: SIMEONE HANA FURAHA KUIVAA LIVERPOOL

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp anatambua kwamba, Liverpool inakabiliwa na mchezo mgumu dhidi ya Atletico Madrid kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya mtoano ya 16-bora, lakini amemnyooshea kidole mpinzani wake, Diego Simeone kwamba atakuwa hana furaha kukabiliana na bingwa mtetezi.

Liverpool ilimaliza ikiwa kinara wa kundi lake dhidi ya Napoli na sasa watakwenda pale kwenye Uwanja wa Wanda Metropolitano - sehemu ambayo msimu uliopita walicheza fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na sasa watakwenda kuwavaa miamba wa La Liga, Atleti.

Klopp amebainisha kwamba alitarajia kurudi Madrid, huku akitambua kwamba mchezo huo utakuwa mgumu.

"Ni droo inayovutia," alisema Klopp akiiambia tovuti ya klabu yake. "Kabla ya droo hii, kwa uhakika nilifikiria inaweza kuwa Madrid.

"Madrid ni sehemu ambayo tunakumbukumbu za kuvutia, kwa sisi wote, hivyo ni jambo kubwa, lakini safari hii tutacheza na Atletico pale na ndio uwanja wao wa nyumbani.

"Ni mchezo mgumu kwa kweli, lakini kama umepita kwenye droo zote, unaona kabisa kama fainali nne au tano zipo tayari kwenye hatua ya 16.

"Hivyo, kwa uhakika kabisa ni nzuri; droo nzuri ni mchezo mgumu kama ambavyo unatarajiwa, lakini sifikirii kama Bw. Simeone atakuwa na furaha na droo hii ya kucheza na Liverpool.

"Utakuwa mchezo mgumu. Timu mbili zinazocheza soka gumu. Staili tofauti na mfumo tofauti kabisa, lakini zote zipo tayari kwa ajili ya mchezo huu."

# Everton kumtangaza Ancelotti kocha wao

**LIVERPOOL,** England

CARLO Ancelotti anatarajiwa kuthibitishwa kuwa kocha mpya wa Everton kati ya Alhamisi au Ijumaa.

Muitaliano huyo mchezo wake wa kwanza utakuwa dhidi ya Arsenal, ambako pia alikuwa akihusishwa, kwenye dimba la Goodison Park Jumamosi, huku wao wakiwa na uwezekano wa kuwa chini ya bosi mpya, Mikel Arteta.

Ancelotti mwenye umri wa miaka 60, amefikia makubaliano ya kuchukua mikoba ya Marco Silva Jumatatu wiki hii baada ya mazungumzo yao pale Merseyside.

Kocha wa muda, Duncan Ferguson, ambaye alipata ushindi dhidi ya Chelsea na sare dhidi ya Manchester United, ataiongoza timu kwenye mchezo wa robo fainali ya Kombe la Carabao leo Jumatano dhidi ya Leicester.

Pengine inaweza kutangazwa mapema Ancelotti kuchukua mikoba hiyo pale Toffees kabla hata vijana hao wa Brendan Rodgers hawajatua pale Goodison.

Ancelotti alianza mazungumzo na mwenye hisa nyingi pale Everton, Farhad Moshiri na mwenyekiti wake, Bill Kenwright baada ya kufukuzwa kama kocha wa Napoli wiki iliyopita.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# NEYMAR AZIKATAA RASMI BARCA, REAL

## Kuondoka? Bado nina miaka miwili katika mkataba wangu, kipaumbele changu ni PSG...

**PARIS,** Ufaransa

NEYMAR anaonekana kuwa na furaha kuendelea kubaki Paris Saint-Germain, ikiwa ni miezi michache baada ya kujaribu kulazimisha kuondoka kwa mabingwa hao wa Ligue 1.

Nyota huyo wa kimataifa wa Brazil alihusishwa sana na kurudi Hispania katika dirisha la hivi karibuni, lakini dili hilo la kurudi tena Barcelona ama kujiunga na Real Madrid lilishindwa kukamilika.

Licha ya kukiri alitaka kuondoka na kuwa akizomewa na mashabiki wa PSG baada ya kurejea katika mechi dhidi ya Strasbourg akitokea kuuguza majeraha Septemba, Neymar ameonyesha kiwango kizuri katika kikosi hicho cha Thomas Tuchel msimu huu wa 2019-20, akifunga mabao tisa na kutoa pasi za mwisho tano katika mechi 11 alizocheza kwenye mashindano yote.

Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 27, sasa amependekeza hana sababu yoyote ya kujaribu kusuka mpango wa kuondoka katika dimba la Parc des Princes, ambapo alitua kwa ada iliyoweka rekodi ya dunia kiasi cha euro milioni 222 miaka miwili iliyopita.

"Kwa nini ningetaka kuondoka? Bado nina miaka miwili katika mkataba wangu, timu inaendelea kupata maendeleo," aliliambia Jarida la France Football.

"Lazima tuendelee kuzingatia msimu huu kufanya mambo vizuri na kushinda mataji mengi iwezekanavyo.

"Msimu huu, lengo ni Ligi ya Mabingwa. Na kipaumbele changu ni PSG, kwa jitihada kubwa kila wiki. Lengo mara zote ni kushinda mechi ijayo."

Wakati mara nyingine akituhumiwa kwa ubinafsi uwanjani, Neymar alisisitiza watu wachache wanaojua ubinadamu wake na anashangaa hayupo katika mchezo kwa sifa binafsi.

"Sichezi kuwa namba moja. Ninacheza tu kwa sababu ninapenda soka. Ninajisikia tu furaha wakati ninacheza. Na kila wakati nipo uwanjani, ninajitoa kwa asilimia 100," alisema.

"Je! Unadhani ukamilifu upo? Ni Mungu tu aliye kamili. Kila mtu ana makosa yake madogo. Kiongozi ni mtu ambaye lazima aisaidie timu kushinda, kuwaongoza kushinda. Wanaweza kuwa nahodha, au mfungaji mabao. Kila mtu ana njia yake ya kuwa kiongozi, na wana uwezo wao wenyewe."

"Ni watu wachache wanaomjua Neymar halisi. Wazazi wangu na marafiki zangu tu. Kile watu wanachokiona ni kitu tofauti kabisa. Na mwishoni, hawaoni mengi!"

## ZISIKUPITE

### YAONYWA KWA ARTETA

MANCHESTER City wanatibuana na Arsenal kutokana na miamba hiyo ya London kujaribu kumshawishi kocha wao msaidizi, Mikel Arteta na wamewaeleza 'Gunners' itawagharimu jumla ya tarakimu saba ili kuweza kumpata. ***(Mirror)***

### IBRA ASUBIRISHWA NAPOLI

MMILIKI wa Napoli, Aurelio de Laurentiis amesema ana "vipaumbele vingine" kuliko kumsajili straika Msweden Zlatan Ibrahimovic, 38, ambaye ni mchezaji huru. ***(Mirror)***

### CAMAVINGA AIVUTIA MADRID

REAL Madrid inavutiwa kumsajili straika Mfaransa mzaliwa wa Angola, Eduardo Camavinga kutoka Rennes. ***(L'Equipe - in French)***

### KROENKE, ARTETA KUTETA J3

MIKEL Arteta atakutana na Mkurugenzi wa Arsenal, Josh Kroenke Jumatatu usiku kwa mara ya tatu na mahojiano ya mwisho wakati huu akikaribia kupewa jukumu la kuinoa klabu hiyo. ***(Mail)***

### CARLO, EVERTON WAKUBALIANA

KOCHA wa zamani wa Chelsea, AC Milan, Real Madrid na Napoli, Carlo Ancelotti amefikia makubaliano kikanuni ya kuwa kocha ajaye wa Everton. ***(Sky Sports)***

### YOUNG KUSEPA MAN UNITED

BEKI wa England, Ashley Young, 34, anatarajia kuondoka Manchester United majira ya joto na yupo tayari kuzungumza na klabu nyingine Januari. ***(ESPN)***

### KWA WERNER, DEMBELE

CHELSEA imewaongeza mshambuliaji wa RB Leipzig, Mjerumani Timo Werner na straika wa Lyon, Moussa Dembele, wote wakiwa na miaka miaka 23, katika orodha ya wachezaji inaotaka kuwasajili dirisha la Januari. ***(Mail)***

### EMERY AIKATALIA EVERTON

UNAI Emery amekataa nafasi ya kuinoa Everton kwa kuchukua nafasi ya Marco Silva aliyetimuliwa kwa sababu alidhani itakuwa ni mapema mno kuinoa klabu nyingine ya Ligi Kuu England kufuatia kutimuliwa pale Arsenal Novemba mwaka huu. ***(Marca)***

### KUJITOSA KWA MCCALLUM

LIVERPOOL inavutiwa kumsajili beki wa kushoto wa Coventry City, Sam McCallum, 19. ***(90min.com)***

### SPURS WAMTAKA TRAORE

WACHEZAJI wa kikosi cha kwanza cha Tottenham Hotspur, wamemshauri kocha Jose Mourinho kumsajili winga wa Wolves, Adama Traore baada ya mchezaji huyo raia wa Hispania mwenye umri wa miaka 23, kuonyesha kiwango cha kuvutia dhidi ya Molineux Jumapili. ***(Football Insider)***

### SANE AREJEA DIMBANI CITY

WINGA wa Manchester City, Mjerumani Leroy Sane, 23, amesema amerudi dimbani wakati akikaribia kupona majeraha ya goti aliyoyapata kwenye Ngao ya Jamii Agosti mwaka huu. ***(Manchester Evening News)***

# AISHA WA TANZANIA U-17 MFUNGAJI BORA CECAFA

**Na Somoe Ng'itu,** JINJA

WAKATI timu ya wasichana wa umri chini ya miaka 17 ya Tanzania Bara ikimaliza katika nafasi ya pili katika mashindano ya Kombe la Chalenji, mshambuliaji wake, Aisha Masaka ameibuka kuwa Mfungaji Bora wa michuano hiyo.

Wenyeji Uganda (She- Cranes) wameutwaa ubingwa huo baada ya kuichapa Kenya kwa mabao 2-0 jana kwenye michuano hiyo iliyochezwa kwa mtindo wa ligi, huku mchezaji wao Fauzia Najemba akitangazwa mchezaji bora wa mashindano.

Burundi ambayo jana ilimaliza michuano hiyo kwa kuichapa Eritrea 4-0, ilitangazwa kuwa timu yenye nidhamu katika mashindano hayo.

**Kwa upande wa Mtanzania Masaka, ametwaa tuzo ya mfungaji bora baada ya kufunga mabao 12, jana pekee akifunga saba katika ushindi wa mabao 10-0 walioupata dhidi ya vibonde Djibouti.**

Wasichana hao wa Tanzania Bara wamemaliza michuano hiyo wakiwa na pointi 11, baada ya kushinda mechi tatu na kutoka sare mara mbili katika mashindano hayo yaliyoshirikisha nchi sita na kuchezwa kwa mtindo wa ligi.

Tanzania Bara ilikwenda mapumziko ikiwa mbele kwa mabao 9-0, huku Djibouti wakionekana kuimarika zaidi katika kipindi cha pili cha mchezo huo uliochezeshwa na mwamuzi Darlene Nduwayo kutoka nchini Rwanda.

Mabao mengine ya Tanzania Bara katika mechi hiyo yalifungwa na Thadea Munga ambaye alifungua ukurasa pamoja na Lucia Mrema aliyefunga bao la 10 katika mchezo huo.

Mapema asubuhi, Burundi ilifanikiwa kupata ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Eritrea na kufikisha pointi saba.




Mshindi wa Shindano la Malkia wa Urembo na Mitindo duniani, kwa watu wenye ulemavu wa kusikia, Winifrida Brayson akiwa na tuzo zake. **PICHA: SABATO KASIKA**

## *Mrembo wa Dunia wasiosikia amuita Mo Dewji*

**Na Juster Prudence**

BAADA ya Mtanzania Winifrida Brayson kufanikiwa kuipeperusha vema bendera ya Tanzania kwa kutwaa taji la Urembo na Mitindo Dunia kwa watu wenye ulemavu wa kusikia, ametangaza dhamira yake ya kutaka kukutana na mfanyabiashara bilionea, Mohamed "Mo" Dewji ili kupata ushauri wake wa namna ya kuweza kufikia ndoto zake.

Winifrida ambaye alishinda tuzo hiyo katika mashindano hayo ya dunia yaliyofanyika nchini Urusi na kushirikisha jumla ya mataifa 57, ambapo Tanzania, Botswana na Uingereza zikiwa nchi zilizofanikiwa kutinga tatu bora kabla ya yeye kuibuka kidedea.

Mbali na kutangazwa kuwa malkia wa kinyang'anyiro hicho, pia Winifrida alizawadiwa tuzo nyingine kwa kushika nafasi ya 10 kwa upande wa mrembo mwenye mvuto katika picha.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, Winifrida alisema haikuwa rahisi kushinda mashindano hayo kutokana na warembo wote kuonyesha uwezo wa hali ya juu, lakini alijiamini na hakukata tamaa hadi alipotangazwa mshindi.

Alisema malengo yake kwa sasa ni kufungua taasisi itakayosaidi vijana wengine wenye hali kama yake(walemavu wa kusikia) ikiwa ni pamoja na kushawishi wadau mbalimbali ili waweze kujitolea katika kuwasaidia watu wote wenye mahitaji maalum.

"Natamani kukutana na Mo Dewji ambaye ni mfanyabiashara maarufu hapa nchini ili nimueleze juu ya mipango yangu ya kuanzisha taasisi ya kusaidia walemavu," Winifrida ambaye aliongozana na mtaalam wa kutafsiri alama za wasiosikia, alisema.

Aidha, aliishukuru Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mchango wake mkubwa waliompa hadi alipofika nchini Urusi kushiriki mashindano.

## Mcharo wa TPC kidedea Gofu Moro

**Na Mwandishi Wetu**

MASHINDANO ya wazi ya gofu Morogoro yamemalizika huku Ally Mcharo wa Klabu ya TPC akiibuka mshindi baada ya kupiga mikwaju 'Gross' 160 kwa siku zote mbili za michuano hiyo iliyofanyika katika Uwanja wa Gymkhana Morogoro.

Zacharia Edward wa Lugalo ambaye alipiga mikwaju 161 aliibuka mshindi wa pili huku upande wa mikwaju ya Jumla kwa Daraja A mshindi akiwa ni Michael Mtweve wa Mufindi aliyepiga mikwaju ya Jumla 155 akifuatiwa na Maurus Kajuna wa Lugalo.

Katika Daraja B, mshindi wa kwanza kwa mikwaju ya jumla ni Amadi Rajabu wa Gymkhana Dar es Salaam akifuatiwa na Teddy Kalinga wa Lugalo huku Daraja C mshindi akiwa ni Rory Mickllem wa Gymkhana Morogoro akifuatiwa na Musa Joseph wa Mufindi.

Kwa upande wa wanawake mshindi ni Vicky Elias wa Lugalo akifuatiwa na Joyce Warega naye wa Lugalo huku kwa upande wa watoto ambao ni wa Morogoro pekee walichuaana mshindi akiwa ni Robert Colnelius huku Rajabu Omary akishika nafasi ya pili na aliyepiga mpira mrefu ni Ally Mcharo na Hadija Selemani na waliopiga mpira jirani ni Zacharia Edward na Edna Chiwinga.

Akifunga mashindano hayo, mgeni rasmi ambaye pia ni Mwenyekiti wa Klabu ya Gofu ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, Brigedia Jenerali Michael Luwongo mstaafu, alizitaka klabu kuendeleza ushirikiano wa karibu.

## Mwadui kutangaza wapya, ikiiwinda KMC Ligi Kuu

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI uongozi ukiendelea kumulika huku na kule kuangazia wachezaji wa kuongeza nguvu kikosi chao, timu ya Mwadui imeendelea kujifua na kujipanga vilivyo kabla ya kuialika KMC FC hapo Desemba 30, mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe juzi, Katibu mkuu wa timu hiyo, Ramadhani Kilao, alisema kabla ya kumalizika kwa wiki hii, watatangaza nyota wapya watakaowasajili kwa ajili ya kuwaongezea nguvu ili kujinusuru na wimbi la kushuka daraja.

Alisema wakati mchakato huo ukiendelea baada ya dirisha dogo la usajili kufunguliwa Jumatatu wiki hii, kwa sasa kikosi chao kinaendelea na maandalizi makali kwa ajili ya kuisubiri KMC FC mwishoni mwa mwezi.

"Maandalizi yanaendelea vizuri kwa ajili ya kukutana na timu ya KMC, tutaingia kwa tahadhari kubwa kuhakikisha tunapata matokeo mazuri nyumbani," alisema Kilao.

Aliwataka wachezaji kujituma kwa kutambua umuhimu wa mchezo huo ili kujiepusha kushuka daraja.

Mwadui ambayo imeshuka dimbani mara 13, ipo nafasi ya 14 ikiwa na pointi 15 huku KMC yenye alama tisa ikiwa nafasi ya 17 baada ya kucheza mechi 11 msimu huu.

# Michezo

Jumatano Desemba 18, 2019

Nipashe



Neymar azikataa rasmi Barca, Real

HABARI UK.30



Kikosi cha Yanga kilichokamilisha ratiba yake ya mechi za kirafiki katika Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani Kigoma Jumapili, kujiandaa na Ligi Kuu. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Uganda inavyoitesa Kili Stars nusu fainali

**Na Adam Fungamwango**

KWA mara nyingine tena, timu ya soka ya Tanzania Bara, Kilimanjaro Stars jana ilitolewa kwenye hatua ya nusu fainali ya michuano ya Chalenji kwa Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati baada ya kuchapwa bao 1-0 kwenye mechi iliyochezwa Uwanja wa KCCA FA nchini Uganda.

Bao lililoendeleza gundu kwa Kili Stars kutolewa kwenye hatua ya nusu fainali kwa mara ya nne tangu 2010, lilifungwa na Fahad Bayo dakika nne kabla ya mechi kumalizika.

Mfungaji aliruka na kuupiga kichwa mpira akiwa yeye na lango, baada ya kipa Matacha Mnata kwenda kuicheza krosi ya Allan Okello ambayo aliikosa na kumkuta mfungaji ambaye hakufanya makosa. Hii ni mara ya tatu kwa Uganda kuifunga Kili Stars kwenye hatua hiyo tangu mwaka 2010.

Baada ya kutwaa Kombe la Challenge kwa mara ya mwisho 2010 kwa kukichapa kikosi cha pili cha Ivory Coast, Kili Stars imekuwa ikikomea hatua ya nusu fainali kila inapofanikiwa kupita hatua za awali.

Mwaka 2011 ilichapwa mabao 3-1 dhidi ya Uganda nchini Tanzania, 2012 ikachapwa tena mabao 3-0 dhidi ya wenyeji Uganda kwenye michuano iliyofanyika 2013, Kili Stars ikachapwa bao 1-0 na wenyeji Kenya, huku mwaka huu ilipigwa tena bao 1-0 dhidi ya wenyeji Uganda.

Katika mechi hiyo, kipa tegemeo, Aishi Manula aliumia dakika ya 34 kwenye harakati ya kuokoa mpira uliokuwa unaingia wavuni na kukanyagwa kichwani na mchezaji mmoja wa Uganda, nafasi yake ikachukuliwa na Mnata.

Kwa matokeo hayo, kesho, Alhamisi Kili Stars itacheza mechi ya kutafuta mshindi wa tatu dhidi ya Kenya ambayo ilichapwa mabao 4-1 dhidi ya Eritrea kwenye mechi nyingine ya nusu fainali, wakati Uganda ikivaana na Waeritrea hao.

# Simba, Yanga rasmi mtoano Mapinduzi

## ●●● Zabadili michuano hiyo kutoka kuchezwa mfumo wa makundi, dimbani baada ya kuvaana Januari 4 kisha...

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya waandaaji wa michuano ya Kombe la Mapinduzi kuridhia kutekeleza masharti yaliyoonekana kuwa "magumu" kwao ili kuzipata Simba na Yanga kwenye kinyang'anyiro hicho, sasa miamba hiyo inaweza kushiriki bila kupepesa macho, imeelezwa.

**Katika mashindano hayo yaliyopangwa kuanza Desemba 31, mwaka huu na kumalizika Januari 13 mwakani, kulikuwa na sintofahamu kuhusu uwezekano wa Simba na Yanga kushiriki kinyang'anyiro hicho hasa kutokana na ratiba ya Ligi Kuu Bara kubana ikiwa ni pamoja na uwapo wa mechi yao ya watani, Januari 4, mwakani.**

Hata hivyo, akizungumza na mwandishi wetu kutoka Uganda, Mwenyekiti wa Bodi ya Ligi Tanzania, Stephen Mguto, alisema moja ya masharti waliyokuwa wamewapa waandaji wa Kombe la Mapinduzi ni kuwataka michuano hiyo kufanyika kwa mtindo wa mtoano badala ya makundi ili kutoa nafasi kwa Ligi Kuu Bara kuendelea jambo ambalo wamelikubali na sasa Simba na Yanga pamoja na bingwa mtetezi, Azam FC zinaweza kushiriki kinyang'anyiro hicho.

Alisema Ligi Kuu haitapanguliwa ikiwa ni pamoja na mechi kati ya Simba na Yanga itakuwa pale pale Januari 4, mwakani katika Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

"Tunaiheshimu sana michuano ya Mapinduzi, ndiyo maana wenzetu tuliwaambia ili timu zetu ziweze kushiriki basi wabadili mfumo na kuchezwa kwa mtoano badala ya makundi jambo ambalo litasaidia timu kuendelea na ratiba nyingine.

"Tunashukuru wametuelewa na kukubali kuchezwa kwa mtindo wa mtoano, hivyo ratiba haitapanguliwa na mechi ya Simba na Yanga itakuwa pale pale Januari 4, mwakani, lakini pia timu zote zitakazoalikwa kwenye michuano hiyo kutoka Bara zinaweza kushiriki," alisema.

Mguto alisema waliwapa taarifa mapema waandaaji mashindano hayo, jambo ambalo wamelifanyia kazi na kuridhia kuchezwa kwa mtindo wa mtoano lakini pia akieleza wameomba ratiba ya Simba na Yanga katika michuano hiyo ianze baada ya Januari 4 watakapocheza mechi yao ya Ligi Kuu.

Alisema mapendekezo ambayo wametoa ni kwa ajili ya kuheshimu umuhimu wa michuano hiyo na kuhakikisha Simba na Yanga zinakwenda Zanzibar kuchuana na hatimaye kutoa fursa kwa mashabiki wao wa visiwani kuwaona wachezaji walioko kwenye vikosi hivyo.

Hata hivyo, baadhi ya mashabiki na wadau wa soka visiwani Zanzibar, licha ya kupokea kwa mikono miwili mabadiliko hayo ya kuchezwa kwa mtindo wa mtoano, wamesema hawataifurahia vizuri michuano hiyo kwa kuwa timu ikitokea kuotewa na kutolewa ndio itakuwa basi tena wakati inapochezwa kwa mtindo wa makundi huweza kuzishuhudia timu zao hatua yote ya makundi.

"Unajua mtoano mara nyingine unaweza kukuta timu unayoishabikia inaotewa na kibonde na kutolewa, hivyo unakosa fursa ya kuendelea kuishuhudia tena kwenye michuano hii, lakini kama ingekuwa kwa mtindo wa makundi unaiona katika hatua nzima," alisema Haji Nassor kutoka Zanzibar.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >